MID WEEK JACKPOT!
TZS. 583,071,860
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



MITAALA MIPYA
**Wadau** wataka mitihani ifutwe, TAMISEMI isiwe inajihusisha masuala ya elimu

UKURASA 3


HOTUBA Jumatatu Mei 15, 2023 Nipashe 9
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya afya
MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2023/24
Ummy A. Mwalimu (Mb) Waziri
Dkt. Godwin Mollel (Mb) Naibu Waziri
Dkt. Grace Magembe Naibu Katibu Mkuu
Dkt. Seif Shekalaghe Katibu Mkuu
Prof. Tumaini Nagu Mganga mkuu wa serikali

UKURASA 9

# Nipashe

Jumatatu Mei 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581311

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



MAZISHI YA MEMBE

# Samia: Nguzo kuu imeondoka

• **Zitto:** Tumepoteza mwanamikakati asiyeogopa... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiaga mwili wa aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Bernard Membe, katika Viwanja vya Karimjee Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 8**

### CPB YATENGA BILIONI 100/- KUNUNUA MAZAO WAKULIMA

BODI ya Wakurugenzi ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imesema inakwenda kufanya mapinduzi makubwa katika mazao na nafaka kwa...



**UKURASA WA 4**

### LE MUTUZ AFARIKI DUNIA

MKURUGENZI wa mtandao wa Lemutuz Tv na blogu maarufu Lemutuz Super Brand, Willium...

**UKURASA WA 18**

### TEMBO NICKEL, JESHI POLISI WAINGIA MKATABA BIL. 1/- KUIMARISHA ULINZI

KAMPUNI ya Tembo Nickel, imeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa zaidi ya Shilingi bilioni moja na Jeshi la Polisi Tanzania, kudumisha ulinzi


## Muhimbili yashtuka ugumba wanaume

UKURASA 18



# Ummy amulika maeneo 14 Afya mwaka 2023/24

Bima ya afya, utafiti vyawekewa mkakati maalum





Kupunguza vifo vya uzazi na watoto wachanga

Ubora wa huduma, dawa na vifaa tiba





Matibabu ya kibingwa na bobezi

UKURASA 9, 10, 11, 12 & 13

**MICHEZO** CAF YABARIKI YANGA FAINALI KWA MKAPA UK.24

**KATUNI** UK.6

# Samia: Nguzo kuu imeanguka

Na Halfani Chusi

RAIS Samia Suluhu Hassan ameongoza mamia ya waombolezaji kuaga mwili wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, aliyefariki Mei 12 mwaka huu baada ya kuugua kwa muda mfupi, akisisitiza "nguzo kuu imeanguka".

Akitoa salamu za rambirambi jana jijini Dar es Salaam wakati wa kuuaga mwili wa Membe, Rais Samia alimtaja alikuwa 'kaka wa karibu' aliyependa kufundisha na kutoa maarifa yake kwa wengine, muungwana, mchapakazi na aliyependa maendeleo ya nchi na wananchi wake, kwa taifa lake na mataifa mengine.

Rais Samia alisema amepokea kwa huzuni na mshtuko mkubwa msiba huo, akieleza "...mimi na familia yangu tunaungana na Watanzania wote kutoa salamu za pole na rambirambi kwa mjane wa marehemu, watoto, ndugu jamaa na wana-Lindi."

Alisema alifanya kazi na Membe katika Baraza la Mawaziri la Serikali ya Awamu ya Nne, Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa muda mrefu.

"Katika mambo ambayo mwanadamu hawezi kujipangia, ni siku ya kuzaliwa na hata kama utakuja kwa njia yoyote ya upasuaji na kwamba daktari atapanga tarehe ya kufanyiwa upasuaji, kama Mungu hakuitaka litatokea jambo utakuja kwa tarehe nyingine. Vilevile, siku ya kufa binadamu hatuwezi kujipangia," alisema.

Alisema kifo hicho kimewagusa wengi ndani na nje ya mipaka kwa kuwa Membe alikuwa mtu mashuhuri na mwanadiplomasia mahiri.

"Ninaelewa machungu ya wanafamilia kufuatia msiba huu, ila msiba huu sio wenu peke yenu. Ni msiba wetu sote ingawa athari na machungu yatakuwa upande wenu kwa kuwa mmeondokewa na mpendwa wenu. Kwa hakika nguzo kuu imeondoka. Ninamwomba Mungu awape subira.

"Kifo chake kimeacha pengo kubwa sio tu katika familia yake, bali kwa Tanzania na mataifa aliyoyafanyia kazi katika kulinda utu na heshima ya mtu. Hakuna anayependa kuondokewa na mpendwa wake, lakini Mungu huchukua amana yake kwa jinsi inavyompendeza," alisema.



Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, akitoa heshima zake za mwisho kwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, marehemu Bernard Membe, katika viunga vya Karimjee jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**ZITTO AFUNGUKA**

Akiwasilisha salamu za pole kwa niaba ya wafuasi na wanachama wa Chama cha ACT-Wazalendo, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema Membe alikuwa mwanasiasa na mwanamikakati wa mfano wa kuigwa.

Alisema alimfahamu mara ya kwanza kwa sifa hiyo mwaka 2005 alipokuwa anapambana kwa ajili ya kupata mgombea atakayemrithi Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

"Kulikuwa na maneno na minong'ono ya chini ya kapeti kuwa mgombea wenu asingeteuliwa mngejiunga nasi tuliokuwa upande wa upinzani. Ni hali ya kawaida kuwa na maneno ya namna hii kila nyakati za uchaguzi.

"Wakati mwingine maneno ya namna hii huwa kweli na wakati mwingine haitokei. Wakati wenu huo haikutokea. Ninadhani kwa sababu mgombea wenu alishinda. "Kitendo chako (Membe) kuja kupaki gari lako mbele ya ofisi ya makao makuu ya chama changu cha wakati huo, na kuzungumza na mmoja wa waliokuwa wabunge wa chama hicho na kumpa salamu za kumletea mwenyekiti wetu, 'kwamba tujiandae mnakwenda Dodoma, demokrasia ikikanyagwa tuwapokee', kilikuwa ni kitendo cha kimkakati mno.

"Hii ni kutokana na ukweli kuwa ulikifanya mchana hadharani, ukijua kuwa ni lazima macho mengi yalikuwa yanakuona. Lengo ni kutengeneza mazingira ya wakubwa wa chama chako kupata ujumbe mahususi uliokusudia.

"Tukio hili kwangu lilikuwa ni mafunzo ya mwanzo ya uanademokrasia na uanamikakati wako. Ni wanasiasa wachache sana wana kipaji cha kukusanya kwa wakati mmoja uanasiasa na uanamipango ya kisiasa. Wewe uliweza kuwa nazo hizo sifa zote."

Kwa mujibu wa Zitto, Membe alikuwa mstari wa mbele kutetea haki za Watanzania wote. Alisema kuwa mwaka 2006 aliisaidia familia iliyoonewa na kupelekwa DRC kwa madai siyo raia hadi wakarejeshwa nchini. Alijali haki za watu zaidi kuliko maslahi finyu ya kisiasa.

Zitto alisema Membe alikuwa mtu mwenye msimamo, hakuogopa kusema lile uliloliamini, ilikuwa fahari kutokubali kutii mambo kwa sababu tu mkubwa kataka na hakujali madhara ya kusimamia hayo.

"Wakati mgumu sana wa maisha yako kisiasa ulikuwa ndio wakati mgumu sana wa kisiasa nchini. Ulisimama na watetezi wa demokrasia na watetezi wa haki za binadamu bila kupepesa macho.

"Ulikuwa nasi kila tulipopata maswahibu kiasi cha kukuingiza wewe mwenyewe kwenye maswahibu uliyokabiliana nayo kwa namna unayojua wewe mwenyewe.

"Mpaka umauti unakufika hukuacha kulionyesha taifa na dunia namna tunapaswa kuhusiana hata kama tunapingana kimawazo na mirengo ya kisiasa," Zitto alifafanua.

Kwa mujibu wa Zitto, Membe alipambana kulinda heshima yake dhidi ya watu waoga ambao badala ya kukabili hoja zake, waliamua kutuma mtu kumchafua pamoja na wote waliokuwa na mawazo mbadala kwa lengo la kuwanyamazisha.

"Kesi yako kupinga kuchafuliwa ulitusemea na sisi wenzako wote. Ulitupigania sisi wote dhidi ya tabia ya ovyo kabisa iliyojitokeza katika nchi yetu. Tabia ya watu wenye mamlaka kutuma wahuni kutukana viongozi wenzao.

"Tabia ya vyombo vya dola, vingine vyombo vya usalama, kuendekeza upuuzi na hata kuwezesha tabia hiyo chafu kabisa. Ni aibu kuwa mitambo ya baadhi ya vyombo vyetu ilitumika kuchapisha mambo ya namna ile.

"Wapo hapa watu ambao walifadhili na kushabikia upuuzi uliopigana kuupinga mpaka mahakamani na ukashinda. Nao eti wanakulilia. Nao eti wanakuaga.

"Ninaamini kifo chako hiki na mazishi yako haya yatazika tabia zile ambazo hukukubali kamwe ziwe sehemu ya utamaduni wetu wa kisiasa. Ninataraji hata katika mioyo yao watu wale watajuta na kukuomba radhi ukiwa kwenye umauti.

"Nilipenda utaratibu uliotumia kujiunga nasi, ukituandikia barua ya kueleza kwa kina kwanini umeichagua ACT Wazalendo, pamoja na mengine, ukituhimiza tusiache kutengeneza mazingira ya kutoa fursa wa kila mwathirika wa siasa na demokrasia kupata nafasi ya kuendelea kufanya siasa kupitia ACT Wazalendo. Tukio hili lilikuwa kilele cha uanademokrasia wako.

"Ulikaa nasi katika ACT Wazalendo kwa muda mfupi sana wa maisha yako ya kisiasa. Lakini muda huo mfupi ulikuwa na mafunzo makubwa sana kwetu. Ucheshi wako uliamsha ari zetu za kazi. Kila jambo lililokuwa linatokea ulikuwa hukosi mfano wa kutupatia kulinganisha mazingira ya sasa na wakati ukiwa ama serikalini au katika majukumu yako ya nje ya nchi."

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax alisema, Membe alikuwa mtu muhimu katika safari yake ya kugombea nafasi ya kuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Binafsi Membe alinitia ujasiri sana wakati taifa langu liliponiteua kwenda kuwania nafasi ya kuwa Katibu Mtendaji wa SADC. Wizara iliyokuwa inatoa mapendekezo ya kuratibu shughuli hii ilikuwa ni ya Mambo ya Nje.

"Tanzania ilionekana kama ni nchi pekee ambayo ingeweza kushika nafasi hii, lakini katika mchakato wa kuwania walijitokeza wahitaji wengi kutoka nchi mbalimbali lakini yeye alisimama akasema 'hatuogopi ushindani'," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa Membe alimwita na kumwambia "tuko nyuma yako, nenda kagombee utashinda". Pia alimsaidia kutekeleza majukumu mengi ya kimataifa kutokana na uzoefu mkubwa aliokuwa nao.

**CHONGOLO**

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo alisema Membe alikuwa mtu mahiri. Chama kimepoteza mtu muhimu aliyekuwa anagusa maslahi ya nchi kwa ujumla. Alisema Membe hakuwa mchoyo wa maarifa pale alipohitajika kuyatoa. Maisha yake ya uongozi ndani ya chama na serikali ameacha mengi mazuri yanayostahili sifa.

Akizungumza kwa niaba ya familia ya Membe, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambaye ni Mbunge wa Mtama anakotokea Membe, Nape Nnauye, alimshukuru Rais Samia kwa mchango mkubwa, ikiwa ni pamoja na kusaidia gharama za kusafirisha mwili.

"Familia inawashukuru wote walioguswa, Wizara ya Mambo ya Nje, uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuungana pamoja tangu alipofikwa na umauti kaka yangu. Pia ninawashukuru madaktari wa Hospitali ya Kairuki kwa jitihada za kujaribu kuokoa maisha yake.

Membe alifariki dunia Mei 12, mwaka huu katika Hospitali ya Kairuki mkoani Dar es Salaam alikokwenda kupata matibabu. Mwili wake unatarajiwa kuzikwa kesho katika Kijiji cha Rondo mkoani Lindi.

# MITAALA MIPYA ELIMU: Wadau wataka mitihani ifutwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa elimu walioshiriki Kongamano la Sera na Mitaala ya Elimu, wametoa mapendekezo kadhaa ikiwamo kufuta mitihani ya kitaifa ya darasa la nne, la sita na kidato cha pili.

Pia wameshauri mtaala uruhusu kumkaririsha darasa mwanafunzi ambaye hatofikia kiwango cha upimaji kitakachowekwa.

Wadau hao pia wameshauri wanafunzi wanaoandaliwa kuwa walimu, wawe na alama za juu za ufaulu ili pindi wanapohitimu wawe na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ya ufundishaji kwa weledi wa kiwango cha juu.

Akitoa mapendekezo wakati wa kongamano hilo jana jijini hapa baada ya kujadiliana katika makundi, Mwalimu Zamoyoni Uzale, alisema mitihani hiyo iondolewe na wanafunzi wasome hadi kidato cha nne moja kwa moja kwa kuwa kipimo cha mitihani kitasababisha wanafunzi washindwe kufikia viwango vinavyotakiwa.

Alisema sera pia iseme usimamizi na uendeshaji wa elimu uwe katika wizara moja kwa kuwa kumekuwapo tatizo la wizara nyingi kusimamia elimu.

"Ninadhani umefika wakati sasa tuwe na wizara moja ambayo inafanya kazi ya usimamizi kuanzia ngazi ya chini na kuendelea na elimu ya awali tunapendekeza iwe ya lazima," alisema.

Mapendekezo ya kundi la viongozi wa serikali na taasisi lililoongozwa na Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Prof. Preksedis Ndomba, ni kwamba sera haijasisitiza vizuri kuwa elimu ya awali ni ya lazima na kupendekeza kuwa kutokana na madhumuni ya elimu hiyo, iwe ya lazima ili watoto wakikutana darasa la kwanza wawe wamepata hiyo elimu.

Alisema kamati hiyo kuhusu elimu ya amali inatoa angalizo kuwa kunawezeka kuwa na elimu ya kikanda na kupunguza mwingiliano uliorithiwa na kushauri tamko liboreshwe.

"Kamati pia inahisi kwenye mikondo ya elimu ya amali kunawezekana wanafunzi kuchangamkia mkondo mmoja. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa tamko la kisera linalotoa uwiano wa idadi ya wanafunzi wa elimu ya amali na jumla," alisema.

Kuhusu ubora wa elimu, Prof. Ndomba alisema wanashauri kuwe na msisitizo na tamko la msingi liseme serikali ihakikishe uwezo wa huduma bora ya maktaba katika hatua ya usajili wa shule, taasisi ya elimu lazima kuwa na huduma hizo na zilizoanzishwa zihakikishe zina huduma hiyo.

Alisema sera haijaeleza umri wa mtoto mwenye ulemavu kuanza shule na kushauri ianishwe vizuri kwa kuwa wanaweza kuanza shule na miaka saba au minane.

Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, alisema wanafunzi kuanzia darasa la saba hadi kidato cha nne wanaonekana wanaishi maisha ya ahueni lakini serikali na wazazi wanateseka kwa watoto waliosoma elimu ya juu.

Mbunge wa Buyungu, Aloyce Kamamba, alishauri iundwe taasisi ya uthibiti ubora wa elimu inayojitegemea ili kukagua ipasavyo elimu nchini.

"Wathibiti ubora ndio jicho la serikali upande wa elimu. Wakifanya kazi vizuri tuna uhakika changamoto zinazoikabili elimu watazibainisha. Zitakuwa wazi na hivyo zitafanyiwa kazi vizuri na kuziboresha," alifafanua.

**MAFUNZO YA AMALI**

Akihitimisha kongamano hilo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema mafunzo ya amali hayatokuwa kwa waliofeli, bali waliofanya vizuri katika masomo yao.

"Niwahakikishie katika mafunzo ya amali, tunataka tusiyafanye watu wakayadharau na ndio maana hasa ya kuanza na vyuo vya ufundi, mafunzo ya amali sio ya waliofeli, bali waliofaulu vizuri," alisema.

Prof. Mkenda alisema wizara itazingatia maoni yaliyotolewa na wadau kwenye kongamano hilo na malengo yaliyopo. Ukusanyaji maoni utaendelea hadi Mei 31 mwaka huu.

"Kuna maoni elimu ya awali iwe ya lazima. Ni suala ambalo hata kamati ya Bunge walisisitiza na sisi tumesema tunalipokea, tunalichakata na kuliangalia. Hatuwezi kusema kwa haraka kwamba litakuwa lazima, lazima tuangalie uwezekano wa utekelezaji," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema wataisimamia serikali ili kutekeleza mambo yaliyomo katika rasimu za sera na mitaala na yaliyoshauriwa na wadau.

"Katika miaka mitano au 10 ijayo, elimu yetu itakuwa imeimarika. Niwatoe shaka elimu ina malengo makubwa mawili. La kwanza ni kuwezesha kujua na pili ni elimu timizi," alisema.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NEEMA ERASTO MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 841 CTJ – SUZUKI CARRY.** Chassis **No. DD51T305044. ENGINE No. F6A1750904.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/146783/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA UMMA**
**KUITWA KUANZA MAFUNZO YA UFUNDI NA STADI ZA KAZI KATIKA FANI MBALIMBALI KWA NJIA YA UANAGENZI**

Itakumbukwa kuwa tarehe **22 Februari, 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (OWM – KVAU)** ilitangaza fursa za mafunzo ambayo yatatolewa katika taasisi za mafunzo zilizotangazwa. Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inapenda kuutaarifu umma kuwa jumla ya vijana 3,765 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo katika vyuo 28 nchini. Majina ya vijana waliochaguliwa yamebandikwa kwenye mbao za matangazo za vyuo husika na katika tovuti ya www.kazi.go.tz. Vijana waliochaguliwa wanatakiwa kuripoti kwenye vyuo hivyo kwa ajili ya kujisajili kuanza mafunzo kuanzia tarehe 15 Mei, 2023. Mafunzo yanayotolewa ni ya kutwa. Mikoa na vyuo husika ni kama ifuatavyo:-

| MKOA | | JINA LA CHUO |
|---|---|---|
| ARUSHA | 1. | CHUO CHA TAIFA CHA UTALII - KAMPASI YA ARUSHA |
| DAR ES SALAAM | 2. | CHUO CHA TAIFA CHA UTALII – BUSTANI KAMPASI |
| DODOMA | 3. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI – MUNGURI – KONDOA |
| | 4. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI – CHISALU - MPWAPWA |
| GEITA | 5. | CHUO CHA VETA - CHATO |
| IRINGA | 6. | IFUNDA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL VTC |
| KAGERA | 7. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI NGARA |
| | 8. | CHUO CHA UFUNDI – KASHOZI VTC |
| KIGOMA | 9. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KIBONDO |
| KILIMANJARO | 10. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SAME |
| MANYARA | 11. | VETA – GOROWA |
| MARA | 12. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KISANGWA |
| | 13. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI TARIME |
| MBEYA | 14. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI NZOVWE |
| | 15. | MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY |
| | 16. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KATUMBA |
| MOROGORO | 17. | CHUO CHA UDZUNGWA UTALII VTC |
| MTWARA | 18. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI NEWALA |
| | 19. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MTAWANYA |
| MWANZA | 20. | CHUO CHA NYAKATO VTC |
| | 21. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI MALYA |
| PWANI | 22. | VIKINDU CATHOLIC POLITECH |
| RUVUMA | 23. | ST. JOSEPH VTC |
| | 24. | CHUO CHA MAENDENDELEO YA WANANCHI MPUTA |
| SHINYANGA | 25. | CHUO CHA UFUNDI ST FRANCIS DE SALES VTC |
| | 26. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI – MWANVA |
| SINGIDA | 27. | CHUO CHA RC MISSION VTC MANYONI |
| TABORA | 28. | CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SIKONGE |

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

World Health Organization

## INVITATION FOR BIDS

The World Health Organization, Country Office for Tanzania is pleased to invite qualified service providers of the below-listed services to participate in the request for bid.

| Bid No. | Service Required | Location | Duration of the Long-Term Agreement |
|---|---|---|---|
| 1 | Supply of Daily Newspapers | Dar es Salaam | 2-year, renewable |
| 2 | Vehicles Maintenance and Repair Services | Dodoma | 2-year, renewable |
| 3 | Vehicles Maintenance and Repair Services | Mwanza | 2-year, renewable |
| 4 | Vehicles Maintenance and Repair Services | Kigoma | 2-year, renewable |
| 5 | Vehicles Maintenance and Repair Services | Iringa | 2-year, renewable |
| 6 | Vehicles Maintenance and Repair Services | Unguja | 2-year, renewable |
| 7 | Vehicles Maintenance and Repair Services | Dar es Salaam | 2-year, renewable |

Interested providers of the above services are required to request detailed ToR documents from the following email addresses **afwcotzremit@who.int and johnsonem@who.int**

The period to request the detailed ToR documents will be between the **16th – 23rd of May 2023.**



Balozi wa Cuba, Humprey Polepole, akizungumza na madaktari bingwa wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) alipokwenda kuwalaki juzi usiku katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana wakitokea Malawi ambako waliweka kambi ya wiki moja kutibu wagonjwa wa moyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Madaktari bingwa JKCI watibu wagonjwa wa moyo 700 Malawi

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI bingwa wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), wamewapatia matibabu ya kibingwa wagonjwa 724 wa moyo Malawi walikoweka kambi ya siku tano.

Matibabu hayo yamefanikiwa chini ya uratibu wa Kamati ya Utalii Tiba inayoongozwa na Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Mohamed Janabi na Makamu wake, Abdulmalik Mollel, ambaye ni Mkurugenzi wa Global Education Link (GEL).

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) baada ya kuwasili jijini Dar es Salaam jana, kiongozi wa msafara wa madaktari hao, Daktari Bingwa wa Maradhi ya Moyo wa JKCI, Angela Muhyoza, alisema kambi hiyo ilifanyika katika Hospitali ya Qeen Elizabeth.

Dk. Muhyoza alisema walikuwa na madaktari bingwa wa watoto wawili na madaktari bingwa wa watu wazima wawili na wataalamu wengine waliokuwa wakiwasaidia madaktari hao.

Alisema kati ya wagonjwa waliowahudumia, 524 waligundulika kuwa na matatizo ya moyo ambapo baadhi yao walipatiwa tiba hapohapo wakati wagonjwa 200 walihitaji huduma za upasuaji mkubwa wa kufungua kifua.

"Miongoni mwa wagonjwa hao, 60 wanahitaji matibabu ya haraka kutokana na matatizo waliyonayo. Kwa hiyo, wasipopata matibabu ndani ya muda huo wanaweza kupata matatizo zaidi. Wananchi wa Malawi wamefurahia huduma zetu na walitamani tuendelee kuwapo nchini kwao," alisema.

Serikali ya Malawi imeishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwapeleka wataalamu wa moyo kwa ajili ya kufanya uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo kwa wananchi wa nchi hiyo.

Shukrani hizo zilitolewa na Waziri wa Afya wa Malawi, Khumbize Chiponda, alipotembelea Hospitali ya Queen Elizabeth kuangalia huduma zilizokuwa zinatolewa na wataalamu wa afya kutoka JKCI wakati wa kambi maalum ya siku tano ya matibabu ya moyo.

Khumbize alisema Malawi na Tanzania wamekubaliana kuwa na ushirikiano katika kujengeana uwezo kwa kuwa nchi hiyo haijaanzisha hospitali ya moyo, hivyo kupitia kambi hiyo wataenda kujitathmini uwezo wao kama wanaweza kuanzisha kituo ambacho kitakuwa kinatoa huduma za matibabu ya kibingwa ya moyo nchini mwao.

"Ndugu zetu Watanzania wapo mbele yetu katika kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya moyo kwa sababu tayari wameshafungua taasisi ambayo inatoa huduma za moyo na imewekeza wataalamu na vifaa vya kutosha. Ninaamini tukiendelea kupata ujuzi kama huu, na sisi tutafungua hospitali ya moyo," alisema Khumbize. Khumbize alisema matibabu ya moyo ni ya gharama. Hadi sasa Malawi ina wagonjwa zaidi ya 500 wenye magonjwa mbalimbali ya moyo wanaosubiria kupelekwa nje ya Malawi kwa ajili ya matibabu.

Akizungumzia kambi hiyo, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kwa Watoto wa JKCI, Parvina Kazaura, alisema katika kambi hiyo walifanya uchunguzi na matibabu ya moyo kwa watu wazima na watoto.

Alisema kila siku watoto zaidi ya 80 walikuwa wakifanyiwa uchunguzi wa moyo na walibaini watoto wengi walikuwa na magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo na wachache kuwa na magonjwa ya moyo waliyoyapata wakati wa ukuaji.

"Kwa bahati mbaya watoto wengi wenye magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo wamekuja wakiwa na umri mkubwa ambapo ilipaswa kufanyiwa upasuaji mapema baada ya kuzaliwa lakini hawakufanyiwa kutokana na huduma hizi kutokuwapo hapa Malawi," alisema.


Tanzania Insurance Brokers Association

**NOTICE OF 14TH TIBA ANNUAL GENERAL MEETING**

*TO: ALL TIBA MEMBERS.*

In terms of section 24.3 of the TIBA Constitution (as amended by the General Meeting on 23rd March 2023), An Annual General Meeting shall be held in the month of May each year.

The Governing Council hereby serves upon TIBA Members a notice for the Annual General Meeting as follows;

**DATE** : Thursday 25th May 2023
**TIME** : From 8.30 AM
**VENUE** : AURA SUITES HOTEL Located at Aura mall building (Morogoro Road at Lumumba Road Junction).

**AGENDA**

1) Opening of the Meeting
2) Adoption of the Agenda
3) Confirmation of the Minutes of the 13th Annual General Meeting
4) Matters arising from Minutes of the 13th Annual General Meeting
5) Approval of the Audited Accounts for 2022
6) Governing Council Report / Report on operations of the association
7) Any other business

All members are kindly requested to attend this meeting as the forum will offer opportunities to discuss a number of issues impacting on our fraternity and members' attendance and contribution is highly welcomed.

**ALIASGHER SOMJI**
**HONORARY SECRETARY**
**12th May 2023**

*1st Floor NIC Building Kisutu*
*Plot No. 9 Block A Olympio Street Upanga*
*P O Box 77042 Dar es Salaam, Tanzania*

*Mobile: +255 677 636 722*
*E-mail: officeadmin@tiba.co.tz*
*Website: www.tiba.co.tz*


# Le Mutuz afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa mtandao wa Lemutuz Tv na blogu maarufu Lemutuz Super Brand, Willium Malecela 'Le Mutuz', amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Taarifa iliyotolewa kwenye mtandao wa Lemutuz Tv asubuhi, ilithitisha kifo cha kiongozi huyo ambaye alikuwa maarufu kutokana na aina ya maudhui kwenye mitandao yake na namna alivyokuwa 'anarusha' picha za watu.

"Uongozi wa Lemutuz Online Tv unadhibitisha kifo cha Mkurugenzi Willium John Malecela (Le Mutuz) kilichotokea mapema leo (jana). Taarifa zaidi zitatolewa," ilisema taarifa hiyo.

Le Mutuz juzi alitoa salamu za pole kwa familia ya aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, aliyefariki siku tatu zilizopita katika Hospitali ya Kairuki, Dar es Salaam.

Le Mutuz aliweka picha yao waliyopiga na kuandika "Rest In Peace Benard Kamilius Membe" huku watu wakitoa pole na jana kwenye ukurasa huo walitoa pole kwa kifo cha aliyeandika ujumbe (Le Mutuz).

Pia alirusha picha yake akiwa eneo la starehe saa chache kabla ya kutangazwa kifo chake.

Hivi karibuni alikuwa mstari wa mbele kupinga ushoga na usagaji kwa kurusha picha za wanaofanya vitendo hivyo kwa lengo la kuwaaibisha ili waache tabia hiyo.

Katika ukurasa huo, hadi kufikia saa nane mchana, zaidi ya watu 1,500 walituma salamu za pole kwa familia na marafiki wa Le Mutuz Superbrand.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Innocent Mtui, aliandika "...pole sana ndugu na wapenzi wa Le Mutuz Super brand, kuna vingi ulituelimisha na kutufundisha ikiwamo jambo la ushoga/kusagana, ndoa za jinsia moja ulipambana nazo siju nani atavaa viatu vyako. Watanzania waendelee kusikia mapambano yako kwa nchi yako pumzika kwa amani kamanda."

Katika ukurasa wake wa Instagram, Innocent Mungy aliandika "...habari hii imeleta majonzi sana kwangu na wote tuliomjua tangu miaka ya 80. Moja ya watu mashuhuri waliotumia social media (mitandao ya kijamii) kuwa sehemu ya maisha yake na walio wengi. Alikuwa supporter (msaada) wa kampeni zilizoendeshwa kwenye Sekta ya Mawasiliano."

# TANGAZO

## POSITION ANNOUNCEMENT
## DIGITAL TOOLS RESEARCH ASSOCIATE
## IITA-TZ2023-R4D-007-NRS-DAR ES SALAAM

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information about IITA.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the vacancy of the **Digital Tools Research Associate.**

**Position Summary:**
The PROSSIVA Digital Tools Research Associate (DRA) will work with the project team of the Programme for Seed System Innovation for Vegetatively propagated crops (VPCs) in Africa (PROSSIVA) from IITA-Mikocheni, Dar es Salaam, Tanzania. The primary research focus for the DRA will be Tanzania, but she/he will also be expected to contribute to PROSSIVA activities in the other project target countries, including Ghana, Rwanda, Tanzania, and Uganda. The DRA will work primarily with the Cross-Cutting Component of the project but will also engage with other Component teams and with the various partner institutions involved in the project.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in **Dar es Salaam, Tanzania.**

**Core Responsibilities:**
1. Provide expertise to the PROSSIVA project in digital tool development, ICT data handling and web page development.
2. Design and run a webpage for PROSSIVA, as a part of the IITA website, and manage the uploading and presentation of PROSSIVA project information on the webpage.
3. Set up a data Dashboard on the PROSSIVA webpage, summarizing progress and key achievements of the project in a graphical and visual manner.
4. Link with the Seed Tracker ICT platform team of IITA-Ibadan to support the scaling of the Seed Tracker application, the enhancement of its features, and the application of its use to all VPC target crops.
5. Work with regulatory partners in East Africa to enhance their use of Seed Tracker and increase their capacity to run the system independently.
6. Provide recommendations on approaches for scaling the application of digital tools for pest/disease identification by regulatory agencies during seed certification.
7. Review the potential for the application of digital tools for the determination of 'true-to-typeness' for VPC varieties being delivered through seed systems of target countries.
8. Work with plant scientist colleagues to compare costs vs benefits in the use of digital tools for seed certification compared with other approaches (visual assessment, molecular diagnostics)
9. Provide recommendations for the development of novel digital tools, including digital marketing approaches, that will serve to enhance the efficiency of VPC seed systems in the target countries of PROSSIVA.
10. Provide training, where required, to project members on how to share their data and how to make the most effective use of the project website and dashboard.
11. Deliver quarterly reports summarizing progress, including metrics quantifying data delivery, ICT tool usage, and access to the project website and dashboard.
12. Perform all other related duties that may be assigned from time to time by the supervisor.

**Qualification, Experience and Key Skills**
- Master's degree in computer science or a closely related subject, preferably including course units and/or a practical project or dissertation work on the application of digital tools to agricultural or rural development.
- Minimum of three years of work and/or research experience following completion of a postgraduate degree
- Have excellent writing and oral communication skills in English for efficient communication with diverse project implementing partners and reporting.
- Practical knowledge of software applications for web development and app creation. At least some coding experience is essential. Some experience of machine learning is preferable. Be proficient in MS-Office (Word, Excel, PowerPoint, Outlook).
- Be well organized, able to multitask and work under pressure to meet deadlines with keen attention to detail.
- Have a positive attitude, strong team spirit and the ability to develop constructive research collaborations with individuals and institutions with a diverse set of backgrounds and geographies.
- The successful candidate should have experience of delivering high quality reports and some examples of successfully completed ICT products.
- A good understanding of opportunities for enhancing rural and/or agricultural development through the deployment of digital tools.

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date: Friday MAY 26th.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

## POSITION ANNOUNCEMENT
## SEED SYSTEMS RESEARCH ASSOCIATE
## IITA-TZ2023-R4D-006-NRS-DAR ES SALAAM

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information about IITA.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the vacancy of the **Seed Systems Research Associate.**

**Position Summary:**
The PROSSIVA Seed Systems Research Associate (SRA) will work with the project team of the Programme for Seed System Innovation for Vegetatively propagated crops (VPCs) in Africa (PROSSIVA) from **IITA- Dar es Salaam, Tanzania**. The primary research focus for the SRA will be Tanzania, but she/he will also be expected to contribute to PROSSIVA activities in the other project target countries in East Africa, including Rwanda and Uganda. The SRA will work primarily with the Cross-Cutting Component of the project but will also engage with other Component teams and with the various partner institutions involved in the project.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position. The incumbent will be based in **Dar es Salaam, Tanzania,** but there will be a requirement for local and international travel.

**Core Responsibilities:**
1. Provide technical and administrative support on implementation of PROSSIVA project activities in East Africa, particularly for the Cross-Cutting Component.
2. Work with the PROSSIVA project team and partners to review VPC seed quality management procedures in target countries and make recommendations for improving current systems.
3. Identify opportunities to improve the application of point-of-care diagnostics for VPC seed systems.
4. Evaluate the potential for the expanded use of decentralized seed quality management systems for VPCs in East Africa, building on current experience from cassava.
5. Support research in East Africa to identify methods to increase participation of informal seed system actors in the formal system.
6. Partner with NGOs to design and implement studies to quantify the benefits of combining multiple VPC crops in small-scale seed businesses.
7. Provide quarterly update reports to the Project Management Team on progress in PROSSIVA seed system development work and compile Cross Cutting Component reports.
8. Analyse and write up research, and work with project colleagues to publish in various formats (reports, blogs, journal publications etc)
9. Assist in building and maintaining good relationships with PROSSIVA partners in Tanzania (TARI and TOSCI) but also in the wider East Africa region (including Rwanda and Uganda). Assure effective linkages with the BASICS-II Project in Tanzania.
10. Perform all other related duties that may be assigned from time to time by the supervisor.

**Qualification, Experience and Key Skills**
- Master's degree in biological or agricultural science, preferably including course units and/or practical experience in crop protection, molecular diagnostics, and agricultural seed systems.
- Minimum of three years of work and/or research experience following completion of a postgraduate degree.
- Have excellent writing and oral communication skills in English for efficient communication with diverse project implementing partners and reporting.
- Be proficient in MS-Office (Word, Excel, PowerPoint, Outlook), and be familiar with teleconferencing applications (such as Zoom and MS Teams), and preferably also in software applications for statistical analysis, such as SAS, SPSS, or R.
- Be well organized, able to multitask and work under pressure to meet deadlines with keen attention to detail.
- Have a positive attitude, strong team spirit and the ability to develop constructive research collaborations with individuals and institutions with a diverse set of backgrounds and geographies.
- The successful candidate will preferably have experience of publishing in peer-reviewed scientific journal articles which are recognized by the Thomson indexing system (https://mjl.clarivate.com/search-results)
- A sound knowledge of agricultural systems in sub-Saharan Africa, preferably also with some experience of working with farmers.

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date: Friday May 26th.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga kamalizeni kazi Afrika Kusini, Watanzania wanataka rekodi CAF

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, Yanga, watashuka katika Uwanja wa Royal Bafokeng uliopo Rustenberg, Afrika Kusini, katika mechi ya mkondo wa pili nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji wao, Marumo Gallants.

Katika mechi ya mkondo wa kwanza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, hivyo kwenye mchezo wa keshokutwa, inahitaji sare yoyote ama kutoruhusu kufungwa zaidi ya bao moja au kupata ushindi wowote, ili kutinga fainali.

Hadi kufika nusu fainali, hiyo ni rekodi kubwa kwa Yanga kuweza kucheza hatua hiyo ya michuano ya CAF ikiwa ni mara ya kwanza tangu klabu hiyo imeanzishwa miaka 88 iliyopita, hivyo kama itafanikiwa kufika fainali, itaendelea kujiwekea rekodi zaidi.

Kwa ujumla, si mashabiki wa Yanga pekee wanaotaka kuona klabu hiyo ikitinga fainali, bali ni Watanzania wote kwa ujumla, wanapenda kuona hilo likitokea kwani haitakuwa heshima kwa timu hiyo pekee bali kwa soka la Tanzania kwa ujumla wake.

Tunasema hivyo hasa tukitambua kwamba mafanikio ya Yanga si tu yataitangaza klabu hiyo, bali soka la Tanzania litazidi kutangazika na kuvutia wachezaji wakubwa na hata wawekezaji zaidi, jambo ambalo litaongeza kipato kwa wachezaji na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Hivyo, ili hilo litokee, juhudi zinahitajika kwa wachezaji wa Yanga, benchi la ufundi na viongozi kwa ujumla kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake ili kwenda kumalizia kazi nzuri waliyoianza tangu kuanza kwa msimu wa michuano hiyo inayoratibiwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Tunaamini Yanga wamejiandaa vizuri na wanaendelea kujiandaa kwenda kupata matokeo chanya ama kulinda ushindi walioupata nyumbani ili kutinga fainali na hata kuchukua ubingwa wa michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tunatambua hautakuwa mchezo rahisi pale katika Uwanja wa Royal Bafokeng, Afrika Kusini, lakini kwa ubora wa Yanga ambao wamekuwa wakiuonyesha katika michuano hiyo nyumbani na ugenini msimu huu, hatuna shaka katika hilo.


Kikubwa ni kila mchezaji kubeba jukumu lake ipasavyo, akitambua kwamba mafanikio katika michuano hiyo si sifa tu kwa klabu, bali pia ni daraja pekee kwake katika kutangaza kipaji chake na kujitafutia soko kwa klabu kubwa nje ya nchi.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba katika michuano hiyo, mawakala wengi hutupia macho hususan kwa klabu zinazofika hatua za juu kama hiyo, jambo ambalo halitashangaza kuona baadhi ya wachezaji wa Yanga wakipata soko kwenda klabu kubwa zaidi baada ya kutamatika kwa mashindano hayo.

Tunaamini katika kipindi hiki kichache kilichobaki, benchi la ufundi la Yanga pamoja na kuendelea kuwapa wachezaji mbinu za kiufundi, lakini pia watakitumia kuwaandaa kisaikolojia ili wakiwa ugenini wasione tofauti yoyote na wacheze kwa kujifurahia mchezo kama wapo vile wakiwa nyumbani bila kujali mchezaji wa 12, ambaye ni mashabiki wa timu mwenyeji.

Nipashe tunaitakia Yanga maandalizi mema na safari njema na matarajio yetu makubwa ni kuona ikirejea nchini na rekodi yao mpya ya kutinga fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Yanga wapuuzeni wapotoshaji wa takwimu na rekodi za soka

Na Adam Fungamwango

**KLABU** ya Yanga juzi ilisherehekea ubingwa wake wa 29, tangu timu hiyo ianzishwe mwaka 1935 jijini Dar es Salaam. Ilifanya hivyo kwa kuifunga Dodoma Jiji FC mabao 4-2, mechi ikichezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Inaendeleza rekodi ya kuwa timu iliyotwaa ubingwa huo mara nyingi zaidi kuliko timu nyingine yoyote. Wakati ikitwaa mara ya 29, Simba inafuata ikichukua ubingwa mara 22 na Mtibwa Sugar ya Morogoro mara mbili.

Hapa tunasema mara 29, licha ya kwamba ligi hiyo imepita kwenye majina na mifumo mbalimbali, ambayo kama wangekuwa wale baadhi ya watu wapotofu wangeanza kuleta sintofahamu ya kuwakanganya watu, na mashabiki wengine wa soka ambao wengi wao ni wa kizazi kipya.

Licha ya kwamba ligi imepita mifumo na majina mbalimbali, lakini haiwezi kuondoa ukweli kuwa ndiyo hiyo hiyo, kama vile Bakari kujiiita Beka, Mohamed kujita Moody ama Mo.

Ilipoanzishwa mwaka 1965 kwa wazo la Kocha wa timu ya Taifa wakati huo, raia wa Yugoslavia, Milan Celebic, mwaka 1964 kwa ajili ya kupata wachezaji wa Taifa Stars kutoka pande zote za nchi badala ya Pwani na Dar es salaam tu, haikuwa kwa mfumo huu wa leo tunaouona.

Awali zilianza timu nane tu na zikawa zinacheza kwa mtindo wa mtoano mwanzo hadi mwisho kama tunavyoona sasa Kombe la FA.

Baadaye timu zilivyokuwa zikiongezeka na msisimko ya ligi yenyewe, timu zikawa zinagawanywa kwa mtindo wa makundi na linachezwa mshindi wa kundi hili anacheza na mshindi wa pili wa kundi lingine hadi timu zinafika fainali na anayeshinda ndiye anakuwa bingwa.

Mfano mzuri kama tunavyoona Kombe la Mapinduzi. Baadaye liliboreshwa na kuanza kuchezwa kwa mtindo wa ligi hii tunayoiona, lakini likianza mwanzo wa mwaka.

Kama vile haitoshi mtindo wa kuanza mwanzo wa mwaka ukabadilika hadi sasa ukawa wa msimu, yaani inaanza mwenzi Agosti au Septemba mpaka mwaka unaofuata, ndiyo tukatoka kuwa na bingwa wa mwaka labda 1973 na kuwa bingwa na msimu 2013/14.

Huku kote ligi hii ilikuwa pia na majina yake ambayo yalikuwa yakibadilishwa. Achilia mbali wadhamini ambao walikuwa wanabadilisha majina ya ligi, lakini ilianza kuitwa Ligi ya Taifa, baadaye Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, baadaye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hakuna yeyote aliyeamka na kusema kwa sababu ilikuwa inabadilishwa mifumo au majina, basi tufute ubingwa ambao Yanga aliupata nyuma wakati mifumo haijabadilishwa, tuanze pale ilipoanza kuitwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hili ndilo linatokea sasa kwa baadhi ya watu ambao wamepata jukwaa la kupasha watu habari, lakini wamekuwa wakipotosha sana.

Mfano mtu anakwambia Simba haikufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, badala yake imefika Klabu Bingwa. Huu ni upotoshaji mkubwa, Hili ni kombe moja tu ambalo limebadilishwa mfumo na majina kama ilivyokuwa ligi yetu.

Wakati inachezwa kwa mfumo wa mtoano mwanzo hadi mwisho iliitwa Klabu Bingwa Afrika, lakini ilipobadilishwa na kuchezwa kwa mfumo huu wa sasa inaitwa Ligi ya Mabingwa. Mwaka 1974, Simba iliingia nusu fainali dhidi ya Mehalla El Kubra ya Misri kwa kutolewa hatua hiyo kwa mikwaju ya penalti.

Upotoshaji mwingine mkubwa ni kulitenganisha Kombe la Shirikisho Afrika na Kombe la Washindi Barani Afrika na Kombe la FA. Yote ni moja tu, ila Shirikisho la Soka Afrika lilikuwa linayabadilisha majina kutokana na sababu mbalimbali mbalimbali, ikiwamo mifumo na wadhamini.

Kwanza liliitwa Kombe la Washindi kuanzia mwaka 1975, hadi mwaka 1992 lilipobadilishwa jina na kuitwa Kombe la CAF, mwaka mmoja baadaye Simba ilifika fainali ikafungwa mabao 2-0 dhidi ya Stella Abidjan, na likabadilishwa tena mwaka 2004 likaitwa Kombe la Shirikisho.

Anapotokea mtu anasema ni makombe mawili tofauti ni wa kupuuzwa.

Ni kama nilivyoeleza kuhusu Ligi Kuu na historia yake. Hakuna tofauti na kilichofanyika kwenye Ligi ya Bongo ni kama ile ya CAF. Ni kubadili mifumo tu na majina.

Utakuwa ni mtu wa ajabu ukisema eti Nuta Jazz, Juwata Jazz, Ottu Jazz na Msondo Ngoma si bendi moja kwa sababu majina ni tofauti.

## TANGAZO

# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

CARING FOR FAMILY ECONOMY

## RIPOTI YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA, 2022

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31/12/2022 | Mwaka Uliopita 31/12/2021 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,611 | 1,799 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,400 | 3,303 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,196 | 6,302 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 416 | 365 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 32,461 | 31,577 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,695 | 1,154 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 35 | 35 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,673 | 1,566 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **48,487** | **46,101** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0.00 | 0.00 |
| 18 | Amana za Wateja | 35,802 | 34,873 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | - | 58 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 0 | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0 | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 747 | 461 |
| 28 | Madeni | 0 | 0 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **36,549** | **35,392** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** | **11,938** | **10,709** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,209 | 10,094 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 17 | 17 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,017 | (766) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 695 | 1,364 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **11,938** | **10,709** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,766 | 3,911 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 809 | 1,435 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| i | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 24.62% | 23.23% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.31% | 11.85% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 92.93% | 94.51% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 68.62% | 71.61% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.73% | 82.17% |
| vi | Ongezeko la Amana | 2.66% | 21.20% |
| vii | Ongezeko la Mali | 5.18% | 16.00% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka sasa 31/12/2022 | Mwaka Uliopita 31/12/2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 6,052 | 5,562 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,244) | (1,277) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba** | **4,808** | **4,285** |
| 4 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (405) | (463) |
| 5 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,071** | **856** |
| | 5.1 Ada na Kamisheni | 843 | 777 |
| | 5.2 Mapato Mengine | 228 | 79 |
| 6 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **4,508** | **3,897** |
| | 6.1 Mishahara na Mafao | 2,442 | 2,080 |
| | 6.2 Gharama za Uendeshaji | 1,686 | 1,586 |
| | 6.3 Uchakavu | 380 | 231 |
| 7 | **Faida /(Hasara) kabla ya kodi** | **966** | **781** |
| 8 | Malipo ya Kodi ya Mapato | 179 | (238) |
| 9 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,145** | **543** |
| 10 | Idadi ya Waajiriwa | 48 | 42 |
| 11 | Mapato kwa Hisa | 11.22% | 5.38% |
| 12 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.42% | 1.27% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9.59% | 5.07% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 63.29% | 60.72% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.43% | 11.30% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka sasa 31/12/2022 | Mwaka Uliopita 31/12/2021 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **966** | **781** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | |
| | - Punguzo/ Ongezeko la tengo katika Mikopo | 405 | 463 |
| | -Punguzo katika gharama za Mali isiyohamishika | 380 | 231 |
| | -Hasara Katika Mali | 0 | 0 |
| | - Mabadiliko akiba ya kisheria | 0 | 0 |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (893) | (2,273) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Wateja | 929 | 6,161 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa za Serikali | 0 | 0 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (185) | (282) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (171) | (908) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (180) | (225) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **1,251** | **3,948** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (487) | (154) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | (75) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | (15) |
| | Mengineyo (bainisha)(Amana za Serikali za mda mrefu) | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(487)** | **(244)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 115 | 1,018 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (460) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (182) | (182) |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(67)** | **376** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tas | 697 | 4,080 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 11,769 | 7,689 |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi la Tengo la Fedha la lazima Benki Kuu | 157 | - |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **12,623** | **11,769** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Ziada Juu ya Hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Ongezeko la Thamani | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **10,094** | **17** | **(766)** | **1,234** | **-** | **30** | **100** | **10,709** |
| Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 115 | - | - | - | - | - | - | 115 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,145 | - | - | - | - | 1,145 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada Juu ya Hisa | - | - | - | - | - | - | (32) | (32) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 638 | (638) | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2022** | **10,209** | **17** | **1,017** | **596** | **-** | **30** | **68** | **11,937** |
| | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita 2021** | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01 .2021** | **9,076** | **17** | **507** | **532** | **-** | **30** | **133** | **10,295** |
| Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 1,018 | - | - | - | - | - | - | 1,018 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 543 | - | - | - | - | 543 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (460) | - | - | - | - | (460) |
| Ziada Juu ya Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (702) | 702 | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ongezeko la thamani | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (654) | - | - | - | (33) | (687) |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2021** | **10,094** | **17** | **(766)** | **1,234** | **-** | **30** | **100** | **10,709** |

**Imesainiwa na:**

| Jina | Cheo |
|---|---|
| Samwel A. Wado: | Ofisa Mtendaji Mkuu |
| Anitha J. Mkeni | Mkaguzi wa Ndani |

Ripoti ya mehesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka ulioishia 31 Disemba, 2022 yameandaliwa kwa kutumia kanuni za mahesabu za kimataifa (IFRS). Ripoti hii ya mahesabu imekaguliwa na **AUDITAX INTERNATIONAL** na kupatiwa hati safi. Taarifa za mahesabu zimeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 12 Mei 2023 na kusainiwa kwa niaba na:-

| Wilson Ndesanjo | Munguatosha Makyao |
|---|---|
| Mwenyekiti wa Bodi | Mkurugenzi |

ACB

*the bank for your development*

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC

**INVITATION TO TENDER**

**TENDER NO: ACB/ADMN/OP/001-2/2023**
**FOR SUPPLY OF GOODS AND PROVISION OF SERVICES**

1. Akiba Commercial Bank PLC is currently inviting sealed bids from all eligible, competent and experienced suppliers to apply for supply of goods and services for year 2023 - 2025 through tendering and pre-qualification of suppliers as listed in the table of this advertisement.

2. Interested suppliers shall obtain Tender and Pre-qualification documents online from Akiba Commercial Bank website: **www.acbbank.co.tz**

3. The list of tendered items and pre-qualification services is here under; you may apply for single applications or more. All existing suppliers and service providers currently operating with Akiba Commercial Bank Plc are also required to apply.

| LOT NO. | A: TENDER FOR SUPPLY OF GOODS AND PROVISION OF SERVICES | QUANTITY |
|---|---|---|
| 1 | SUPPLY OF OFFICE STATIONERIES AND COMPUTER CONSUMABLES | Various |
| 2 | PRINTING AND SUPPLY OF PRINTED BANK FORMS | Various |
| 3 | PROVISION OF OFFICE CLEANING SERVICES | Various |
| 4 | SERVICING OF FIRE EXTINGUISHERS AND OTHER FIRE FIGHTING EQUIPMENTS | Various |
| 5 | SERVICING OF THE STRONGROOM DOORS, EMERGENCE & SECURITY SAFES | Various |
| 6 | PROVISION OF HYGIENE AND SANITARY SERVICES | Various |
| 7 | PROVISION OF FUMIGATION SERVICES | Various |
| 8 | HIRING EMPTY BOTTLES AND SUPPLY OF PURE DRINKING WATER | Various |
| 9 | PROVISION OF SECURITY GUARDS INCLUDING INTRUDER ALARM SYSTEM | Various |
| 10 | SERVICING AND MAINTENANCE OF STANDBY GENERATORS | Various |
| 11 | SERVICE AND MAINTENANCE OF MOTOR VEHICLES | Various |
| 12 | SERVICE AND MAINTENANCE OF AIRCONDITIONS | Various |
| LOT NO. | B: PRE – QUALIFICATION OF SUPPLIERS OF GOODS AND SERVICES | QUANTITY |
| 13 | SUPPLY, SERVICING AND SUPPORT CCTV CAMERA SYSTEM | Various |
| 14 | SUPPLY OF DESKTOP COMPUTERS, LAPTOPS AND OTHER ICT EQUIPMENT | Various |
| 15 | SUPPLY OF OFFICE GROCERIES / SUNDRIES FOR HEAD OFFICE | Various |
| 16 | SERVICING AND MAINTENANCE OF HP SERVERS | Various |
| 17 | SERVICING, MAINTENANCE AND SUPPORT OF INVERTER SYSTEMS | Various |
| 18 | SERVICING AND REPAIR OF PRINTERS AND PHOTOCOPIERS | Various |
| 19 | PROVISION OF BUILDING MAINTANANCE AND REPAIR WORKS | Various |
| 20 | PROVISION OF FURNITURE REPAIRS AND CARPENTRY WORKS | Various |
| 21 | PROVISION OF MARKETING AND ADVERTISING AGENCY SERVICES | Various |
| 22 | PROVISION OF SIGNAGE AND BRANDING ACTIVITIES | Various |
| 23 | PRODUCTION OF BANK PROMOTIONAL MATERIALS | Various |
| 24 | PROVISION OF WEBSITE DEVELOPMENT AND HOSTING SERVICES | Various |
| 25 | PROVISION OF CONSULTANCY SERVICES FOR CUSTOMER SATISFACTION SURVEY | Various |
| 26 | PROVISION OF ELECTICAL WORK SERVICES | Various |
| 27 | PROVISION OF PROPERTY VALUATION SERVICES | Various |
| 28 | PROVISION OF AUCTIONING AND DEBT COLLECTION SERVICES | Various |
| 29 | PROVISION OF ASSET TRACING/ INVESTIGATION SERVICES | Various |
| 30 | PROVISION OF EXTERNAL AUDITING SERVICES | Annually |
| 31 | PROVISION OF TAX ADVISORY SERVICES | Annually |

4. A complete set of the Tender documents shall be submitted in hardcopy to the address below and upon payment of non-refundable fee of TZS 50,000/= (Tanzania Shillings Fifty Thousand only) for each Lot applied. Payment should be made at Akiba Commercial Bank Plc, Main Branch, Amani Place Building, Ohio Street, Dar es Salaam, Head office control A/C No. TZS 1485800010100.

5. Original Tender plus a copy, properly filled in and enclosed in a plain wax sealed envelope should be addressed to the Secretary, Tender Committee, Akiba Commercial Bank Plc, P. O. Box 669 Dar Es Salaam. All tenders may either be delivered by hand to the Tender Committee Secretary, 3rd Floor, Amani Place Building, Ohio Street or by registered post so as to reach the ACB Tender Box before the submission deadline of the tenders.

6. The deadline for submission of bids is Friday, 2nd June 2023 at 10.00 am. Tenders will be opened soon thereafter at Akiba Commercial Bank Boardroom located at 3rd Floor, Amani Place Building, Ohio Street Dar es Salaam in the presence of the bidders or their representatives who may wish to attend.

**THE SECRETARY**
**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC., TENDER COMMITTEE,**
**P.O.BOX 669,**
**DAR ES SALAAM**

# CPB yatenga bilioni 100/- za kununua mazao ya wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BODI ya Wakurugenzi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imesema inakwenda kufanya mapinduzi makubwa katika mazao na nafaka kwa ujumla kwa kutenga Sh. billioni 100 kwa ajili ya ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima nchini.

Bodi hiyo pia imetangaza fursa kwa wakulima wote nchini kulima mazao mengi msimu huu kwa kuwa inakwenda kuyanunua kwa wingi na kwa bei ya soko.

Mwishoni mwa wiki baada ya ziara ya bodi hiyo kutembelea miradi ya Kanda ya Ziwa, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, aliyezungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Kapenjama Ndile, alisema wanakwenda kufanya mapinduzi makubwa ambayo hayajawahi kutokea.

"Tunakwenda kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya mazao na nafaka kwa ujumla. Tunakwenda kununua mazao ya zaidi ya Sh. billioni 100 kutoka kwa wakulima nchini," alisema Ndile.

Aliwataka wakulima nchini wazalishe mazao mengi kwa kuwa CPB itanunua mazao hayo kwa bei ya soko. Inatoa fursa kwa Watanzania kuuza mazao yao katika bodi hiyo ili wajikwamue kiuchumi.

"CPB ni kimbilio kwa wakulima. Tunanunua mazao kutoka kwao. Tunaongeza mazao thamani kwa kuchakata mazao kupitia viwanda vyetu vilivyoko katika baadhi ya mikoa," alisema.

Aliongeza kuwa kipaumbele cha kwanza ni chakula na usalama wa chakula, ndiyo maana serikali iliunda bodi hiyo ili kuwe na usalama wa chakula.

Ndile alisema bodi hiyo inaendelea kujenga viwanda kikiwamo cha kuchakata muhogo kitakachojengwa katika Jiji la Mwanza na kingine kitajengwa Handeni mkoani Tanga.

Alisema wataendelea kupanua viwanda vilivyopo na kuajiri wataalamu wa viwandani kwa lengo la kupanua wigo wa uzalishaji ili wauze bidhaa ndani na nje ya nchi.

"Tuna viwanda vingine vilivyomo Arusha ambapo kuna kiwanda cha kuchakata mahindi na ngano. Kiwanda kingine kipo Iringa kinachakata mhindi. Cha Dodoma kinachakata mahindi na alizeti," alisema Linde.

Mjumbe wa Bodi hiyo, Fadhili Ngajilo, alisema bodi hiyo imepania kuleta mabadiliko makubwa kwa Watanzania kwa kufungua milango ya biashara.

# Waziri aingia mtaani kufuatilia utekelezaji wa maelekezo yake

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameingia katika Mtaa wa Ndachi jijini Dodoma kuangalia utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa kwa idara za ardhi nchini kuhakikisha zinawafuata wananchi angalau mara mbili kwa wiki kwa lengo la kutoa huduma za sekta ya ardhi.

Dk. Mabula alifanya ukaguzi huo mwishoni mwa wiki katika eneo hilo la Ndachi. Ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa wizara kuhakikisha huduma za sekta ya ardhi zinasogezwa karibu na wananchi badala ya huduma hizo kupatikana ofisini pekee.

Mbali na juhudi hizo, kwa sasa Wizara ya Ardhi inabadilisha mifumo yake kutoka analogia kwenda digitali. Moja ya hatua kubwa zilizofikiwa ni utaratibu wa kuwapelekea wamiliki wa ardhi ankara za malipo kupitia ujumbe wa simu za kiganjani. Katika ukaguzi huo, Dk. Mabula alianzia ziara yake Ofisi ya Mtendaji Kata iliyopo eneo la Ndachi Boda. Aliwakuta watendaji wa sekta ya ardhi kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma wakitoa huduma kama alivyoelekeza.

"Nimekuja kuangalia kuona maelekezo yangu kuwa badala ya wananchi kwenda kila mara ofisi za jiji kupata huduma, basi ofisi hiyo ipange walau mara mbili kwa wiki kwenda katika mitaa kusikiliza changamoto za ardhi. Nimekuja hapa kuangalia kuona kama hilo limetekelezwa," alisema Dk. Mabula.

Waziri huyo, akiwa katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Ndachi, alipata malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wakidai kuna mtu aliyemilikishwa kiwanja eneo la Ndachi Mnadani kwa maelezo kuwa kimetokea kwenye shamba lake, jambo walilodai siyo kweli.

Kufuatia hali hiyo, Dk. Mabula aliongozana na walalamikaji pamoja na wananchi wengine kwenda kuliona eneo la shamba hilo. Akiwa katika eneo hilo, walalamikaji walidai mmiliki huyo alipatiwa eneo hilo kiulaghai kwa kushirikiana na baadhi ya watendaji wa jiji.

Kufuatia madai hayo, Dk. Mabula alimpigia simu Mkuu wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Maduhu Ilanga na kuweka sauti kubwa ili wananchi wasikie moja kwa moja. Mkuu huyo wa idara alieleza utaratibu mzima uliotumika hadi mdaiwa kumilikishwa, pamoja na mgogoro uliopo katika eneo hilo.

Mkazi wa Ndachi, Joel Said Katala, alimweleza Waziri wa Ardhi kuwa Dodoma ina changamoto kubwa hasa Halmashauri Jiji la Dodoma kutokana na watendaji wake kutosimamia ukweli na kuangamiza wananchi huku wakijua ukweli. Alisema watendaji hao hutengeneza uongo kwa sababu wao ni wa mwisho kuzungumza na viongozi.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Shaban Haruna, alisema changamoto ya eneo linalolalamikiwa imetokana na serikali kutangaza kuwapo mabadiliko katika eneo hilo kutoka mashamba kuwa makazi huku wananchi wakiwa tayari walishaanza kuishi. Alisema Mkuu wa Wilaya ya Dodoma tayari ameshaunda kamati itakayoshughulikia umilikishaji kwenye maeneo hayo.

Salum Juma, Mwenyekiti wa Shina Namba Moja eneo la Ndachi Mnadani, alisema kuwa katika mchakato mzima wa utwaaji shamba alilomilikishwa mlalamikiwa, kamati inayosimamia suala hilo haijahusishwa. Alisema mchakato unatia shaka.

Baada ya kupata maelezo kuhusiana na mgogoro huo, Dk. Mabula aliwaeleza wananchi kuwa, pamoja na wizara yake kupitia Idara ya Ardhi Jiji la Dodoma kuwafuata wananchi katika maeneo yao, migogoro ya ardhi itaisha tu iwapo wananchi watazingatia sheria, kanuni na taratibu na kuacha kuwa na haraka kujenga nyumba bila kuwa na vibali.

"Sasa hivi Jiji la Dodoma linakua kwa kasi na fursa zipo nyingi na watu wanakimbilia. Kuweni na subira katika ujenzi. Fuateni taratibu," aliagiza.

Waziri huyo alielekeza ujenzi unaoendelea eneo linalolalamikiwa kusitishwa hadi ufumbuzi wa mgogoro wa eneo hilo utakapopatikana.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Wizara ya afya**

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2023/24



Ummy A. Mwalimu (Mb)
**Waziri**

Dkt. Godwin Mollel (Mb)
**Naibu Waziri**

Dkt. Grace Magembe
**Naibu Katibu Mkuu**

Dkt. Seif Shekalaghe
**Katibu Mkuu**

Prof.Tumaini Nagu
**Mganga mkuu wa serikali**

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2023/24

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Afya, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/23 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2023/24.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Afya, sekta ambayo inayogusa maisha ya kila siku ya kila mtu, mwanamke au mwanaume, kijana au mzee, tajiri au masikini kwani Mtu ni Afya na Afya ni Mtaji. Ninatambua jukumu kubwa nililonalo mimi pamoja na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitaendelea kuifanya kazi hii kwa weledi, uaminifu na ubunifu mkubwa ili kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora za Afya. Vilevile, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutupatia rasilimali fedha ili kuimarishaji utoaji wa huduma bora za afya nchini ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya afya katika Halmashauri na Mikoa yote nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa Bobezi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa. Deni sasa limebaki kwetu Sekta ya Afya kwa kuhakikisha tunatoa huduma bora za afya kwa wananchi wetu kwa kuzingatia weledi, maadili na miiko ya kitaaluma ya watoa huduma za afya sambamba na kuzingatia kutoa huduma nzuri kwa mteja (good customer care), matumizi ya lugha ya staha na ya Faraja kwa wateja wetu. Tumuhakikishie Mheshimiwa Rais, waheshimiwa wabunge na watanzania kuwa nasi hatutalala, tutatanya kazi usiku na mchana katika kupambana na adui maradhi ili kuhahakikisha wananchi wanapata huduma bora za kinga na tiba na kwa gharama nafuu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wake wa kuboresha huduma za afya nchini hususani kwa wananchi wa maeneo ya Vijijini. Nitumie fursa hii pia kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na maelekezo yake ya mara kwa mara ya kuhakikisha tunaimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya nchini kuanzia ngazi ya Msingi hadi Taifa. Aidha, ninampongeza kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 5 Aprili, 2023 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2023/24.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi **Mheshimiwa Spika** kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa weledi, ubunifu na kwa uadilifu mkubwa, lakini pia kwa kuzingatia na kusimamia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge lako tukufu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Aidha nampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu**, **Naibu Spika** na **Wenyeviti wa Bunge** kwa kazi nzuri ya kukusaidia kuliongoza Bunge letu pamoja na kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge. Tunapenda kukuhakikishia kuwa uongozi na watumishi wa Wizara ya Afya tutakeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia Sheria na Kanuni mbalimbali zinazopitishwa na Bunge lako tukufu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao umeiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki** na Makamu wake, **Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile**, **Mbunge wa Kigamboni** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara hususani katika kipindi cha maandalizi ya bajeti hii. Aidha, ninawashukuru waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa wananchi. Kipekee ninawashukuru sana waheshimiwa wabunge kwa jitihada binafsi mnazofanya ili kutatua chhangamoto za upatikanaji wa huduma za afya katika majimbo yenu ikiwemo kuchangia ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Wizara yangu itaendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zenu za kuwatumikia Wananchi ndani na nje ya Bunge.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi kwa **Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa **Jimbo la Amani – Zanzibar**. Aidha, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa Familia na Wananchi wa Jimbo la Amani - Zanzibar kwa kifo cha **Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar**.** Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee natoa pole kwa familia na jumuiya ya wataalam wa afya nchini kwa kupoteza wataalam mbalimbali wakati wakitimiza wajibu wao wa kuhudumia wananchi. MUNGU azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Pamoja na kupoteza baadhi ya wataalam wa afya wakati wa kutoa huduma, natoa pongezi na shukrani za pekee kwa wataalam wote wa afya nchini hususan waliokuwa mstari wa mbele kutoa huduma kwa wahisiwa na wagonjwa wa Marburg mkoani Kagera, kuhudumia wagonjwa mahututi na wagonjwa wengine kwa ujumla usiku na mchana bila kuchoka.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/23, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24. **Kama inavyoonekana kwenye kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 6 hadi 186**

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23**

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 622,986,024,980.00** Hadi kufikia Machi, 2023, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekusanya jumla ya kiasi cha Shilingi **435,074,652,838.23** sawa na **asilimia 70** ya lengo.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **Shilingi 1,109,421,722,000.00** ili kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2023, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha Shilingi **742,905,741,100.11** sawa na **asilimia 67** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, kiasi cha Shilingi **458,486,800,216.86** sawa na **asilimia 83** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **284,418,940,883.25** sawa na **asilimia 51** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. **Taarifa za kina zimeainishwa kuanzia ukurasa wa 7 hadi 10 na kiambatisho namba 1 hadi namba 3 katika hotuba yangu**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea kiasi cha **shilingi 77,209,210,120.00** kupitia mfumo wa *D-Fund* kwa ajili ya **utekelezaji wa miradi misonge UKIMWI, TB, Malaria, UVIKO 19, Chanjo za watoto afya ya mama na mtoto.** Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni **68.6** kutoka Mfuko wa Dunia "*Global Fund*", Shilingi bilioni **5.8** kupitia *Susan Thompson Buffer Foundation*, Shilingi bilioni **2** kupitia *BADEA-COVID 19 Response grant* na Shilingi milioni **192.6** kupitia *Global Alliance of Vaccine (GAVI)* kwa ajili ya huduma za Chanjo.

**13.** **Mheshimiwa Spika,** maelezo zaidi kuhusu kazi muhimu zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, zimeainishwa **kuanzia ukurasa wa 10 mpaka ukurasa wa 186 wa Hotuba yangu.** Kwa kuwa taarifa hiyo ni ndefu ikilinganishwa na muda uliopo, naomba uridhie niwapitishe katika baadhi ya maeneo machache kama ifuatavyo;

**HUDUMA ZA KINGA**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha **huduma za chanjo** na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana kulingana na mahitaji ya Mikoa yote nchini. Chanjo zinazotolewa ni kwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, wajawazito na wasichana wenye umri wa miaka 14. Aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa chanjo na vifaa vya kutolea chanjo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 vinapatikana.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia mwezi Machi 2023 jumla ya **watoto 1,596,951** sawa na **asilimia 98.6** walikuwa wamechanjwa **chanjo ya Penta3** kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha chanjo ikilinganishwa na **asilimia 94.6** mwaka 2021/22.

**16.** Kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 jumla ya **Wasichana 535,708** wamepatiwa **chanjo ya kuzuia Saratani ya mlango wa kizazi (HPV) Huduma za Lishe**

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha huduma za lishe kwa Watoto kwa kuendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa matone ya Vitamini A kwa Watoto walio chini ya miaka mitano. Malengo ya kampeni yalikuwa ni kutoa matone ya Vitamin A kwa **watoto 9,460,369** wenye umri wa kati ya miezi 6 mpaka 59 nchi nzima. Jumla ya **watoto 9,456,436** walipatiwa matone ya vitamin A ambayo ni sawa na **asilimia 99** ya lengo

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha masuala ya lishe yanatekelezwa na kusimamiwa vizuri katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji, kwa mara nyingine **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **ametia saini Mikataba ya Lishe na Wakuu wa Mikoa** yote Tanzania Bara tarehe 30 Septemba, 2022. Utekelezaji wa mikataba hiyo hupimwa kwa kuangalia viashiria 15 vinavyopima ufanisi wa mkoa husika. Hatua ya Mhe Rais kusaini kwa mara ya pili mikataba ya lishe na wakuu wa mikoa, inaonyesha utashi, uongozi na dhamira yake ya dhati ya kuboresha hali ya Lishe kwa watanzania hususan Watoto, vijana na wanawake wa umri wa kuzaa. **Ukurasa wa 15 hadi 19 wa hotuba yangu**

**AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma kabla ya kujifungua ambapo, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Serikali kwa kushirikiana na wadau ilitoa elimu ya uzazi wa mpango pamoja na kununua na kusambaza **bidhaa za uzazi wa mpango** ikiwemo vidonge vya uzazi wa mpango, sindano za uzazi wa mpango na vipandikizi ambapo katika kipindi cha taarifa hii jumla ya wateja 4,509,605 walitumia njia mbalimbali za kisasa za uzazi wa mpango ikilinganishwa na wateja 4,905,854 kipindi kama hicho mwaka 2021/2022

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya wakati wa ujauzito** kwa kuhakikisha elimu inatolewa kuanzia ngazi ya jamii kuhusiana na umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki kama inavyoainishwa katika Mwongozo wa Huduma za Kliniki kwa Wajawazito wa Mwaka 2018 Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, takwimu za MTUHA zinaonyesha kuwa, **jumla ya wajawazito 2,028,151** sawa na asilimia 98 walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza, ikilinganishwa na wajawazito 1,572,778 sawa na asilimia 86 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. ***Nitumie fursa hii kuwahimiza akinamama wajawazito kuwahi kuanza kliniki mapema ili kutambua mimba zilizo salama na zile zenye matatizo kama kutunga nje ya kizazi, kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana toka mimba ikiwa changa ikiwemo vipimo, matumizi ya dawa kinga kama foliki asidi inayokinga tatizo la kuzaliwa na mgongo wazi.***

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Upande wa **huduma za wakati na baada ya kujifungua** kwa kutumia takwimu za Mfumo wa Taarifa za Utoaji wa Huduma za Afya (MTUHA) zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **Wajawazito 1,500,404** walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya **ikilinganishwa na wajawazito 1,403,761** katika kipindi cha mwaka 2021/22. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Takwimu za MTUHA zinaonesha kuwa **jumla ya vifo 943** vitokanavyo na uzazi vilitolewa taarifa ikilinganishwa na **vifo 982** kipindi cha mwaka 2021/22. Hata hivyo Takwimu rasmi ya vifo vya wajawazito zitatolewa Rasmi na Taasisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) baada ya kukamilisha kazi ya kuchakata taarifa zilizokusanywa nchi nzima mwaka 2022

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma kwa Watoto wachanga** ambapo matokeo ya utafiti wa Viashiria vya Afya ya Uzazi na Mtoto "TDHS 2022" ya mwaka 2022 inaonesha kuwa vifo vya watoto wachanga ni 24 kwa vizazi hai 1,000 Matokeo haya yanatuonesha umuhimu wa Serikali kuongeza nguvu zaidi katika kupunguza vifo vya watoto wachanga ili kufikia lengo la Kimataifa la kupunguza vifo vya watoto wachanga kufikia 12 kwa vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030. Kwa kutambua kuwa baadhi ya wodi za wachanga zilikuwa na upungufu wa vifaa muhimu vya kutolea huduma, Wizara imenunua vifaa tiba vya huduma za watoto wachanga wagonjwa wakiwemo mahututi na njiti vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 6.3** ambavyo katika awamu ya kwanza vitasambazwa kwenye vituo **120** vya kutoa huduma za afya. **Kiambatisho na. 4 na 5.**

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia **huduma za afya kwa watoto walio chini ya miaka mitano.** Kwa mujibu wa Takwimu za TDHS 2022 vifo vya watoto umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kwa asilimia 23 kutoka vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 vya mwaka 2016 hadi vifo 33 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022. Aidha, vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2022. Mafanikio haya ni matokeo ya kuimarika kwa huduma za chanjo, udhibiti na Matibabu ya Magonjwa ya Watoto kwa uwiano

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilinunua na kusambaza dawa kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa **homa ya mapafu (Nimonia)** ya kidonge myeyuko cha **Amoxicillin** vidonge milioni 30.1, na dozi 94,300 za **Zinki na ORS** kwa ajili ya **matibabu ya kuharisha**. Ununuzi wa dawa hizi uliwezesha kuimarika kwa upatikanaji wa dawa za watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika vituo vya kutolea huduma kwa asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 85.3 katika kipindi hicho mwaka 2022. ***Naomba kutumia fursa hii kusisitiza kuwamba dawa za kidonge myeyuko cha Amoxicillin,Zinki na ORS kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, zinanunuliwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau na dawa hizi hazipaswi kuuzwa. Hivyo, nawaelekeza Waganga wakuu wa Mikoa na Halmashauri wasimamie suala hili kwa ukamilifu.***

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kuboresha **huduma za afya ya uzazi kwa kundi la vijana** ikiwemo kuongeza na kuimarisha **vituo vya huduma rafiki** za Afya ya uzazi kwa vijana kutoka **215** mwaka 2021 hadi **901** Machi 2023. Katika Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Serikali iliweza kutoa elimu kwa watoa huduma 750 kuhusu namna ya kutoa huduma rafiki kwa vijana kwa masuala ya afya ya uzazi.

**MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuboresha afua mbalimbali za **kudhibiti maambukizi ya VVU/UKIMWI, Homa ya Ini, Malaria na Kifua kikuu** ikiwemo kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi, kutoa huduma za ushauri na upimaji, matunzo na huduma za dawa. Kwa upande wa udhibiti wa maambukizi ya VVU/UKIMWI hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya **wateja 1,632,328** sawa na **asilimia 94.4** ya watu 1,729,408 wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI nchini walikuwa **wanatambua hali zao za maambukizi** (95 ya kwanza). Kati yao **wateja 1,612,520** walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, ambapo watoto walikuwa ni 58,760. Idadi hii ya wagonjwa walio katika **matumizi ya dawa** za kufubaza Virusi vya UKIMWI ni **asilimia 98.8** ya watu wanaotambua hali zao za maambukizi (95 ya pili). Aidha, Jumla ya vipimo 309,263 vya kujua wingi wa Virusi vya UKIMWI kwa wagonjwa walioanza kutumia dawa vilifanyika na kati ya vipimo hivyo, vipimo 298,657 ambavyo ni sawa na **asilimia 96.6** vimeonesha kuwa wagonjwa hawa wa**mefubaza** Virusi vya UKIMWI (95 ya tatu) **Ukurasa wa 40 hadi 53 wa hotuba yangu**

**HUDUMA ZA TIBA**

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya nchini zinazotolewa kupitia Vituo vya kutolea huduma vya Serikali, binafsi na mashirika ya Dini. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kufikia **jumla ya vituo 11,040** ikilinganishwa na vituo **8,549** mwaka 2021. Kati ya hivyo, Hospitali zilikuwa 430, Vituo vya afya vilikuwa 1,030, Zahanati

zilikuwa 7,458, Kliniki zilikuwa 906 na Maabara Binafsi 1,216

**Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na vifaa tiba**

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bohari ya Dawa hununua, hutunza na husambaza zaidi ya aina **2,976 za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.** Kati ya hizo **aina 290 zimeainishwa kuwa ni dawa muhimu** na za kipaumbele cha Wizara ya Afya kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinapatikana nyakati zote katika Bohari ya Dawa (MSD). Aidha, hadi sasa, Wizara ya Afya imeshapokea na kupeleka MSD kiasi cha **shilingi bilioni 159.9** sawa na **asilimia 80** ya bajeti ya shilingi Bilioni 200 iliyoidhinishwa na Bunge lako kwa ajili ya ugharamiaji wa mnyororo mzima wa upatikanaji wa bidhaa za afya. Katika hili tunampongeza na kumshukuru sana Mhe Rais

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, kupatikana kwa fedha hizi kumewezesha upatikanaji wa bidhaa za afya za kipaumbele **aina 290** kuongezeka kutoka wastani wa **asilimia 52.4** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi kufikia wastani wa **asilimia 73** katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya (Zahanati asilimia 52, Vituo vya Afya asilimia 57), Hospitali za Wilaya asilimia 67, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 98 na Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa ni asilimia 94.

**Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha **huduma za uchunguzi wa Magonjwa** katika vituo vya kutolea huduma za afyaambapo jumla ya mashine za **MRI sita (6)** kwa gharama ya **shilingi 14,534,624,000. k**ati ya hizo mashine nne (4) zimeshasimikwa na kuanza kutoa huduma katika Hospitali ya Taifa-MNH, Hospitali ya Taifa ya Saratani-Ocean Road, **Hospitali ya kanda-CHATO** na **Hospitali ya kanda-MTWARA**. Usimikaji wa mashine mbili (2) za MRI unatarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 30 June 2023 katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya na hospitali ya MOI.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha ununuzi wa **mashine za CT scan 32** zenye gharama ya **shilingi 56,465,145,570,** ambapo **CT Scan 24** tayari zimeanza kufanya kazi katika Hospitali za Taifa, Kanda na Hospitali Rufaa za Mikoa 24 ikiwemo Kagera, Maweni-Kigoma, Iringa, Dodoma, Shinyanga, Morogoro, Tumbi-Pwani, Singida, Mount Meru-Arusha, Mwananyamala, Amana, Temeke, Hospitali Mzena (DSM), Bombo-Tanga, Sokou Toure-Mwanza, Mawenzi-Kilimanjaro, Manyara, Kitete-Tabora, Geita, Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Njombe na Simiyu na taratibu za usimikaji CT Scan 8 zinaendelea. Ununuzi wa mashine hizi umewezesha kuimarika kwa huduma za Radiolojia kwa kuwa na mashine za CT Scan 45 nchi nzima kutoka 13 mwaka 2021. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI iliratibu ununuzi wa **Digital X-Ray 199** zenye gharama **ya shilingi 44,680,031,171** ambapo Digital X-Ray 168 zimeshasimikwa katika vituo mbalimbali zinaendelea kutoa huduma, usimikaji wa Digital X-Ray 31 bado unaendelea na utakapokamilika utawezesha Sekta ya afya kuwa na jumla ya **Digital X-Ray 346.** Aidha, mashine za **Ultrasound 76** zenye gharama ya **shilingi 4,695,000,000** zimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Ongezeko hili la ultrasound machine 76 linafanya sekta ya afya kuwa na jumla ya **mashine za Ultrasound 552 kutoka 476 mwaka 2021/22.** ***Lengo la kuboresha huduma za uchunguzi na utambuzi wa magonjwa kuanzia ngazi ya msingi hadi Taifa ni kuimarisha huduma za matibabu sahihi kwa wagonjwa na kuzisogeza karibu zaidi na wananchi***. **Ukurasa wa 60 hadi 63 wa hotuba yangu**

**UTOAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU**

**32.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kusimamia **utoaji wa huduma za matibabu** kwa wananchi ambapo, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya **Wagonjwa 35,873,466** walipatiwa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikilinganishwa na wagonjwa 33,688,803 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Aidha, wagonjwa walioonwa katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa walikuwa Wagonjwa 2,529,971 sawa na asilimia 7.1 na wagonjwa 31,075,478 sawa na asilimia 86.6 walipata huduma katika ngazi ya Msingi *(Primary health Care)* Takwimu hizi zinaonesha huduma za afya zimezidi kusogezwa karibu na wananchi na kuboreshwa. Jedwali namba 4 ukurasa wa 65 katika hotuba yangu

**33.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 **magonjwa yaliyoongoza katika kuwaathiri zaidi wananchi** na kuwasababishia kwenda katika vituo vya huduma kupata matibabu ni maambukizi katika mfumo wa hewa, Maambukizi ya njia ya mkojo, na Malaria. Aidha, **magonjwa yaliyoongoza Kulazwa** ni Malaria, Homa ya Mapafu, na Anemia. Aidha, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa ndani ya magonjwa kumi yaliyoongoza. **Taarifa ya kina inapatikana katika ukurasa wa 66 hadi 68 na kiambatisho namba 6 hadi 9 katika Hotuba yangu.**

**Huduma za Wagonjwa wa Dharura na Ajali**

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kukamilisha ujenzi wa **majengo 23** ya kutoa **huduma za dharura (EMD)** katika Hospitali Maalum, Kanda na Mikoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya EMD 15 zilikuwa zimekamilika na zimeanza kutoa huduma. Kukamilika kwa ujenzi wa EMD kumeongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, maalumu, na kanda zinazotoa huduma hiyo kutoka nane **(8)** mwaka 2021 na kufikia **38** kipindi cha mwezi Machi 2023. Aidha, Serikali ya awamu ya sita kupitia OR-TAMISEMI imewezesha ujenzi wa majengo ya **EMD 80 katika ngazi ya Hospitali za Halmashauri.** Jumla ya majengo yakutoa **huduma za dharura (**EMD) yamefikia **118 kutoka 8** mwaka 2021. ***Haya ni mapinduzi makubwa katika Sekta ya Afya hapa Tanzania tangu uhuru kwa Serikali kuweka mfumo madhubuti wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya. Matokeo ya uwezekaji huu yatapunguza vifo ndani ya Hospitali kwa asilimia 40 na kuokoa maisha ya wananchi wanaohitaji huduma za dharura***.

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kukamilisha ujenzi wa **wodi 45** kwa ajili ya **wagonjwa mahututi na wanaohitaji uangalizi maalum (ICU)** katika Hospitali ngazi ya Taifa, Maalum, Kanda na Mkoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba, ambapo hadi kufikia Machi 2023 jumla ya **ICU 33** zilikuwa zimekamilika na zimeanza kutoa huduma. Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya ICU kutaongeza idadi ya vitanda vya ICU kutoka **vitanda 258** vilivyokuwepo na kufikia jumla ya **Vitanda 1,000.** ***Uwekezaji huu uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan utaokoa maisha ya wananchi wengi zaidi ndani ya Hospitali kwa asilimia 20 hadi 30.***

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini ya **magari ya wagonjwa (Ambulance)** nchini ambapo jumla ya **magari 595** kati ya **magari 761** yaliyopo yanafanya kazi na **221** yapo katika hatua mbalimbali za matengenezo. Serikali kupitia Wizara ya Afya na OR TAMISEMI imekamilisha ununuzi wa magari ya kubebea **wagonjwa 727** ambapo hadi sasa jumla ya **magari 77** yamewasili nchini. ***Uwepo wa magari ya wagonjwa (ambulance) utasaidia kusafirisha wagonjwa mbalimbali wakiwemo akinamama wajawazito kwa wakati na kuokoa maisha yao na vichanga vyao. Magari haya pia, yatasaidia huduma za uokoaji na huduma kwa wahanga wa ajali katika barabara kuu na kuwasafirisha kwa wakati huku wakipatiwa huduma wakati wakiwa njiani.***

**UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU YA KIBINGWA NA UBINGWA BOBEZI**

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya Kibingwa na Ubingwa bobezi nchini kwa kusogeza huduma hizi karibu na wananchi. Huduma hizi hutolewa na Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za kanda, Hospitali maalum na Hospitali za Rufaa za Mikoa katika kutoa huduma za afya nchini **kama ilivyoainishwa kuanzia ukurasa wa 79 hadi 112 wa hotuba yangu.** Katika Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya **wagonjwa 4,797,988** walihudumiwa katika hospitali hizi. Aidha katika kutekeleza sera ya matibabu sawa kwa wote, matibabu ya misamaha yenye thamani ya **shilingi 88,565,989,835** yalitolewa katika hospitali hizi kwa kipindi hiki, ikilinganishwa na misamaha yenye thamani ya shilingi 38,942,930,007.19 iliyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. **Kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 11 hadi 12 la Hotuba yangu.**

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali zimeendelea kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, ikiwa ni Pamoja na **huduma ya upandikizaji figo** *(Renal Transplant)* kwa wagonjwa wanne (4), huduma ya **upandikizaji vifaa vya usikivu *(cochlea implant surgery)*** kwa watoto tisa (9), **huduma ya upandikizaji wa uloto** *(bone marrow transplant)* kwa wagonjwa 11, Huduma za **upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua** na mishipa ya damu kwa wagonjwa 502, huduma za **upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo** kwa kutumia mtambo maalum *"Catheterization Laboratory"* kwa **wagonjwa 1,069 upasuaji wa mifupa** mbalimbali kwa wagonjwa 2,313, **kubadilisha nyonga** wagonjwa 145; **upasuaji wa goti** wagonjwa 124; **upasuaji wa goti kwa kutumia matundu** wagonjwa 228; **upasuaji wa mfupa wa kiuno** wagonjwa 77; **upasuaji wa uti wa mgongo** wagonjwa 277; **upasuaji wa ubongo** wagonjwa 160; upasuaji wa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 364; upasuaji wa dharura 1,679, **upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu (Angio – Suite)** kwa wagonjwa **94.**

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Hospitali ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum ziliweza kuanzisha huduma mpya za ubingwa na ubingwa bobezi zikiwemo;

a) Huduma za **Upandikizaji wa Uloto (*Bone marrow Transplant*)** kwa watoto wenye **Siko seli** katika Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyoanza mwezi Januari 2023 na hadi sasa wagonjwa watatu **(3)** wamependikizwa.

b) Huduma ya **kupunguza uzito kwa kuwekewa Puto** *(Intragastric balloon)*, katika Hospitali ya Mloganzila ambapo wagonjwa 87 wamehudumiwa.

c) huduma ya **matibabu ya kuondoa mawe** kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi mshtuko (*Extracorporeal Shock Wave Lithotripsy*) katika Hospitali ya Mloganzila ambapo wagonjwa 380 wamehudumiwa

d) Huduma ya **matibabu ya njia ya mirija** kwenye kansa mbalimbali kwa mfano ya ini (trans arterial chemo embolization of liver tumor, TACE) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambapo wagonjwa 14 wamehudumiwa.

e) Huduma ya **kuchepusha damu** iliyoshindwa kupita kwenye ini lenye unyafuzi (Trans jugular trans-hepatic portal systemic shunt, TIPS, in liver cirrhosis) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambapo wagonjwa 8 wamehudumiwa.

f) Huduma ya **ufunguaji wa mishipa iliyobana au kuziba** iliyokua inatanuka kwenye usafirishaji wa damu (percutaneous transluminal angioplasty) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambapo wagonjwa 63 wamehudumiwa.

**g) huduma ya uwekaji wa betri kwenye moyo** *(Pace Maker)* katika Hospitali ya Benjamin Mkapa ambapo jumla ya wagonjwa 12

h) Huduma za **magonjwa ya Damu** zimeanzishwa katika Hospitali ya Kanda za Juu kusini Mbeya ambapo jumla ya wagonjwa 322 wamehudumiwa

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kuimarika kwa matibabu ubingwa bobezi Hospitali zetu zimeweza kuhudumia wagonjwa nje ya nchi na hivyo kama huduma za **utalii tiba** *(Medical Tourism)* .Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya **wagonjwa 812** wamehudumiwa na Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda ukilinganisha na **wagonjwa 368** kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Wagonjwa hao walikuwa wanatoka katika nchi za Kenya, Uganda, Congo, Comoro, Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi, Msumbiji, DRC, South Sudani. Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma hizo na kuanzisha nyingine kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii tiba katika nchi za Afrika. Nitumie Bunge lako Tukufu kuitambulisha kamati ya taifa ya kuimarisha utalii tiba inayoongozwa na Prof. Mohamed Janabi

**41.** ***Mheshimiwa Spika;*** **Taarifa ya utekelezaji wa majukumu** ya Hospitali za Kitaifa, Maalum, Kanda; Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Hospitali ya Kibong'oto, Hospitali ya Mirembe, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya nyanda za juu kusini Mbeya, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma (BMH), Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando na Hospitali za Rufaa za Mikoa**. Taarifa hii ipo kuanzia ukurasa wa 79 hadi 112 wa hotuba**

**UTAYARI, UDHIBITI NA KUKABILIANA NA MAGONJWA HATARI YA KUAMBUKIZA NA MILIPUKO**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kujiandaa na kukabiliana na magonjwa hatari ya mlipuko yanayoathiri afya ya Jamii ikiwemo UVIKO-19, Ebola, Marburg, Kipindupindu, Homa ya Mgunda. Wizara imeweza kudhibiti Mlipuko wa **Homa ya Mgunda** iliyotokea Mkoani Lindi katika Wilaya ya Ruangwa. Aidha, Wizara iliweza kudhubiti **ugonjwa wa Ebola** kuingia nchini tangu ugonjwa huo uliporipotiwa nchini Uganda tarehe 20 Septemba 2022.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeweza kudhibiti **ugonjwa wa Marburg ambao uligundulika** katika Wilaya ya Bukoba vijijini, Mkoani Kagera ambapo watu waliopata maambukizi ya virusi vya Marburg walikuwa tisa (9) na kati yao sita (6) wamefariki, Aidha wagonjwa watatu wamepona na wanaendelea na shughuli zao. Nitumie fursa hii kuwashukuru watumishi wa afya hususani walio mstari wa mbele kwa kupambana usiku na mchana kuhakikisha tunaudhibiti ugonjwa huu nchini. Kwa mujibu wa miongozo ya WHO tutatangaza kumalizika kwa mlipuko huu hapa nchini siku 42 toka tulipomruhusu mgonjwa wa mwisho. **Ukurasa wa 113 hadi 120 wa Hotuba yangu**

**RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto zinazoikabili Sekta ya Afya kutokana na upunguful wa rasilimali watu, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kupunguza pengo kati ya upatikanaji wa Watumishi wa afya ikilinganishwa na mahitaji halisi. Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya **watumishi wa afya 8,317** ambapo Ofisi ya Rais TAMISEMI imepokea kibali cha kuajiri watumishi 8,070 katika ngazi ya msingi na watumishi 247 katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Kanda na Mikoa. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **jumla ya wataalamu 8,992 waliajiriwa kwa utaratibu wa mikataba** ambapo wataalamu 4,183 waliajiriwa kwa mikataba kupitia mapato ya ndani ya vituo vya kutolea huduma na 4,809 kupitia wadau wa maendeleo.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi na wataalam wa afya katika kada mbalimbali za kitabibu, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za Afya na zinazotolewa na watoa huduma wenye ujuzi wa kutosha. Katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi, Wizara imeanzisha mkakati mpya uitwao ***Samia Health Super Specialization Program*** wa kutoa ufadhili kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa utaratibu wa ***set*** ambapo, **watumishi 981**, wanaochukua mafunzo ya uzamili katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi walipata ufadhili wa masomo, kati yao 802 ni vyuo vya ndani na 179 ni mafunzo nje ya nchi. Tunamshukuru Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kutoa fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 8** kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu bingwa na bobezi nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imetoa ufadhili wa wanafunzi 287 wa fani ya uuguzi na ukunga katika ngazi ya Stashahada.

**MIRADI YA MAENDELEO**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara imeendelea na ukamilishaji wa miradi ya maendeleo katika Vituo vya kutolea huduma za Afya. Hatua iliyofikiwa ni Miradi 29 inayotekelezwa na Fedha za Ndani; miradi minne (4) imekamilika kwa asilimia 100, miradi 10 imefikia asilimia 80 hadi 99, miradi 12 ipo chini ya asilimia 80 huku miradi mitatu (3) utekelezaji wake haujaanza kufanyika. Kwa upande mwingine kati ya miradi 150 inayotekelezwa kupitia fedha za UVIKO-19, miradi 107 imekamilika kwa asilimia 100, miradi 36 imefikia wastani wa asilimia 80 hadi 99 na miradi saba (7) ipo chini ya asilimia 80. Vilevile, miradi 7 inayotekelezwa na Wadau wa Maendeleo, miradi minne (4) imekamilika kwa asilimia 100, miradi mitatu (3) imefikia wastani wa asilimia 80 hadi 99. **Taarifa ya kina ya utekelezaji wa miradi hiyo imeambatishwa katika taarifa hii Kiambatisho Na. 17**

**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa na Taasisi 6 zilizopo chini yake. Taasisi hizo ni pamoja na Bohari ya Dawa (MSD), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), **Taarifa ya utekelezaji wa Taasisi hizi zimeainishwa kuanzia ukurasa wa 134 hadi ukurasa wa 163 katika Hotuba yangu.** Hata hivyo kwa upande wa mfuko wa bima ya Taifa ya afya ninapenda nizunguzie mambo mawili kwa lengo la kutoa ufafanuzi, wa hatua zilizochukuwa na Serikali katika kuimarisha uhai na uendelevu wa mfuko huu muhimu kwa Sekta ya Afya nchini

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na tathmini hii, ni wazi kuwa kundi hili lina matumizi makubwa na hivyo kutishia uhai na uendelevu wa Mfuko endapo hatua hazitachukuliwa. Hivyo, kuanzia mwezi februari 2023, utaratibu wa kuandikisha kundi hili kwa mtoto mmoja mmoja umesitishwa na msisitizo kuwekwa katika usajili kupitia vifurushi ambavyo vina utaratibu wa kusajili katika ngazi ya familia. Vifurushi hivi vijulikanavyo kama Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya vinatoa fursa kwa familia kusajiliwa kulingana na ukubwa wake pamoja na kipato. Aidha, watoto hawa wanaweza kusajiliwa kupitia shule wanazosoma, lengo ikiwa ni kusajili watoto wengi kwa umoja wao kulingana na misingi na dhana ya bima. ***Nitoe rai kwa wananchi wote kutumia fursa hii kwa kuandikisha familia zao mapema na wasisubiri kuugua na ndipo wajiunge, jambo ambalo ni kinyume na***

*dhana ya bima.*

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya Udanganyifu ambayo kwa kiasi kikubwa hufanywa na baadhi ya watoa huduma wasio waaminifu, wanachama na waajiri. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, Mfuko ulifanya chunguzi **311** za matukio ya viashiria vya udanganyifu. Kutokana na chunguzi hizo na kupitia taratibu zake za ndani, Mfuko ulibaini madai yasiyo halali ya **shilingi bilioni 9.74** kutoka kwa watoa huduma mbalimbali yaliwasilishwa na kulipwa na Mfuko. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2023, kiasi cha **shilingi bilioni 6.46** tayari kimerejeshwa na kwa kiasi kilichosalia, makato yanaendelea kupitia madai ya vituo husika kwa utaratibu uliopo. Hatua kali zimeendelea kuchukuliwa dhidi ya wale wanaofanya vitendo hivi vya udanganyifu ikiwemo kusitisha mikataba baina ya Mfuko na wamiliki wa vituo pamoja na kuwasilisha majina ya watumishi katika Bodi zinazosimamia taaluma zao. Hadi kufikia Aprili 2023, Mfuko ulisitisha mikataba na vituo **38** na kuwasilisha watumishi **131** katika mabaraza yao ya kitaaluma kwa hatua zaidi. Nitoe rai kwa watoa huduma wote pamoja na wanachama wa Mfuko, kuacha vitendo vya udanganyifu ili mfuko huu uendelee kuwa endelevu.

**D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MABARAZA NA BODI ZA KITAALUMA**

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa Wataalam wa Sekta ya Afya. Katika kutekeleza hilo, **Mabaraza nane (8)** na **Bodi mbili za kitaaluma** zilizoundwa kisheria kwa ajili ya kusimamia maadili ya kitaaluma, kusajili Wataalam na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na wataalam wa kada husika. Mabaraza na Bodi za kitaaluma ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Macho, Baraza la Radiologia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB) na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi. Taarifa ya utekelezaji wa Mabaraza na Bodi za Kitaaluma zimeainishwa kuanzia **ukurasa wa 163 hadi ukurasa wa 186 katika Hotuba.**

**E. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara ya Afya imejiwekea **vipaumbele kumi na nne (14)** ili kuboresha huduma za afya nchini: -

i. Kuimarisha huduma za Kinga dhidi ya magonjwa ikiwemo huduma za chanjo, huduma za lishe, huduma za usafi na afya mazingira na huduma za afya ngazi ya jamii;

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma katika ngazi zote;

iii. Kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na damu salama katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya;

iv. Kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vya watoto wachanga;

v. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi ili kusogeza huduma hizi karibu na wananchi na kuwapunguzia gharama za kupata matibabu haya nje ya nchi.

vi. Kuimarisha huduma za Afya ya Akili, huduma za utengamao na Tiba Shufaa

vii. Kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatari ya kuambukiza;

viii. Kudhibiti magonjwa ya kuambukiza hususani Malaria, Kifua Kikuu (TB), VVU/UKIMWI na Homa ya ini.

ix. Kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza hususani kisukari, shinikizo la juu la damu na magonjwa ya Moyo na kuimarisha huduma za dharura nchini ikiwemo ajali;

x. Kuimarisha upatikaji wa wataalam katika Sekta ya Afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi

xi. Kuendeleza na kusimamia huduma za tiba asili na tiba mbadala nchini

xii. Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu;

xiii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;

xiv. Kusimamia tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za Afya;

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2023/24, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 1,234,816,516,000.00** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa Ofisi na miradi ya maendeleo. Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

**1.** Katika kuimarisha **huduma za Kinga** dhidi ya magonjwa ambapo kiasi cha shilingi , kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuimarisha utekelezaji wa Afua za Chanjo kwa watoto nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 114,369,238,904.00** kimetengwa. Afua hizo ni:-

a) Kununua, kutunza na kusambaza chanjo kwa gharama ya **Shilingi 87,044,538,781.**

b) Kununua majokofu 1,601 ya mnyororo baridi wa chanjo yenye thamani ya **Shilingi 21,025,327,723.**

c) Kununua magari 102 ya kusambazia chanjo yenye thamani ya **Shilingi 6,299,372,400.**

ii. Kuimarisha **huduma za lishe** kwa kununua na kusimika vinu 300 vya kuongeza virutubisho na kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) ili kuboresha huduma za Lishe nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000.00** kimetengwa

iii. Kuimarisha utekelezaji wa afua za **usafi na afya mazingira** katika jamii na taasisi za umma na binafsi,

iv. Kuanzisha mafunzo maalumu ya miezi sita kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao 5,000 ambao wataajiriwa na kupewa vitendea kazi ambapo kiasi cha **Shilingi 13,500,000,000** kimetengwa.

**2.** Katika kuboresha ubora wa huduma, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

i. Kuanzisha programu ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wasimamizi na watoa huduma za afya (**Leadership4Health Transfomation Program**) ili kuongeza uwajibikaji, ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote

ii. Kuimarisha utawala bora, uongozi na menejimenti ya usimamizi wa huduma za afya kwa kushirikisha kamati za ulinzi na usalama na viongozi na watendaji wa Serikali katika ngazi zote.

iii. Kufanya kaguzi za mara kwa mara pamoja na kuimarisha usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya

iv. Kuhakikisha utoaji wa huduma za afya unazingatia weledi, maadili na miiko kupitia mabaraza ya kitaaluma na bodi za usajili ikiwemo kuanzisha mfumo wa kuwatambua na kuwapa tuzo wataalam wanaofanya vizuri

v. Kujenga na kukarabati Miundombinu ya kutolea Huduma za afya katika ngazi ya Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 91,898,000,000.00** kimetengwa. Maeneo yaliyohusika ni pamoja na;

a) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda za Chato, Mtwara; na kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi na Hospitali Maalum ya Taifa ya huduma za Mama na Mtoto katika Mkoa wa Dodoma ambapo jumla ya **Shilingi 29,572,910,244** kimetengwa.

b) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali (4) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya Katavi, Geita, Songwe na Simiyu ambapo jumla ya Shilingi bilioni 13 kimetengwa.

c) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali mpya tatu (3) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa ya Shinyanga, Singida na Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Mara ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 11 kimetengwa.

d) Kuendelea kukamilisha upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali Rufaa za Mikoa za Ligula (Mtwara) Kagera, Maweni (Kigoma), Kitete (Tabora), Sekou – Toure (Mwanza) na Mawenzi (Kilimanjaro), Songea (Ruvuma), Manyara, Bombo (Tanga), Mount Meru (Arusha), Sokoine (Lindi), Mbeya, Hospitali ya Ukerewe na uimarishaji wa Hospitali za Rufaa (dharura) ambapo kiasi cha **Shilingi 36,398,000,000** kimetengwa.

e) Kuendelea na ujenzi wa wodi ya wagonjwa binafsi (Private word katika hospitali ya Taifa Muhimbili) ambapo kiasi cha Shilingi 4,500,000,000 kimetengwa.

v. Kuanzisha utaratibu wa kupima utendaji wa timu za uendeshaji wa huduma za afya katika ngazi za Vituo/ Hospitali, Halmashauri (CHMT) na Mikoa (RHMT) katika maeneo ya maoteo ya dawa, upatikanaji wa dawa, huduma za uchunguzi (maabara na Radiolojia) udhibiti wa kuchina na kuchotora wa dawa, taratibu za kushughulikia malalamiko ya wagonjwa, muda wa kuwahudumia wagonjwa.

vi. Kuunganisha baadhi ya mabaraza ya kitaaluma na kuhamasisha wanataaluma wengi kusajiliwa kwa kupunguza kiwango cha ada za usajili.

vii. Kuhamisha majukumu ya usimamizi wa Maduka ya Dawa kutoka Baraza la Wafamasia na kuhamishia Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba ili Baraza lijikite zaidi katika kusimamia wanataaluma.

viii. Kuimarisha mfumo wa rufaa wa wagonjwa ili kuwezesha Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa kujikita katika kutoa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi.

**3.** Katika kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za uchunguzi wa magonjwa, yafuatayo yamepewa kipaumbele;

i. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maabara za uchunguzi wa magonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo upatikanaji wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara

ii. Kusogeza huduma za radiolojia kwa wananchi kwenye ngazi za afya ya msingi (ununuzi wa Ultrasound na digital Xrays)

iii. Kuratibu na kusimamia mpango wa matengenezo na matengenezo kinga ya vifaa na vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kuanzisha karakana , kutoa mafunzo ya mafundi na kununua vifaa na vipuli vya matengenezo

iv. Kusimamia ubora wa huduma kwa kuzingatia miongozo ya ubora kwa maabara zote hadi ngazi ya afya ya msingi ili kupata ithibati

**4.** Katika kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na damu salama katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya, kiasi cha **Shilingi 205,063,250,000.00** kimetengwa kwa malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha uandaaji wa Maoteo ya dawa kutoka katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma kwa kuwasimamia kikamilifu wafamasia wa Halmashauri na mikoa kwa kuweka mfumo wa uwajibikaji na kuhakikisha wanatumia mifumo iliyopo ya maoteo ya dawa na taarifa za wagonjwa. ***Nitumie fursa hii kuwaelekeza Wafamasia katika ngazi ya Halmashauri na Mikoa kuandaa na kuwasilisha maoteo sahihi ya dawa na vifaa tiba kabla ya tarehe 31 Januari ya kila mwaka kwa mujibu wa kanuni namba 141 ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake.***

ii. Kununua, kutunza na kusambaza bidhaa za Afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

iii. Kujenga maghala mapya ya kuhifadhia dawa katika mikoa mbalimbali nchini

iv. Kuweka mifumo thabiti ya udhibiti na ukaguzi wa dawa nchini ikiwemo kuimarisha kamati za tiba na dawa (Therapeutic committees) kwa kuzifanyia mapitio na kuzijengea uwezo ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu

v. Kufanya kaguzi za mara kwa mara za hali ya dawa katika vituo ili kudhibiti upotevu na kuzuia kuchina kwa dawa

vi. Kusimamia matumizi sahihi ya miongozo ya matibabu kwa magonjwa (STGs) kwa kuhakikisha watoa huduma za afya wanatumia miongozo hii.

**5.** Katika kuimarisha ubora wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kiasi cha **Shilingi 16,216,250,000** zimetengwa na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

i. Kusimamia upatikanaji wa huduma bora na salama za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa wakati ikiwemo kufanya uhakiki na kaguzi za mara kwa mara katika vituo vya kutolea huduma ili kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa wajawazito na watoto wachanga zinazingatia ubora, weledi, maadili na ziendane na miongozo ya kitaifa.

ii. Kuhakikisha uzingatiwaji wa miongozo ya kutoa huduma za uzazi salama kabla na baada ya kujifungua ikiwemo kuhakikisha wajawazito wanafanyiwa vipimo vyote muhimu hususani wingi wa damu, sukari, Shinikizo la damu (BP), uzito, protein kwenye mkojo na maambukizi mengine wakati wa ujauzito ili kubaini viashiria vya hatari na kuchukua hatua stahiki kwa wakati

iii. Kutoa mafunzo kazini na unasihi (*on job training and clinical mentorship*) kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma mfano Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA), Chama cha Madaktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake na uzazi (AGOTA) ili kuwaongezea ujuzi na weledi (*Skills and competence*) wataalam wa ngazi za msingi katika kuwahudumia wajawazito na watoto wachanga. Kupitia mpango huu, **wataalam bingwa na bobezi 100** wakiwemo Madaktari bingwa, wauguzi, wakunga, na watoa dawa za usingizi wameandaliwa kutekeleza mpango huu kwa awamu ya kwanza.

iv. Kununua na kusambaza dawa muhimu za uzazi salama ikiwemo dawa *Magnesium sulphate (za kuzuia kifafa cha mimba), Oxytocin (dawa za kuzuia mjamzito kutoka damu wakati na baada ya kujifungua), FeFo* (kwa ajili ya kuongeza damu) na *SP* (kwa ajili ya malaria), dawa za uzazi wa mpango, dawa za watoto wa umri wa chini ya miaka 5 kwa ajili ya kinga za minyoo, dawa za kuongeza damu na dawa za Malaria.

v. Kununua Vifaa Tiba kwa ajili ya Upasuaji kwa wajawazito na kuvisambaza katika vituo 278 vya afya msingi katika mikoa yote.

vi. Kuongeza wodi maalum 100 zenye vifaa vya kutolea huduma za watoto wachanga zikiwemo huduma za Mama Kangaruu (Kangaroo mother care) na huduma za watoto wachanga mahututi (Neonatal Intensive Care Unit-NICU)

vii. Kuongeza vituo vipya 100 vinavyotoa huduma za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi

viii. Kuongeza vituo vipya 300 vya kutoa huduma rafiki kwa vijana

ix. Kuongeza vituo vipya 16 vinavyotoa huduma jumuishi kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto

x. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali Maalumu ya Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto Dodoma.

**6.** Katika kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi kiasi cha **shilingi 23,000,000,000.00** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuendelea kutoa huduma za matibabu ya ubingwa bobezi katika, Taasisi, Hospitali za Kanda na Maalum pamoja na kuanzisha huduma mpya kulingana na mahitaji;

ii. Kuanzisha programu ya kugharamia huduma za matibabu ya ubingwa bobezi yanayotolewa na Hospitali za ndani ya nchi hususan kupandikiza figo, kupandikiza uloto kwa watoto, kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto na kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu ambapo kiasi cha **shilingi 5,000,000,000.00** zimetengwa;

iii. Kuimarisha **miundombinu** katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Hospitali maalum ya Kibong'oto na Hospitali za Rufaa za Kanda za KCMC, Bugando, Mbeya na Benjamin Mkapa. Kiasi cha **Shilingi 10,000,000,000.00** zimetengwa;

iv. Kuwekeza vifaa tiba, vifaa vya uchunguzi na vitendanishi vitakavyowezesha utoaji wa huduma za kibingwa bobezi ikiwemo kupandikiza figo, kupandikiza uloto, kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto na kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu ambapo Kiasi cha**Shilingi 8,000,000,000.00** zimetengwa;

v. Kuimarisha utoaji wa huduma za mkoba na tembezi katika ngazi ya msingi;

vi. Kuimarisha na kuongeza wigo wa ushirikiano na Taasisi/Hospitali za kimataifa zinazotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ikiwemo kupeleka wataalamu katika hospitali hizo na kufanya kambi za pamoja za matibabu;

vii. Kuhakikisha Hospitali na taasisi za ubingwa bobezi zinatekeleza mpango wa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wataalam wao ili kuwaongezea ujuzi na weledi wa kutoa huduma za ubingwa bobezi.

**7.** Katika kuimarisha **huduma za Afya ya Akili, huduma za utengamao na Tiba Shufaa**, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja:

i. Kutoa elimu kwa umma kuhusu vihatarishi vya afya ya akili na namna ya kukabiliana navyo;

ii. Kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu wa afya ya akili kwa kushirikiana na vyuo vikuu na vyuo vya kati. Kwa mwaka 2023/24 Chuo kikuu cha Afya MUHAS kinaanzisha shahada ya kwanza ya Sayansi ya Saikolojia tiba (Clinical Psychology*)*. Aidha, Vyuo vya kati pia vitaanzisha mafunzo ya wataalam wa afya ya akili ili kusogeza huduma za afya ya akili karibu na jamii;

iii. Kuanzisha kozi maalum za muda mfupi za Afya ya Akili na huduma za utengamao ili kupata wataalam watakaoenda kutoa huduma hizi katika vituo vyetu vya ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa hadi ngazi ya Afya ya Msingi katika kipindi ambacho tunaandaa watalaam wabobezi katika taaluma hizo;

iv. Kuipandisha hadhi na kuiongezea majukumu Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe na kujenga miundombinu ya kutolea huduma za Afya ya Akili ambapo kiasi cha **Shilingi 2,000,000,000.00** kimetengwa;

v. Kuimarisha huduma za Afya ya Akili kwa wagonjwa wa nje wa kuanzia na Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Halmashauri.

vi. Kufanya utambuzi wa vituo vinavyotoa huduma za afya ya akili.

vii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa vya uchunguzi na vifaa tiba kwa ajili ya wagonjwa wa afya ya akili;

viii. Kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu wa huduma za utengamao kwa kushirikiana na vyuo vikuu na vyuo vya kati, kipaumbele kikiwa ni kuanzisha mafunzo ya kada za kati katika eneo la huduma za utengamao hususan tiba mazoezi (physiotherapy), tiba kazi (occupational therapy) na Tiba lugha na tiba matamshi (speech therapy);

ix. Kuimarisha na kuanzisha huduma za tiba za utengamao (rehabilitative medicine services) hususan kwa watoto katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri

x. Kuimarisha huduma za utengamao na kuanzisha vituo maalum vya huduma hizo ikiwemo za wagonjwa wa Kiharusi (Stroke centers) ili kuboresha huduma hizo, kuwawezesha kumudu shughuli zao kadri inavyowezekana na kuongeza ubora wa maisha.
xi. Kufanya utambuzi wa vituo vinavyotoa huduma za tiba za utengamao; na
xii. Kuimarisha upatikanaji wa viungo saidizi kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa viungo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha karakana za kutengeneza viungo hivyo na mafunzo kwa wataalam

**8.** Ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatari ya kuambukiza, kiasi cha **Shilingi 20,750,402,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza afua zifuatazo:

i. Kuendeleza ujenzi wa vituo vya kuhudumia wagonjwa wa wahisiwa wa magonjwa hatari ya kuambukiza (Highly Infectious Disease Treatment Unit) Kisopwa Dar es Salaam na kuanza ujenzi wa kituo katika Mkoa wa Kagera.
ii. Kutoa mafunzo ya wataalam wa Sekta mbalimbali zinazogusa masuala ya afya (one health) ikiwemo kuendesha mafunzo kwa vitendo (*simulation exercises*) angalau mara mbili kwa mwaka ili kuimarisha uwezo wa nchi katika kujiandaa na kukabiliana na magonjwa hatari ya milipuko
iii. Kuandaa na kuboresha mifumo ya uratibu wa majanga na milipuko ya magonjwa hatari ikiwemo uanzishwaji wa Vituo vya Operesheni ya Matukio ya Dharura (PHEOCs) katika mikoa mitano (5)
iv. Kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa vituo vya Operesheni wa Matukio ya Dharura katika ngazi ya mikoa nchini ambapo wataalam wa mikoa mitano itapatiwa mafunzo.

**9.** Katika Kutekeleza Afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza hususani Malaria, Kifua Kikuu (TB), VVU/UKIMWI na Homa ya ini, kiasi cha **Shilingi 101,456,809,628.00** kimetengwa. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni:

i. Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria ambapo kiasi cha **Shilingi 25,363,979,112.00** kimetengwa kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vyandarua vyenye dawa kwenye jamii, ununuzi wa vitendanishi na dawa ili kuwezesha ugunduzi na matibabu ya ugonjwa malaria pamoja na ufuatiliaji wa wagonjwa kwenye maeneo yanayotekeleza afua za kutokomeza malaria.
ii. Utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 16,173,530,473.00** zimetengwa kwa ajili ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu kwenye jamii, tiba kinga dhidi ya kifua kikuu kwa WAVIU na watoto chini ya miaka mitano wanaoishi na waliopata maambukizi ya Kifua Kikuu, ununuzi wa vifaa tiba, vitendanishi na dawa, huduma za uchunguzi na matibabu ya kifua kikuu na kifua kikuu sugu.
iii. Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, homa ya ini na magonjwa ya ngono nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 59,919,300,043.00** kimetengwa kwa ajili ya manunuzi ya vitendanishi vya kupima VVU, kondomu, dawa kinga na dawa za kufubaza VVU

**10.** Ili kudhibiti Magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na kuimarisha huduma za dharura nchini ikiwemo ajali, kiasi cha **Shilingi 22,000,000,000.00** zimetengwa. Maeneo yatayotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kutoa elimu kwa umma kuhusu vichochezi na visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza kama vile tabia bwete, uzito uliokithiri, matumizi ya sukari, chumvi na mafuta kupita kiasi ambavyo vinaweza kusababisha magonjwa ya Kisukari, Shinikizo la Juu la Damu na magonjwa ya moyo
ii. Kuimarisha huduma za uchunguzi ili kuweza kuyatambua mapema magonjwa yasiyoambukiza yaliyopewa kipaumbele
iii. Kuimarisha huduma za utambuzi na matibabu ya magonjwa ya Damu ikiwemo ugonjwa wa selimundu (Sickle Cell) na himofilia (hemophilia) pamoja na kufanya upandikizaji wa uloto (bone marrow transplant) ambapo kipaumbele kitatolewa kwa watoto chini ya umri wa miaka 12.
iv. Kuimarisha upatikanaji wa dawa za kutibu magonjwa yasiyoambukiza ambapo kuanzia Julai 2023, aina mbili (2) za dawa za kutibu shinikizo la juu la damu zitapatikana katika ngazi ya Zahanati na aina tano (5) za dawa hizi zitapatikana katika ngazi ya Vituo vya Afya (Health Center) ambapo awali zilikuwa zinapatikana katika katika ngazi ya Hospitali za Halmashauri
v. Kuimarisha mfumo wa kuwahudumia wagonjwa wa dharura na ajali na kuwasafirisha kutoka kituo kimoja kwenda kingine ili kupata huduma za rufaa. Wizara itatekeleza yafuatayo:

a) Kujenga miundombinu kwa ajili ya vituo vya uratibu wa magari ya wagonjwa (ambulance dispatch centers) katika mikoa 5 ya kimkakati kwa awamu ya kwanza;
b) Kufunga mfumo wa uendeshaji, ufuatiliaji na uratibu wa magari yote ya wagonjwa na uokozi ili kuboresha huduma hizi na kupunguza vifo vinavyozuilika vinavyotokana na kuchelewa kufika kwa magari ya uokozi katika matukio ya ajali na kuwasafirisha majeruhi wa ajali kwenda katika vituo vya tiba;
c) Kuanzisha na kuimarisha mfumo wa kielectroniki wa takwimu za ajali (trauma registries) kwenye idara za dharura nchini ili kuratibu taarifa za kiafya za wahanga wa ajali na kuwezesha mikakati ya kuzuia na kupunguza madhara yanayotokana na ajali;
d) Kuanzisha mafunzo kwa watoa huduma za dharura nje ya hospitali na kuandaa kanuni za usimamizi na uendeshaji. Hii ni pamoja na kuandaa mtaala kwa ajili ya watoa huduma za magari ya wagonjwa (paramedics) kwa kushirikiana na Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu nchini. Kwa awamu ya kwanza, mafunzo yatafanyika kwa watoa huduma 6 kwa kila ambulance wakiwemo wauguzi, maafisa tabibu, madaktari na madereva. Pia mafunzo shirikishi yatafanyika kwa jeshi la polisi, jeshi la zimamoto na uokoaji na wananchi wa kujitolea; na
e) Kuendelea kutoa mafunzo kwa vitendo (mentorship) kwa watoa huduma za EMD kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri ili kuboresha huduma za dharura nchini

**11.** Katika kuimarisha upatikaji wa wataalam katika Sekta ya Afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi kiasi cha **Shilingi 83,142,000,000.00** kimetengwa. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni:

i. Kuandaa na kuweka mpango wa muda mrefu wa watoa huduma wa afya ili kukidhi mahitaji (human resource planning);
ii. Kutoa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya vya umma na kusimamia ubora wa mafunzo haya katika vyuo vya umma na binafsi;
iii. Kuendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wataalam wa ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi 649 wanaoendelea na wataalam wapya 450 pamoja na kufadhili mafunzo ya kada za kati za kimkakati ambapo kiasi cha **Shilingi 17,142,000,000.00** kimetengwa;
iv. Kugharamia mafunzo kwa vitendo ya watarajali (Interns) wa kada mbalimbali za Afya wakiwemo Madaktari Wauguzi, Wafamasia, wataalam wa maabara na wataalam wa afya mazingira. Kiasi cha **Shilingi 56,000,000,000.00** kimetengwa;
v. Kukarabati na kujenga majengo mapya katika vyuo vya mafunzo ya Afya vya umma, ambapo kiasi cha **Shilingi 6,000,000,000.00** zimetengwa; na
vi. Kufufua Chuo cha mafunzo endelevu kwa wataalam wa afya walioko kazini (Center for Educational Development in Health-CEDHA), ili kuimarisha weledi, maadili, ujuzi na uongozi katika sekta ya afya. Kiasi cha **Shilingi 4,000,000,000.00** kimetengwa.

**12.** Katika kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 2.5** kimetengwa. Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma na kupunguza muda wa wananchi kusubiri kupata huduma za afya. Hatua hii pia itawezesha kudhibiti udanganyifu na upotevu wa rasilimali fedha, dawa na bidhaa zingine za afya;
ii. Kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Afya ili iweze kusomana, kuleta ufanisi na kupunguza usumbufu kwa watoa huduma na wananchi;
iii. Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika ngazi zote za kutoa huduma za afya ; na
iv. Kuanzisha kituo cha Taifa cha Umahiri wa masuala ya TEHAMA katika Sekta ya Afya (Center for digital Health).

**13.** Katika kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kukamilisha Mwongozo wa Taifa wa uchangiaji wa huduma za afya;
ii. Kuimarisha mfuko wa Taifa wa Bima ya afya;
iii. Kufanya mapitio ya mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya huduma za sekta ya afya (resource tracking studies);
iv. Kutafuta na kuratibu upatikanaji wa fedha za Afya kutoka kwa wadau wa maendeleo ikiwemo kuratibu mfuko wa afya wa pamoja (Health Basket Fund); na
v. Kufuatilia rasilimali fedha za afya zinazopelekwa kwa Asasi zisizo za kiserikali kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara inayosimamia Usajili wa Asasi hizo.

**14.** Katika kuimarishaji shughuli za Tafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMR), kiasi cha **Shilingi 20,378,969,000** kimetengwa ili kutekeleza afua hii.

## F. SHUKRANI

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa nchi rafiki, Mashirikaya Kimataifa na Sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za Afya na Ustawi wa Jamii.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za **Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), Ireland (Irish Aid), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia**, **UNICEF,** kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja **(Health Basket Fund),** ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini hususani afya ya msingi. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali ikiwemo kufadhili miradi mbalimbali inayotekelelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuboresha huduma za afya nchini.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN-Women, **WHO** na IAEA); Jumuiyaya Nchi za Ulaya (EU); IMF, **Benki ya Dunia**, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); **GAVI; US-PEPFAR**; **US-CDC; USAID**; PMI; Abbott Fund; DFID; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; **Global Fund (for HIV, TB na Malaria);** Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; KfW; Save the Children; World Vision; Benki ya STANBIC; Walter REED; Jhpiego na Delloite

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na **Benjamin Mkapa Foundation**, AGOTA, Aga Khan Foundation, **APHFTA**, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania SurgicalAssociation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Kivulini, WiLDAF, TCRF na FSDT.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.),** Naibu Waziri wa Afya. Aidha, naomba kuwashukuru **Dkt. Seif A. Shekalaghe** Katibu Mkuu na **Dkt Grace Maghembe,** Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Tumaini Nagu**, Mganga Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia Wakurugenzi Wakuu wa Hospitali za Taifa na Kanda ambao ni **Prof. Mohamed Janabi** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Dkt. Respicious L. Boniface** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Dkt Peter Kisenge** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Julius Mwaiselage,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Leonard Subi** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dkt. Paul S. Lawala** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Dkt. Alphonce Chandika** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Mawala** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Fabian A. Massaga** (Hospitali ya Bugando) na **Prof. Geleard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC).

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru wakurugenzi na wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambazo ni MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TFNC pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili. Vilevile ninawashukuru Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa Sekta zote ambazo tunashirikiananazo katika kutoa huduma za afya pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa watanzania kujali na kulinda afya zao ikiwemo kwa kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa, kufanya mazoezi ya viungo mara kwa mara na kujiepusha na unywaji wa pombe kupita kiasi. Ni muhimu watanzania wakatambua kuwa **Mtu ni Afya na Afya ni Mtaji.**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru Familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Jimbo letu la Tanga Mjini.

## G. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2023/24

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka** 2023/24

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni mia sita sabini na saba, milioni mia sita ishirini na moja, laki moja na sitini na nane, mia tatu tisini na senti tisini na tano** (677,621,168,390.95). Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni themanini na nane, milioni mia nne kumi na nne, laki saba na elfu sabini na tano, mia moja sabini na saba bila senti** ( 88,414,775,177.00) zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi bilioni mia moja kumi na moja, milioni mia tano themanini na tano, laki mbili na elfu ishirini na nne, na mia nane ishirini na tatu bila senti.** (111,585,224,823.00) zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, **Shilingi bilioni mia nne sabini na saba, milioni mia sita ishirini na moja, laki moja na sitini na nane, mia tatu tisini na senti tisini na tano** (477,621,168,390.95) zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Mashirika yaliyo chini ya Wizara.

**Matumizi ya Kawaida**

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni mia tano na mbili, milioni mia tisa hamsini na moja, laki tisa na elfu tisa bila senti** (502,951,909,000.00) kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 41** ya bajeti tengwa, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni mia tatu Hamsini nan ne, milioni mia tatu arubaini na mbili, laki nne na elfu themanini na sita bila senti** (354,342,486,000.00) ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha **Shilingi bilioni mia moja arubaini na nane, milioni mia sita na tisa, laki nne na elfu ishirinin na tatu bila senti** (148,609,423,000.00) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi bilioni mia saba thelathini na mbili, milioni mia tatu sitini nan ne, laki sit ana elfu saba bila senti** (732,364,607,000.00) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 59** ya bajeti tengwa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi bilioni mia nne thelathini, milioni mia mbili tisini na nane bila senti** (430,298,000,000.00) na fedha za nje ni **Shilingi bilioni mia tatu na mbili, milioni sitini na sita, laki sita na elfu saba bila senti** (302,066,607,000.00)

**64.** ***Mheshimiwa Spika;*** jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni **Shilingi trilioni moja, bilioni mia mbili thelathini na tano,milioni mia tatu kumi na sita, laki tano na elfu kumi na sita bila senti** (1,235,316,516,000.00) ili kutekeleza malengo iliyojiwekea

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida | % | Miradi ya Maendeleo | % | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 52 | 502,951,909,000.00 | 41 | 732,364,607,000.00 | 59 | 1,235,316,516,000.00 |

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya ***www.moh.go.tz.***

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



Wafungaji wa mabao yote ya Yanga dhidi ya Dodoma Jiji FC juzi, Mudathir Yahaya (kushoto), Farid Mussa (katikati) na Kennedy Musonda, wakishangilia moja kati ya mabao waliyofunga juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-2 na kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya 29 kwa misimu tofauti tangu kuanzishwa mwaka 1965. **MPIGAPICHA WETU**

# MAMBO MA5 USIYOYAJUA UBINGWA YANGA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

BINGWA wa Tanzania Bara msimu wa 2022/23 amepatikana, naye si mwingine ni Yanga ya Dar es Salaam, iliyopata ushindi wa mabao 4-2 juzi dhidi ya Dodoma Jiji FC, mechi ikipigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

**Yalikuwa ni mabao matatu yaliyofungwa na wachezaji wawili wa Kitanzania, Mudathir Yahaya akipachika mawili, moja Farid Mussa, huku lingine likifungwa na mchezaji wa kimataifa kutoka Zambia, Kennedy Musonda.**

Mwamuzi Omari Mdoe, alipopuliza filimbi ya kuashiria mechi hiyo kumalizika na Yanga kuibuka na ushindi huo, iliashiria kuwa pointi tatu ambazo ilizipata zimeifanya kuwa jumla ya pointi 74, ambazo haziwezi kufikiwa na timu zote 15 zilizobaki za Ligi Kuu.

Ilikuwa hoi hoi nderemo na vifijo kwa wachezaji, wanachama, mashabiki na viongozi waliohudhuria mechi hiyo ambao wengi walikwenda na familia zao, wakiongozwa na Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi Said, ambaye aliungana na wachezaji na viongozi wenzake kushangilia ubingwa huo.

Yanga imetwaa ubingwa huo ikiwa imebakisha mechi mbili mkononi dhidi ya Mbeya City na Prisons.

Kwenye makala haya, tunakuletea takwimu za rekodi mbalimbali za Yanga kuhusu ubingwa wa ligi, pamoja na historia ya Ligi Kuu Tanzania Bara, haya sasa...

**1. Inaongoza kwa kutwaa mara 29**

Yanga imetwaa ubingwa mara 29 sasa kwenye vipindi na misimu tofauti na inaendelea kuwa timu iliyotwaa mara nyingi zaidi tangu kuanza kwa mfumo wa ligi Tanzania mwaka 1965.

Yanga ilianza kuutwaa ubingwa wa Tanzania mwaka 1968, ikishindwa kulipata lilipoanzishwa mwaka 1965 lilipochukuliwa na Simba wakati huo ikiitwa Sunderland mara mbili, mwaka 1965 na 1966, klabya mwaka 1967 kuchukuliwa na Cosmopolitan.

Wakati Yanga ikiwa inaongoza kwa kutwaa ubingwa mara nyingi, Simba inashika nafasi ya pili kwa kutwaa mara 22, Mtibwa Sugar imetwaa mara mbili mwaka 1999 na 2000.

**2. Mara nne kutwaa mfululizo ('back to back')**

Inakuwa ni mara ya nne kwa Yanga kutwaa ubingwa mara mbili mfululizo. Ingawa imeshawahi kutwaa mara tano mfululizo kuanzia mwaka 1968 hadi 1972, lakini hapa tunazungumzia mara mbili mfululizo tu.

Ilianza kufanya hivyo mwaka 1996 na 1997, ikarudia tena 2005 na 2006, ikatwaa tena msimu wa 2007/08 na 2008/09, kabla ya kurudia ilichokifanya mara tatu, msimu uliopita na huu.

**3. Inaziongoza timu za Dar**

Yanga imeendeleza rekodi ya timu za Dar es Salaam kutwaa ubingwa mara nyingi zaidi kuliko za mikoa mingine.

Kwa jumla timu za Dar es Salaam zimechukua ubingwa mara 54, Yanga ikitwaa mara 29, Simba mara 22, Pan African na Cosmopolitan na Azam FC ambazo zote zimechukua mara moja, dhidi ya mara tano ya timu za mikoani ambazo ni Mtibwa Sugar iliyotwaa mara mbili 1999 na 2000, Mseto ya Morogoro iliyotwaa mwaka 1975, Tukuyu Stars mwaka 1986, Coastal Union ikilichukuwa mwaka 1988.

**4. Miaka 58, timu tisa**

Ingawa timu ni nyingi zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara tangu lianzishwe mwaka 1965, lakini mpaka sasa ni timu tisa tu ambazo zimetwaa ubingwa huo.

Ni miaka 58 imepita, lakini ambazo zimeshaonja raha ya kulibeba ni Yanga, Simba, Mseto, Cosmopolitan, Pan African, Tukuyu Stars, Coastal Union, Azam, na Mtibwa Sugar tu.

**5. Ligi Kuu Bara ilivyoanzishwa**

Lilikuwa ni wazo la Kocha wa Timu ya Taifa ya wakati huo raia wa Yugoslavia, Milan Celebic, mnamo mwaka 1964 ikiwa ni njia ya kupata wachezaji wa timu ya taifa.

Alitaka ianzishwe ligi ya klabu, badala ya mashindano ya Sunlight Cup (baadaye Taifa Cup) yaliyokuwa yanazishirikisha timu za majimbo baadaye mikoa.

Ingawa timu za Simba wakati huo ikiitwa Sunderland na Yanga zilikuwapo, lakini zilikuwa zikicheza na timu za mikoa ya Pwani tu ambayo sasa ni Dar es Salaam.

Mwaka 1965, Chama cha Mpira wa Miguu (FAT), kikaanzisha Ligi ya Taifa ikiwa inashirikisha timu nane na hapa ndio ukawa mwanzo Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ilikuwa ikipitia hatua mbalimbali za mifumo, ikianza kwa mtindo wa mtoano mwanzo hadi mwisho, baadaye makundi, mpaka aina hii ya ligi tuliyonayo leo.

**JE, WAJUA?**



DAVID de Gea ameokoa penalti 13 tu kati ya 72 walizokabiliwa nazo Manchester United kipa huyo akiwa langoni, ikiwa ni rekodi mbaya zaidi. Aidha, hakuweza kuokoa penalti hata moja kwenye fainali ya Ligi ya Europa mwaka 2021 dhidi ya Villarreal.



# Waliofyeka miti 8,000 Msitu wa Mkola kukiona

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameagiza kukamatwa watu watano wanaodaiwa kufyeka miti 8,000 iliyopandwa kwenye Hifadhi ya Msitu wa Mkola.

Akikagua mwishoni mwa wiki uharibifu kwenye msitu huo, Serukamba alisema wananchi hao wamekata miti na kufungua mashamba huku wengine wakianzisha makazi na kuendesha shughuli za ufugaji.

"Naagiza hawa waliovamia msitu huu wakamatwe haraka, serikali haitavumilia mtu yeyote atakayefanya shughuli za kilimo, ufugaji na ujenzi kwenye Hifadhi ya Msitu wa Mkola, uliopo Kata ya Mgori, Wilaya ya Singida Vijijini kwa kuwa uharibifu uliofanyika eneo hilo una athari endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo," alisema.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakitoa vitisho kwa viongozi wa kijiji wakidai hawana maeneo mengine ya kuendesha shughuli zao.

Serukamba alimwagiza Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kijiji cha Msikii, kuwasilisha majina ya watu wote wanaolima katika maeneo hayo kwa kuwa ndiyo wanao tuhumiwa kukaidi amri ya serikali.

Alizitaka serikali za vijiji kutumia sheria na taratibu kuhakikisha msitu huo unalindwa kwa gharama yoyote bila kumwonea mtu.

Naye Mkuu wa Wilaya Singida, Paskas Muragili, alisema msitu huo wenye hekta 1393.6 una umuhimu mkubwa katika utunzaji wa mazingira na vijiji hivyo viliwahi kutoa Sh. milioni 17 kwa ajili ya utunzaji wa msitu huo na lazima utunzwe.

Alisema mwaka juzi walishirikiana na vijiji hivyo wakapanda miti 6,000 na mwaka jana wakapanda tena miti 8,000, lakini inashangaza kuona miti imekatwa yote na mingine imeliwa na mifugo jambo ambalo serikali haitalifumbia macho.



Meneja Uanachama na Masoko wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) makao makuu, Hipoliti Lelo, akitoa mada kuhusu vifurushi na huduma zinazotolewa na mfuko huo kwa waandishi wa habari wanaoandika habari za Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# KOICA yatoa mil. 200/- mafunzo vijana kujiajiri

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la Ushirikiano wa Kimataifa la Serikali ya Korea Kusini (KOICA), limetoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya ujuzi kwa vijana wa kike na wa kiume ili kujiajiri wenyewe na kujiinua kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Mkurugenzi wa Utahini na Utunuku wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Francis Komba, alisema mafunzo hayo yanatolewa kupitia mradi wa ujuzi wa ajira kwa maendeleo nchini Tanzania (E4DT) na fedha zitatumika kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, uatamizi na kuwaongezea ujuzi vijana watakaokuja na mawazo ya kibunifu.

Alisema mradi huo utawasaidia vijana kupata mafunzo ya ujasiriamali, kukuza ujuzi katika bunifu zao na watapata mafunzo ya miezi minne, miwili itatolewa darasani na miwili mingine hutolewa mafunzo ya vitendo.

"Sisi kama VETA tumeomba mafunzo haya yatambulike kimataifa ili vijana wetu waweze kupata nafasi ya kufanya kazi katika miradi mikubwa inayoendelea nchini," alisema Komba.

Komba alifafanua kuwa mradi huo umelenga kunufaisha vijana 4,000 nchini katika mikoa ya Manyara, Lindi, Dodoma na Dar es Salaam huku Mkoa wa Dodoma ukitarajia kuchukua wanafunzi 2,200.

Naye Mkurugenzi wa KOICA nchini, Manshik Shin, aliwataka vijana kuja na ubunifu katika sekta mbalimbali za ujasiriamali katika kozi ambazo wanataka kusoma ili kujiendeleza zaidi.

Manshik alisema mradi huo umejikita pia katika sekta za afya, elimu, miundombinu, lakini kipaumbele katika awamu ya pili ya mradi ni mafunzo ya ujasiriamali.

"Fedha zipo, kinachotakiwa vijana kuja na mawazo ya kibunifu tutawasaidia kuongeza ujuzi kwenye bunifu zao ili waweze kujiajiri na kupunguza changamoto ya ajira nchini," alisema Manshik.

Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Dk. Kennedy Hosea, alisema serikali itaendelea kusimamia mfumo huo katika ngazi zote na kuhimiza ushiriki wa wanawake.

Alisema katika mradi uliopita wanawake walikuwa asilimia 18 pekee na kuona namna ya kuwaongezea fursa za kupata mafunzo hayo.

Dk. Hosea aliwataka vijana waliohitimu mafunzo hayo kuwa waaminifu na kujiongezea maarifa na kujitangaza.

# Kata zitakazoongoza kwa uchafu kupewa hati chafu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inatarajia kuanza kutoa hati chafu kwa kata zitakazokuwa vinara wa uchafu kwenye maeneo yao na kushindwa kutunza mazingira na kufanya usafi.

Ofisa Mazingira wa jiji hilo, Dickson Kimaro, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na madiwani kwenye kikao cha baraza baada ya kukabidhi vyeti vya pongezi kwa kata nne zilizofanya vizuri kwa kuweka mazingira safi kati ya 41 zilizopo.

Kimaro alisema kuwa Jiji limedhamiria kutoa hati chafu kwa kata zitakazokuwa chafu ili kuwahamasisha wananchi wao kufanya usafi wa mazingira wa kila siku kwenye maeneo yao.

Alisema, ili kuleta ushindani huo wa kutunza mazingira na kufanya usafi, jiji limetoa vyeti hivyo vya pongezi kwa kata hizo kinara wa safi.

"Jiji la Dodoma kuna kata 41, lakini zilizoonyesha na kutekeleza usafi wa mazingira ni nne tu kati ya hizo na kwenye kikao hiki cha Baraza la Madiwani zitakazostahili kupewa vyeti vya pongezi ni kata ya Ipagala, Chamwino Tambukareli na Mnadani ambazo mitaa yao imefuzu kwa usafi," alisema.

Kimaro aliwaomba wenyeviti wa serikali za mitaa kwa zile kata ambazo hazijapewa vyeti vya pongezi kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa usafi wa mazingira na kuhamasisha wananchi wao ili kujitokeza kwenye usafi.

Naye Juma Mazengo, Diwani wa Kata ya Tambukareli, aliwaasa madiwani ambao kata zao hazikufanikiwa kutoa elimu itakayowahamasisha badala ya vitisho na faini zisizokuwa na mishiko.

Mazengo alisema kupatikana kwa cheti hicho cha pongezi ni kutokana na elimu ya uhamasishaji ambayo iliwafanya wananchi kujitokeza wao wenyewe na kupenda kufanya usafi wa mazingira bila kushurutishwa.

"Niwaombe viongozi wenzangu wa ngazi za kata tuendelee kushirikiana na wananchi wetu katika suala hili la usafi wa mazingira ili jiji letu liwe kinara wa kuwa wasafi kwenye maeneo yote huku ikiwa na ustawishaji wake wa upandaji miti," alisema.





# Wenye mahitaji maalum waombewa msaada

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WATANZANIA wenye uwezo wametakiwa kuwa na utamaduni wa kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu chakula, mavazi na kugharimia huduma za matibabu ili watu wa makundi hayo waendelee kuishi.

Mchungaji wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Upatanisho, lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapo, Mikael Mwanizuwa, alitoa rai hiyo wakati kanisa hilo lilipokuwa linatoa msaada wa vitu mbalimbali kwa makundi ya wahitaji.

Makundi yaliyonufaika na msaada huo ni watu wenye ulemavu, wazee, wajane na wagane pamoja na wagonjwa ambao wanahitaji kwenda hospitalini.

Mchungaji Mwanizuwa alivitaja vitu walivyowapatia makundi hayo kuwa ni chakula, sabuni, chumvi, mavazi pamoja na fedha taslimu kwa ajili ya nauli kwa waliotoka mbali na eneo hilo pamoja na fedha ya matibabu kwa wagonjwa.

Alisema waliamua kutoa misaada hiyo baada ya kubaini makundi hayo yanaishi katika mazingira magumu na kuhitaji kusaidiwa.

Alisema viongozi wa kanisa hilo walikubaliana kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wanajamii wa eneo hilo kuchangishana vitu hivyo ili kuwasaidia wahitaji hao.

"Tulitangaza kupitia vyombo vya habari kwamba siku ya leo (jana) tutakuwa na zoezi hili, tumepokea watu wengi sana na hapa tumewagawia chumvi, miche ya sabuni na debe la mahindi kwa kila mmoja," alisema Mwanizuwa.

Mmoja wa viongozi wa kanisa hilo, Samwel Mwahalende, alisema misaada waliyoitoa ni sawa na sadaka ambazo hutoa kila siku kwa lengo la kumtukuza Mungu na ni utaratibu wa kanisa hilo kutoa misaada.

Alisema michango hiyo wameikusanya kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo waumini wa kanisa hilo pamoja na majirani ambao baadhi yao hawasali katika kanisa hilo.

Baadhi ya watu walionufaika na msaada huo, waliushukuru uongozi wa kanisa hilo kuwa vitu walivyopatiwa vitawasaidia kuendesha maisha yao na wakawaomba watu wengine wenye uwezo kuendelea kuwasaidia.

Mmoja wa wanufaika hao, Salome Timotheo, ambaye ana ulemavu wa miguu, alisema hana uwezo wa kutafuta fedha kutokana na hali aliyonayo na maisha yake yamekuwa ya kubahatisha kwa muda mrefu.

Alisema kutokana na hali hiyo anahangaika na mume wake kutafuta fedha ya kununulia chakula na mahitaji mengine na sehemu kubwa wanategemea misaada.

"Mimi kama mnavyoniona sitembei bali natambaa kwa hiyo uwezo wa kujitafutia kipato sina, namshukuru Mungu kwa waumini wa kanisa hili pamoja na viongozi wao kwa msaada huu walioutupa, chakula walichotupatia kitatusaidia sana," alisema Salome.

Naye Herena Mwasomola ambaye ni mzee alisema kutokana na umri wake anashindwa kujitafutia chakula na mahitaji mengine na msaada aliopewa ni muhimu kwake na utamsaidia kuendesha maisha yake.

Aliutaka uongozi wa kanisa hilo kuendeleza utaratibu huo wa kuwasaidia watu wenye mahitaji kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujitafutia kama yalivyo makundi mengine.



Mchungaji wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Upatanisho lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, Mikael Mwanizuwa (kushoto), akikabidhi msaada wa nguo kwa baadhi ya watu wa makundi maalumu jana wakati wa ibada maalumu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanafunzi sita wachunguzwa kujihusisha mapenzi jinsia moja

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO sita wa shule za msingi, sekondari na vituo vya kulelea watoto yatima katika Kata ya Iwambi, jijini hapo Mbeya wamekamatwa kwa ajili ya kuchunguzwa kuhusu tuhuma zinazowakabili za kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Diwani wa Kata ya Iwambi, Humphrey Ngalawa, aliyasema hayo wakati wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa shule mbalimbali za kata hiyo ambayo iliratibiwa na Dawati la Jinsia la Chuo cha Afya cha Jiji la Mwanza.

Alisema baadhi ya wanafunzi hao wamekuwa wakiingiliana wenyewe kwa wenyewe wanapokuwa shuleni na kwenye vituo vya kulelea watoto yatima jambo linaloashiria mmomonyoko wa maadili kwa watoto kuongezeka.

Alisema watoto waliokamatwa ni wa Shule ya Msingi Iwambi, Shule ya Sekondari Iwambi na wa Kituo cha kulelea watoto yatima cha Iwambi ambao wanaendelea kufuatilia ili kuwabaini na wengine wanaojihusisha na vitendo hivyo.

"Tunafuatilia ili tubaini na wengine wanaoshiriki vitendo hivyo, kwa hiyo tunaendelea kuwahoji hawa, mbaya zaidi ni kwamba miongoni mwa hawa watoto ni wale wanaolelewa kwenye kituo chetu cha kulelea watoto yatima," alisema Ngalawa. Alisema watafuatilia katika shule zote za kata hiyo ili kuhakikisha wanakomesha tabia hizo ambazo zimeanza kuibuka kwa kasi kwa vijana wa kiume na wa kike.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Iwambi, Nicholous Kipete, aliwataka wanafunzi kuepuka vishawishi mbalimbali ambavyo vinawalazimisha kuingia kwenye mapenzi ya jinsia moja vitendo ambavyo ni kinyume na maadili ya kiafrika.

Alisema wapo watu wamekuwa wakiwashawishi watoto kuingia kwenye vitendo hivyo kwa kuwapa vitu mbalimbali, kuwashawishi kwa maneneo na kutoa ahadi mbalimbali ambazo nyingi ni za uongo.

Vilevile, aliwataka wanafunzi kutoa taarifa wanapobaini kuwa kuna wenzao wanafanya vitendo hivyo vya kishetani ama kuna mtu yeyote anawashawishi kushiriki.

"Nawaomba wanangu msikubali kushawishika na mtu yeyote kufanya vitendo hivi, vitendo hivi ni vya kishetani kabisa na ni kinyume kabisa na mila na desturi zetu za kiafrika, mtu yeyote akikushawishi tuleteeni taarifa," alisema Kipete.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Mbeya, Francis Ngelela, alisema kampeni ya kupinga mapenzi ya jinsia moja inaendelea nchi nzima kutokana na kuanza kushamiri katika maeneo mbalimbali nchini.

# Waandishi wa habari wakumbushwa kuzingatia maadili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAANDISHI wa habari mkoani hapo wametakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, miiko na sheria za taaluma hiyo ili kuepuka kuingia kwenye migogoro na serikali pamoja na kuepuka kuzua taharuki miongoni mwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe mkoani humo, Jaffar Haniu, alitoa ushauri huo juzi alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kwenye maadhimisho ya miaka 30 ya Uhuru wa Vyombo vya Habari yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Mbeya (MBPC).

Aidha, Haniu ambaye kitaaluma ni mwandishi wa habari aliwataka wanahabari nchini kuwa wazalendo kwa taifa lao kwa kuepuka kutumiwa na mataifa ya nje kutoa taarifa zinazoweza kuchafua taswira ya nchi.

Alisema taaluma ya habari ni nyeti ili kuepuka kuzua matatizo ni vyema kila mwandishi afanye kazi kwa kuzingatia miiko ya taaluma hiyo.

"Nawaombeni pia mjitahidi sana kujiunga na vyama vya kitaaluma vikiwamo hivi vya mikoa na vya kikanda, mimi wakati nafanya kazi kwenye Shirika la Utangazaji la Taifa, nilishawahi kupata nafasi ya kwenda kukaa Afrika Kusini miezi mitatu nikifanya kazi pale, nilipata nafasi hiyo kupitia MISA Tan," alisema Haniu.

Awali, akisoma risala ya MBPC, Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Elizabeth Nyivambe, alisema chama hicho kimekuwa kikifanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na umaskini kwa wanachama wake hasa kwa kuanzisha miradi ya kuwanufaika.

Alisema chama hicho kimeanzisha VICOBA na mpaka sasa kina mtaji wa zaidi ya Sh. milioni 30 zinazotokana na michango ya wanachama, wadau pamoja na faini mbalimbali ambazo wanachama wanatozwa.

Alisema pamoja na kazi kubwa ambayo waandishi wa habari wanaifanya, lakini wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo baadhi ya taasisi za umma na binafsi kutowapatia ushirikiano wanapohitaji taarifa.

"Baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri wanawazuia watendaji walio chini yao kutoa taarifa kwa waandishi kuhusu taasisi zilizo chini yao jambo ambalo linasababisha hata sisi waandishi tushindwe kutekeleza vizuri majukumu yetu," alisema Elizabeth.

Alisema waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya wamekuwa wakifanya kazi kwa weledi hali inayowafanya wawe wanajizolea tuzo mbalimbali zinazotolewa na taasisi tofauti za ndani na nje ya nchi.



# Serikali yaahidi kujenga kituo kurekebisha watumia dawa kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itajenga kituo cha kurekebisha vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya huko Kangagani Pemba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023-2024.

Hayo yalisemwa juzi katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, wakati akijibu hoja za wajumbe waliochangia makadirio matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema serikali imetenga eneo la Kangagani lenye ukubwa wa eka sita ambalo litajengwa kituo kitakachotumiwa na vijana kurekebisha tabia kuachana na dawa za kulevya ambalo ni janga la kitaifa.

"Serikali imetenga eneo la Kangagani kwa ajili ya kujenga kituo cha kurekebisha tabia kwa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kama ilivyo kwa upande wa Unguja huko Kidimni wilaya ya kati Unguja," alisema.

Alitoa ufafanuzi huo baada ya wajumbe wa baraza hilo kuhoji hadi sasa kwa upande wa Pemba hakuna kituo cha kurekebisha vijana kuachana na uraibu wa dawa za kulevya baada ya kubainika tatizo hilo kuongezeka kisiwani humo.

Waziri Harusi alikiri umuhimu wa uwapo wa kituo hicho na kutoa mfano wa kituo kilichopo Kidimni Wilaya ya Kati Unguja kilivyosaidia kurekebisha tabia kwa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya na kuwapo kwa mafanikio makubwa.

Alisema kituo cha Kidimni tayari kina uwezo wa kutibu vijana wanaotumia uraibu wa dawa za kulevya 50 kwa mwaka na kitakapomalizika baadhi ya majengo yake kitakuwa na uwezo wa kutibu vijana 200 kwa mwaka.

Akifafanua kuhusu baadhi ya tuhuma za kukimbia kwa vijana 60 waliofikishwa katika kituo hicho kupata tiba, alisema sababu kubwa ni vijana hao kutokuwa tayari kupata huduma za matibabu kurekebisha tabia zao na kuachana na dawa za kulevya.

Alisema walipelekwa katika kituo hicho kwa kulazimishwa na wazazi wao na ili uweze kuachana na matumizi ya dawa za kulevya ni suala la hiyari ya mtu.

"Ni kweli wapo vijana wapatao 60 wamekimbia katika kituo hicho baada ya kuletwa kupata tiba ambapo sababu yake kubwa ni kwamba hawajawa tayari kuachana na matumizi ya dawa za kulevya...ili mtu aweze kuachana na dawa za kulevya ni hiyari yake mwenyewe na sio kulazimishwa na wazazi," alisema.

Hata hivyo, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipitisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2023-2024 jumla ya Sh. 16,778,429,375,00 kwa kazi za

# Balozi Norway ataka wanawake waungwe mkono uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, amesema kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kuwaunga mkono wanawake Zanzibar ili kushika nafasi za uongozi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa haki za wanawake katika Ofisi ya TAMWA, Tunguu nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema Norway inashirikiana na Tanzania kwa miaka 60 sasa katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii, ikiwamo masuala ya kuwaunga mkono wanawake katika uongozi.

Alisema pia wataendelea kufungua milango zaidi kukaribisha asasi za kiraia, waandishi wa habari na jamii wakiamini kuwa wana mchango mkubwa kwenye jamii na kwamba wanapaswa kuungwa mkono.

Balozi huyo anaamini kuwa suala la wanawake kuwa viongozi linaweza kuchukua muda mrefu, lakini kama watajengewa uwezo watakuwa na uthubutu, kujiamini na kushughulikia changamoto kuanzia ngazi ya familia.

Aidha, alisikitishwa na vitendo ya udhalilishaji kwa wanawake na kusema kuna haja ya kuunganisha nguvu zaidi katika mapambano hayo huku lengo likiwa ni kuwaweka wanawake katika mazingira salama.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema wanawajengea uwezo wanawake kuwa viongozi na kwa kiasi fulani kuna mafanikio makubwa na wapo ambao wameshika nyadhifa hizo.

Naye Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mahmoud, alisema licha ya wanawake kujengewa uwezo, pia huwajengea uwezo wahamasishaji jamii ili kutoa elimu katika jamii kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake.

Ujio wa Balozi wa Norway, ni utekelezaji mradi wa kuhamaisha wanawake Zanzibar kushiriki kwenye nafasi za uongozi (SWIL) ambao unatekelezwa na TAMWA, ZAFELA pamoja na PEGAO kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway.

Katika hatua nyingine Balozi huyo alikutana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kuisifu Tanzania kuendelea kuwa nchi ya amani, yenye raia wenye upendo, ushirikiano, umoja na utulivu wa kisiasa.

Alisema Tanzania ni kielelezo cha nchi ya mfano barani Afrika na kwengineko duniani kuwa ni taifa lenye demokrasia kwa kutekeleza haki za binadamu na siasa safi.

Alimwahidi Rais Mwinyi, kwamba Serikali ya Norway daima itaendelea kuiunga mkono Tanzania ikiwamo Zanzibar kwenye sekta za maendeleo.

Rais Mwinyi, alisema Zanzibar imenufaika na fursa nyingi kutoka Norway zikiwamo sekta za afya, umeme na elimu na uhusiano wa Norway na Tanzania utakumbukwa zaidi kwa kuinufaisha Zanzibar kupitia sekta ya umeme, hasa wa kutoka Tanga hadi Pemba na Dar es Salaam hadi Zanzibar.




Balozi wa Norway Nchini Tanzania, Elisabeth Jacobsen (kushoto), akipokea zawadi ya mkoba wa ukili kutoka kwa Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, baada ya kumaliza mkutano na wadau wa utetezi wa haki za wanawake, uliofanyika jana ofisi za TAMWA Tunguu nje ya Mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ujenzi bandari kavu Fumba wanukia

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar kupitia shirika la bandari imetiliana saini na kampuni ya Fumba Inland Container Deport Limited kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu (ICD) katika eneo la Fumba nje ya mji wa Zanzibar.

Mkataba huo kwa niaba ya wizara umesainiwa jana mjini Zanzibar na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Nahat Mohamed Mahafoudh na kwa upande wa Kampuni ya Fumba Inland Contaner Deport Limited umewakilishwa na mwakilishi, Twalib Khamis.

Akizungumza baada ya kuwekwa saini kwa mkataba huo Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amepongeza jitihada zilizochukuliwa na wadau wa taasisi mbalimbali kwa kusimamia kwa karibu kukamilika kwa taratibu za kuanza ujenzi wa bandari hiyo ya kushushia na kupakia makontena ya mizigo.

Waziri Dk. Khalid alisema kukamilika kwa ujenzi wa bandari hiyo na kuanza kutumika kutasaidia kuondoa changamoto ya msongamano wa ushushaji wa makontena katika Bandari ya Malindi.

Pia alisema kukamilika kwa bandari hiyo kutawezesha kuondoa changamoto ya usafirishaji wa makontena yaliokuwapo Mombasa Kenya na badala wake kushushwa moja kwa moja katika Bandari ya Fumba ndani ya kipindi cha muda mfupi.

Aidha, Dk. Khalid aliwahakikishia wajenzi wa bandari ya Fumba kuwa, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Bandari watatoa kila aina ya ushirikiano, kuhakikisha ujenzi unafanikiwa kwa haraka ili kuwaondolea changamoto wananchi wa Zanzibar hasa katika upatikanaji wa bidhaa kwa bei nafuu.

Naye mwakilishi kutoka kampuni hiyo, Fumba Inland Container Deport Limited, Twalib Khamis, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa ujasiri wa kuchukua hatua za haraka za kupunguza tatizo la msongamano wa meli na mizigo katika Bandari ya Malindi.

Khamis aliihakikishia serikali kuwa, kampuni yao ina uwezo mkubwa wa kuifanya kazi hiyo kutokana na uzoefu wao na watahakikisha kazi inakamilika kwa muda mfupi ndani ya makubaliano ya mkataba.

"Tutahakikisha kazi hii inakamilika kwa wakati na meli ya kwanza itaanza kushusha makontena mwezi Agosti ndani ya wiki ya kwanza," alisema Khamis.

# Muhimbili yashtukia ongezeko shida ya ugumba kwa wanaume

## • Mloganzila yaweka mkakati kuwatibu

**Na Elizabeth Zaya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), Tawi la Mloganzila, inatarajia kuanzisha huduma maalum ya kutibu tatizo la ugumba kwa wanaume.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi Kitengo cha Upasuaji wa MNH Mloganzila, Dk. Godlove Mfuko, alisema huduma hiyo inatarajiwa kuanza hivi karibuni na kabla ya kuanza watatoa taarifa kwa umma.

Dk. Mfuko alisema tayari maandalizi ya kuanzisha huduma hiyo yalishafanyika ikiwamo kuandaa madaktari wabobezi katika eneo hilo ambao walipelekwa nje kwa ajili ya kuongeza ujuzi mahsusi kwa kazi hiyo.

Alisema miongoni mwa maeneo yatakayolengwa zaidi katika utoaji wa huduma hiyo ni tiba dawa, saikolojia na upasuaji.

"Huduma hii itaanza muda si mrefu katika hospitali yetu ya Mloganzila na tunashukuru hatua hii inawezeshwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka miundombinu ya kufanikisha huduma hii, wataalamu wabobezi na vifaa vya uhakika katika hospitali yetu ya Mloganzila," alisema Dk. Mfuko.

Alisema tatizo la ugumba halipo kwa wanawake tu. Hata wanaume limekuwa likiwatesa. Lakini wanaume hawawezi kusema ni wagumba kwa sababu wanaona aibu tofauti na ilivyo kwa wanawake na ndiyo maana wameona kuna umuhimu wa kuwasaidia.

Alisema tatizo hilo la ugumba kwa wanaume kwa sasa ni kubwa na imebainika si wale wanaokwenda katika kliniki ndogo wala kubwa. Kote wamekuwa wakiwabaini waathirika.

Alisema zipo sababu mbalimbali zinazochangia tatizo hilo la ugumba kwa wanaume na kutaja baadhi kuwa ni pamoja maambukizi kwenye njia ya mkojo, uvimbe kwenye viungo vya uzazi, ulevi, magonjwa ya shinikizo la damu, kisukari, tatizo kwenye mishipa ya damu na hata tatizo la kisaikolojia.

Sababu nyingine ya ugumba kwa mwanaume, alisema ni maumbile pamoja na tatizo la nguvu za kiume.

"Kupitia huduma hii tunayoanzisha itasaidia wote wenye shida hii hata kama mtu amepooza. Kuna vifaa maalum ambavyo vitatumika kutoa mbegu zake na kuzipandikiza.

"Na sasa hivi wanaokumbwa na tatizo hili la ugumba si wale wenye umri mkubwa pekee. Hata vijana wapo wengi tu na ndio maana tumeweka pia na hiyo huduma ya saikolojia ili tuguse kila eneo.

"Na kadri tutakavyoendelea kulishughulikia ndivyo tutazidi kuboresha zaidi. Huduma hizi zimekuwa zikifanywa lakini siyo kwa ukamili. Kwa hiyo hii tunayoanzisha itakuwa imekamilisha kila kitu katika eneo hili," alisema.




Watoto wenye ulemavu wanaolelewa katika kituo cha St.Justin kilichopo mjini Musoma, walezi wao na wafanyakazi wa kituo hicho wakifurahia baada ya kukabidhiwa msaada wa hundi ya dola 10,000 kutoka kwa Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko, katika hafla ilifanyika kituoni hapo mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tembo Nickel, Jeshi Polisi waingia mkataba bil. 1/- kuimarisha ulinzi

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

KAMPUNI ya Tembo Nickel, imeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa zaidi ya Shilingi bilioni moja na Jeshi la Polisi Tanzania, kudumisha ulinzi na usalama katika jamii inayozunguka mradi wa Kabanga Nickel uliopo wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera.

Pamoja na mambo mengine, katika utekelezaji wa mkataba huo kitajengwa kituo cha polisi daraja A, Kata ya Bugarama wilani humo, nyumba za askari na kununua gari la polisi.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Awadhi Juma, alisema jukumu la kuhakikisha usalama wa wananchi na wawekezaji, wanalitekeleza ili kuhakikisha usalama ndani ya nchi unaendelea kuimarika.

Alisema, wana utaratibu wa kutoa ulinzi mahususi kwa taasisi, utiaji saini makubaliano hayo ni utekelezaji wa sehemu ya majukumu yao.

"Tunaposema tunajenga kituo cha polisi daraja A, maana yake hiki kituo daraja A ni kituo sawa na vile vyenye hadhi ya kituo cha mkoa, lakini hiki sasa kitajengwa katika kata hii na kuhudumia tarafa hii ya Rulenge, naamini kwa kushirikiana na wananchi usalama kawenye eneo letu na mradi wetu utaimarika sana," alisema Kamishina Awadhi.

Meneja Mkaazi wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu, alisema ushirikiano wao na serikali pamoja na wananchi umeundwa kwa lengo la kuhakikisha uwapo wa thamani inayotokana na usawa na uaminifu.

Alisema utiaji saini wa mkataba huo ni makubaliano ya kuboresha ulinzi na usalama katika vijiji vilivyozunguka Mradi wa Kabanga Nickel na wilaya yote ya Ngara.

Kampuni ya Tembo Nickel inatambua kuna uwezekano kutokea ongezeko la watu katika jamii inayozunguka eneo la mradi wa Kabanga Nickel kwa lengo la kutafuta fursa na kwamba itakuwa na mpango maalum wa kutoa elimu kwa umma kupata fursa katika mradi ili kupunguza madhara ya ongezeko la watu.

Kampuni ya Tembo Nickel inaihakikishia jamii ya Wangangara pamoja na Watanzania kuwa imejipanga vyema kushirikiana na Jeshi la Polisi kama mmoja wapo wa wadau muhimu katika jamii inayozunguka mradi ili Jeshi la Polisi la Tanzania liweze kuboresha shughuli zake katika eneo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, aliyekuwa mgeni rasmi katika shughuli hiyo, alipongeza kampuni hiyo kwa uamuzi wake wa kutaka wananchi wanaozunguka mradi huo kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana katika mgodi huo ili kuinua maisha na uchumi wa mkoa huo.

"Tembo Nickel mna kazi ya kuinua maisha ya wananchi wa eneo hili na wananchi niwaambie tu sio kwamba Tembo Nickel watakuja kuwawekea fedha mifukoni mwenu, watakachofanya ni kuboresha huduma za jamii.

"Kwa mfano kama suala lilikuwa ni mnashindwa kufanya shughuli kwasababu ya usalama sasa usalama ndio huu unaimarishwa, najua wanafanya kazi kubwa kuboresha miundombinu ya afya ya elimu, umeme utakuja, ajira zaidi ya 1,500 watatoa mradi utakapoanza, mkoa wetu wa Kagera kwa naamini uchumi wake utakuwa, kwa sasa kwa kigezo cha GDP ndo mkoa wa mwisho kwa umaskini Tanzania, lakini uwapo wa mgodi huu utabadili mambo," alisema.

# Makalla aitaka DAWASA kuongeza uzalishaji maji

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kuongeza nguvu katika uzalishaji wa maji kupitia visima virefu vya Kigamboni.

Amesema hatua hiyo itasaidia kwa kiwango kikubwa visima hivyo kuongeza upatikanaji wa maji na kukidhi mahitaji ya wananchi kipindi cha kiangazi hadi maeneo ya pembezoni.

Makala aliagiza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya uchimbaji na usafishaji wa visima virefu vya Kigamboni vinavyochimbwa na kusafishwa ili kuongeza huduma.

Alisema DAWASA inapaswa kuhakikisha visima virefu vinavyotakiwa kuchimbwa, vinachimbwa haraka na kwa vile vinavyotakiwa kusafishwa, kazi hiyo ifanyike kwa kasi ili visaidie katika upatikanaji wa maji wakati wa kiangazi.

Alimtaka Mkandarasi wa Kampuni ya Serengeti kurejea kazini mara moja ili akamilishe kazi ya uchimbaji wa visima na kusafisha vilivyopo.

"Leo nimekuja rasmi kuona maendeleo ya mradi wa visima na kujua mpango uliopo wa kuhakikisha visima vyote 20 vinakamilika na vinatoa maji sanjari na maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyoyatoa wakati wa ziara yake Kigamboni.

"Tunahitaji kuwa na maji ya kutosha ya kuhudumia wananchi wote wa Kigamboni, katikati ya jiji na maeneo ya pembezoni hususani wakati wa kiangazi," alisema Makalla.

Alisema visima saba vinavyotoa maji kwa sasa havitoshi kuhudumia wananchi wote, hivyo inahitajika nguvu zaidi ya kuongeza visima ili wakati wa kiangazi pasiwe na changamoto ya wakati uliopita.

Aliitaka Menejimenti ya Mamlaka kuandaa mpango kazi wa ujenzi wa miundombinu ya kupokea maji kutoka kwenye visima virefu na kuyapeleka kwenye bomba kuu.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, aliahidi kufanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa ili kuimarisha utoaji wa huduma ya maji kwenye katika yote.

Mwakilishi wa Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Shabani Mkwanywe, alisema mamlaka imepokea maelekezo yote ya Mkuu wa Mkoa na utekelezaji wake utaanza mara moja.

Alisema kuwa tayari mamlaka imeandaa mpango kazi wa namna ya kuongeza uzalishaji wa maji kupitia visima virefu vya Kigamboni pamoja na maeneo mengine ili kuongeza upatikanaji wa maji na kukabiliana na changamoto wakati wa kiangazi.

## Mzee wa miaka 72 alivyouawa na tembo akienda kuchimba mihogo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji na Kata ya Namikango, Tarafa ya Mnero, Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Issa Mnunduma (72) ameuawa kwa kukanyagwa na tembo, wakati akienda shambani kuchimba mihogo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwenye kata hiyo na kuthibitishwa na Diwani Siasa Chikawe na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nachingwea, Adinani Mpyagila, Mnunduma alikutwa na umauti huo Mei 5, saa 10 alasiri.

Diwani Chikawe alisema siku ya tukio, Mnunduma akiwa na baiskeli umbali wa kilomita 50 kutoka nyumbani kwake, alikutana na kundi la tembo wakiwa katika matembezi yao na walimshambulia kwa kumkanyaga maeneo mbalimbali ya mwili na kufariki papo hapo.

"Mwananchi huyu amekanyagwa na tembo akiwa njiani kuelekea shambani kuchimba muhogo kwa ajili ya kunywea chai asubuhi," alisema Chikawe.

Alitaja maeneo aliyokanyagwa na kumchomwa na meno yao kuwa ni kichwani na kumvunja sehemu ya kifuani, shingoni na kumkanyaga miguuni, kisha kuendelea na safari zao za kuharibu mazao kwenye mashamba ya wakulima.

Alisema, kutokana na tukio hilo, walitoa taarifa mamlaka husika ya wanyama pori (TAWA), kituo kilichopo Kijiji cha Nditi na askari walifika na kuwaondoa wanyama hao kuwarejesha msituni.

Chikawe alisema wakati askari wakiwaondoa wanyama hao kwa kupiga risasi za juu, tembo wawili walionyesha jeuri na kuwafuata askari kutaka kuwashambulia, lakini kabla ya lengo lao halijatimia, mmoja alipigwa risasi na kufariki papo hapo huku mwingine akikimbia na kuwafuata wenzake msituni.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nachingwea, Adinani Mpyagila na Mkuu wa wilaya hiyo, Mohamedi Hassani Moyo, wamekiri kuuawa kwa mkulima huyo na kusema wanyama hao wameondolewa na askari wanyama pori kituo cha Nditi na kuelekea msituni wanakoishi.

Kuhusu kuuawa kwa tembo anayedaiwa kuonyesha kiburi wakati wakiondolewa kurejeshwa msituni na askari hao, viongozi hao walisema mnyama huyo alikuwa na lengo baya kwa walinzi hao.

"Ni kweli tembo wawili kati ya kundi lililokuwapo walionyesha jeuri ya kukataa kurejea msituni na kuwafuata askari ndipo mmoja akapigwa risasi."

TATU TIBASHENGWA

# Kutoka ndoto za mwanasheria hadi mhasibu mashuhuri



Tatu Tibashengwa akiwa ofisini kwake. **PICHA: HALFAN CHUSI**

**Na Halfan Chusi**

AKIWA msichana mdogo, Tatu Tibashengwa alitaka kuwa mwanasheria. Kilichomfanya atamani taaluma hiyo, ni mwanasheria ni filamu iitwayo Neria.

Anasema "...nilimpenda sana mwanasheria aliyekuwa mmoja wa washiriki wa filamu hiyo kwa namna alivyowatetea wateja wake. Hilo likanifanya nitamani kuwa mwanasheria."

Hata hivyo, alipoufikia ujana, alihamishia mapenzi yake katika uhasibu - mambo ya hesabu za fedha.

Alipohitimu kidato cha nne, akaamua kuchukua mchepuo wa ECA (Uchumi, Biashara na Uhasibu) Kidato cha 5 na 6. Akafaulu vizuri.

Akawa na shauku katika ulimwengu wa uchumi na akanuia kufanya kila awezalo kusomea Shahada ya Kwanza ya Biashara na Uhasibu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Akakubaliwa kujiunga na chuo kikuu hicho kikongwe zaidi nchini. Alihitimu mwaka 2010 (miaka 13 iliyopita).

Baada ya kuhitimu shahada ya uhasibu, mwaka 2012 alihitimu cheti cha taaluma ya juu ya uhasibu (CPA) kinachotambuliwa Bodi ya Wahasibu Tanzania. Baadaye alifanya kazi kwa miaka miwili katika moja ya taasisi kisha akaomba kujiunga na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited. Ikamwajiri kwa cheo ya Ofisa wa Udhibiti wa Ndani kuanzia mwaka 2015.

Tangu ajiunge na GGML, Tatu amekuwa mmoja wa wafanyakazi hodari. Mnamo 2017, alipandishwa cheo hadi Msimamizi Daraja la Pili wa Udhibiti wa Ndani katika Idara ya Fedha.

Mazingira ya kazi ndani ya GGML yamemruhusu Tatu kujifunza ujuzi mpya kutokana na mwingiliano wa mara kwa mara na wafanyakazi wenzake.

Baada ya kupanda cheo ndani ya miaka miwili akiwa GGML, Tatu anasema alikuwa mfanyakazi aliyejitolea kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu. Anaamini ndicho kilichowavutia viongozi wake.

Mnamo mwaka wa 2019, alichaguliwa kujiunga na Programu ya Masuala ya Uongozi - MBA kutoka Chuo cha Uongozi cha Afrika Mashariki na Kusini (ESAMI) ambako alihitimu Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara (MBA).

Katika shahada hiyo, Tatua alijifunza mambo mbalimbali kuhusu uongozi, utawala, usimamizi wa miradi na sheria za biashara. Zikamsaidia kuendelea kuifanya kazi yake vizuri zaidi.

Mnamo mwaka 2020, Tatu alihitimu mafunzo ya Kozi (cheti) ya Ukurugenzi kutoka Taasisi ya Wakurugenzi nchini. Programu hizo pia zilikuwa sehemu muhimu ya mipango ya GGML kuwaandaa wafanyakazi wake kuwa viongozi wa baadaye ili kutimiza lengo la kuwawezesha Watanzania wengi kushika nafasi za uongozi ndani ya kampuni.

Tatu ambaye ni mama wa watoto watatu, anasema anatekeleza majukumu yake kwa usawa kuanzia ngazi ya familia hadi katika kampuni kutokana na ushirikiano mzuri anaoupata kutoka pande mbalimbali za jamii inayomzunguka.

"Hata kunapokuwa na tatizo katika shule wanayosoma watoto wangu, nina mtu ambaye ninaweza kumtegemea, na ikitokea kunahitajika kusafiri kikazi, nina mtu wa kumsaidia majukumu mengine," anasema.

Anautaja ni mfumo wa usaidizi ambao ameutengeneza. Huhakikisha hana wasiwasi na anaweza kumudu majukumu yake ya kuwa mama na mfanyakazi kwa wakati huohuo.

Tatu ana maoni kuhusu GGML inavyosaidia wafanyakazi wake. Anasema... "kwa kweli niseme wazi kwamba unapokuwa ndani ya kampuni hii, unayo fursa pana ya kujiendeleza kitaaluma. Kwa sababu wanakuunga mkono ipasavyo.

"Kuna mafunzo mbalimbali utafaidika kuyapata ndani ya kampuni hii ikiwa ni pamoja mafunzo kazini. Pia unapata fursa ya kujifunza kutoka kwenye migodi mingine inayoendeshwa na kampuni mama ya AngloGold Ashanti katika nchi zingine na tunajifunza mambo mengi."

Kwa yeyote ambaye bado anasita kuingia kwenye taaluma ya uchimbaji madini, Tatu anasema... "GGML ni mwajiri mzuri ambaye anajali watu wake. Kuna fursa nyingi kwa mtu ambaye yuko tayari kukua kitaaluma."

Tatu anasema uwiano kati ya wafanyakazi wanawake katika sekta ya madini hauridhishi kulinganishwa na wingi wa wanaume kwenye sekta hiyo. Anasema GGML imepambana kufuta dhana hiyo kwamba kazi za migodini ni za wanaume pekee.

Kampuni ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited imeitikia wito huo kuhakikisha malengo ya kuwawezesha wanawake kujiunga na sekta ya madini yanafanikiwa.

Mapema mwaka huu, Tatu alikuwa miongoni mwa wahitimu wa kundi la nane la mafunzo ya Mwanamke Kiongozi kupitia Programu ya Female Future Tanzania (FFT) iliyoratibiwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kwa kushirikiana na Chuo cha ESAMI.

Mpango huo unalenga kuimarisha usawa wa kijinsia mahali pa kazi, kuboresha uwakilishi wa wanawake katika michakato ya kufanya uamuzi wa usimamizi na kuwavuta wanawake kwenye nyadhifa za juu za sekta ya binafsi na serikalini.

Haikuwa bahati mbaya kwamba baada ya kuhitimu mafunzo hayo ya FFT Machi mwaka huu 2023, Tatu alipandishwa cheo kushika wadhifa wa Meneja (Utawala Bora) Fedha, hatua ambayo ni muhimu kwa kampuni katika kutimiza lengo la ushirikishaji wa usawa wa kijinsia katika sekta ya madini.

## HABARI MICHEZO

# PALASA AULA TENA NAFASI URAIS NGUMI ZA KULIPWA

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limemwidhinisha bondia wa zamani wa mchezo wa ngumi za kulipwa nchini, Chaurembo Palasa, kuwa Rais wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa baada ya kuibuka mshindi kwa kupata kura 19 dhidi ya mpinzani wake wa karibu, Meja Bakari Songoro aliyepata kura 15 huku kukiwa na hakuna kura iliyoharibika kati ya 34 zilizopigwa.

Katika uchaguzi huo uliofanyika juzi, Jumamosi kwenye Ukumbi wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kusimamiwa na BMT kupitia Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Allen Alex, Palasa alikuwa kitetea nafasi yake ya urais aliyoshinda mwaka jana baada ya kumbwaga Meja Bakari Songoro kwa kura moja.

Katika nafasi ya Makamu wa Rais wa Kamisheni hiyo, Nassoro Chuma, alikuwa mgombea pekee na amepita kwa kura 28 huku sita pekee zikiwa za hapana kwa upande wake.

**Kwa upande wa nafasi ya Katibu Mkuu, George Silas, amembwaga kwa kishindo Ibrahim Kamwe 'Big Right' kwa kupata jumla ya kura 25 huku mpinzani wake huyo akiambulia kura nane pekee.**

Nafasi ya mweka hazina ilikuwa na mgombea mmoja pekee, Elius Mlundwa, ambaye amepita kwa jumla ya kura 31 huku kukiwa na kura moja tu ya hapana.

Kwa upande wa nafasi nne za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa Kamisheni hiyo, daktari wa mchezo huo na Mjumbe wa Kamati ya Afya, Dk. Hadija Hamisi, ameshinda kwa kura 33 akifuatiwa na Abdallah Juma aliyepata kura 30 wakati Peter Kulunge akiwa amepata jumla ya kura 28 na Hamis Kimanga akiwa mjumbe wa mwisho katika wajumbe wa nne waliochaguliwa kwa kupata kura 24.

Baada ya ushindi huo, Palasa aliwashukuru wajumbe wa mkutano mkuu kwa kumwamini na kumchagua kwa kipindi cha miaka minne kwa ajili ya kuongoza kamisheni hiyo huku akisema kuwa atahakikisha anaendeleza mipango mizuri ya kusimamia mchezo huo, akifuata maagizo yote yaliotolewa na serikali katika kuusimamia mchezo huo.

"Kwanza nataka niwashukuru wajumbe wote kwa kuweza kunipa ridhaa ya kunichagua kuongoza kamisheni yetu kwa kipindi cha miaka minne, niwakati wa kuvunja makundi yote na kujenga au kurudisha umoja tuliokuwa nao ili tuweze kupiga hatua kubwa katika mchezo wetu wa ngumi.

"Najua tunachangamoto nyingi ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi, lakini kwa kufuata maelekezo na maagizo ya serikali kupitia sera ya michezo, ni imani yangu umoja wetu utasaidia kutupeleka mbali katika mchezo wetu," alisema Palasa.

Katibu Mkuu wa Kamisheni hiyo, George Silas, alisema: " Nashukuru kwa nafasi mliyoweza kunipa, hii inaonyesha imani kubwa juu yangu katika kuhakikisha ngumi zetu zinapiga hatua, lakini kuweza kulinda maslahi ya mabondia wetu.

"Nataka niwaambie kwamba nitafanya kazi yangu wakati wote kwa sababu mchezo wetu unahitaji muda mwingi wa kuweza kuwahudumia wadau lakini kufuata na kusikiliza yote yatakayokuwa yakielekezwa na serikali kupitia BMT," alisema Silas.

## INAWEZEKANA...



Wanachama wa timu za Joging za Smart, Talent na Wanaki za Tabata Dar es Salaam, wakiwa katika mazoezi jana, huku wakibeba mabango yenye ujumbe unaohamasisha vita dhidi ya rushwa ya ngono, ikiwa ni sehemu ya Kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', inayoendeshwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kitayosce nayo yapanda Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Kitayosce ya Tabora, imepanda Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake, baada ya kuifumua African Sports mabao 3-0 juzi, mechi ikipigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora.

Ilikuwa ni mechi ya kufa au kupona ambapo hakuna ilichokihitaji Kitayosce zaidi ya ushindi na ikafanya hivyo kwa mabao ya Moses Nassor, Fabrice Ngoy wa Ngoy na Daniel Lukandamila.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo kumaliza Ligi ya Championship ilifikisha pointi 60, hivyo kuungana na JKT Tanzania ambayo tayari ilitangulia kupanda.

Timu hiyo ilianzishwa mwaka 2014, na Kitayosce ni kifupi cha maneno ya Lugha ya Kingereza, 'Kilimanjaro Talented Youth Sports Centre.'

Kitayosce na JKT Tanzania ambao ndiyo mabingwa wa Championship msimu huu, wataanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2023/24.

Haikuwa siku nzuri kwa Pamba ya Mwanza, kwani pamoja na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Fountaine Gate Princess, imeshindwa kupanda kwa kumaliza ligi na pointi zake 59, moja nyuma ya Kitayosce na kipindi chote kulikuwa na mchuano mkali baina ya timu hizo mbili kuwania nafasi ya kupanda moja kwa moja.

Kwa matokeo hayo, Pamba iliyoshika nafasi ya tatu, itasubiri timu zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu ili kujaribu tena bahati yake kama inaweza kupanda kupitia mechi za 'play off' (mchujo).

Timu ya Mashujaa ya Kigoma nayo imepata nafasi ya kucheza mechi za mchujo, baada ya kumaliza nafasi ya nne ya ligi hiyo, ilipoibamiza Mbuni FC mabao 2-1, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Mechi zingine zilichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam, Pan African ilibugizwa mabao 3-2 dhidi ya Green Warriors, KenGold ikaichapa Biashara United 3-2 na Mbeya Kwanza ikaibamiza Copco 4-3.

# KMKM, KVZ FC vita vya ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VITA ya ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, imeendelea kupamba moto dhidi ya timu mbili KMKM SC na KVZ FC, baada ya kushinda michezo yao miwili kati ya mitano iliyobaki.

KMKM FC imefikisha alama 60 huku KVZ FC ikifikisha pointi 59 katika michezo yao ya 27 kila timu iliyocheza zikiwa zimesalia na michezo mitatu kila moja kabla ya ligi msimu huu kumaliza.

Kwa mujibu wa ratiba ya ligi hiyo KMKM, itacheza mchezo wake wa 28 dhidi ya Black Sailor Jumanne katika Uwanja wa Mau majira ya saa kumi alasiri, wakati wapinzani wao, KVZ Alhamisi wakiwa ugenini Kisiwani Pemba dhidi ya wenyeji wao, Chipukizi FC katika Uwanja wa Finya, mechi ikipigwa majira ya kumi alasiri.

Wadau wa soka visiwani hapa wanauangalia zaidi mchezo wa KMKM dhidi ya Black Sailor ambao kila timu inahitaji kupata alama tatu ili kutimiza lengo lake.

Black Sailor inahitaji alama tatu ili kuendelea na harakati za kuepuka kushuka daraja wakati KMKM ikihitaji alama tatu ili kuendelea kuzichanga karata zake za ubingwa wa Ligi Kuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema kila mchezo wanaoshuka dimbani wanautazama kama fainali kwao.

Alisema kila mchezo unaumuhimu kwao mpaka ule wa mwisho wa kumaliza ligi, kulingana na msimamo wa ulivyokuwa.

Alisema mchezo wa Black Sailor ndio mgumu zaidi kutokana na kila timu kuhitaji kupata alama tatu kutimiza lengo lake.

"Tumejipanga kupata alama tatu, lakini kama unavyojua ukicheza na timu ambayo inapambania kubaki katika ligi, basi mchezo huwa mkali kwa kuwa mpinzani wetu ili abaki Ligi Kuu anatakiwa ashinde michezo yote, hivyo tunatakiwa kucheza kwa tahadhari sana bila kuharibu mipango yetu," alisema Msimu.

**Black Sailor inahitaji alama tatu ili kuendelea na harakati za kuepuka kushuka daraja wakati KMKM ikihitaji alama tatu ili kuendelea kuzichanga karata zake za ubingwa wa Ligi Kuu.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AIKUBALIA CHELSEA

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur na Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, amekubali kuinoa Chelsea msimu huu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### MOUNT ATAKIWA KUBAKI

MAURICIO Pochettino anataka Mason Mount kubaki Chelsea, ingawa kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 24, amebakisha mwaka mmoja tu katika mkataba wake. ***(Mail)***

### ALLISTER KUNUNULIWA LIVER

LIVERPOOL iko tayari kumnunua mshindi wa Kombe la Dunia, Alexis Mac Allister, kwa dili la pauni milioni 70 kutoka Brighton na Argentina. ***(Mirror)***

### WALKER KUKOMAA CITY

MLINZI wa Manchester City na England, Kyle Walker, mwenye umri wa miaka 32, yuko tayari kukataa kutoka nje ya nchi na kukamilisha miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake katika Uwanja wa Etihad. ***(Sun)***

### KUONGEZEWA MPUNGA

MLINZI wa Manchester United na Argentina, Lisandro Martinez, mwenye umri wa miaka 25, anatarajia kuongezwa mshahara msimu huu wa majira ya joto punde tu masuala ya umiliki wa klabu hiyo yatakapotatuliwa. ***(Sun)***

### ONANA KUPIGWA BEI

KLABU ya Everton itakuwa tayari kukubali pauni milioni 50 msimu huu kwa mlinzi wa Ubelgiji, Amadou Onana, ikiwa watashushwa daraja kutoka Ligi Kuu. ***(Football Insider)***

### NEVES ATAKIWA BARCA

KLABU ya Barcelona ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves, 26. ***(Talksport)***

### BELLINGHAM AIKATAA CITY

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham, ameripotiwa kukataa kuhama kutoka Borussia Dortmund kwenda Manchester City. ***(FourFourTwo)***

### ASENSIO ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inamtaka kiungo wa kati wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio, mwenye umri wa miaka 27, na mshambuliaji wa Barcelona na Hispania, Ferran Torres, 23. ***(Sport)***

### GRAVENBERCH AWANIWA

KLABU ya Manchester United imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich na Uholanzi, Ryan Gravenberch mwenye umri wa miaka 20, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### RAIS APIGA KIMYA YA MESSI

RAIS wa Klabu ya Al-Hilal ya Saudi Arabia, Fahad Bin Saad Bin Nafel, amekataa kutoa maoni yake kuhusu uvumi wa uhamisho wa mshambuliaji wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi, 35. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO … KA MAGAZETI … AYA



# KLOPP: TUTAIZUIA MAN CITY EPL MSIMU UJAO

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp ana imani timu yake inaweza kuziba pengo la Manchester City msimu ujao.

**Kutokuwa na uwiano wa matokeo - iliishinda Manchester United mabao 7-0 na Bournemouth 9-0, lakini ikapoteza kwa Leeds United kipigo chao pekee cha nyumbani msimu huu – kumeifanya Liverpool kuachwa pointi 20 na vinara hao wa Ligi Kuu England, Man City.**

Imekuwa kawaida zaidi kwa wawili hao kusukumana hadi siku ya mwisho ya msimu, Liverpool ikishika nafasi ya pili kwa pointi mara mbili, na licha ya matatizo yao ya hivi majuzi, Klopp anatarajia huduma ya kawaida itaanza tena wakati kampeni mpya itakapoanza Agosti.

"Kuna mechi mbili kwa msimu, labda na mataji matatu, manne au matano, unapocheza na City, Arsenal na wengine," alisema kabla ya safari ya Leicester City wanaocheza nao leo, Jumatatu.

"Kuna njia milioni tano za kushinda mchezo wa soka, lazima utafute moja tu. Msimu wenye mafanikio ni kwamba uko tayari kwa michezo yote, kwamba unaweza kushinda michezo 25-isiyo ya kawaida.

"Ikiwa City, Arsenal, Chelsea, Newcastle, Tottenham, Man United wote wanahusika katika 25 basi ni bora zaidi.

"Lakini tunaweza kuunda timu ambayo inaweza kushinda michezo mingi? Ndio, tunaweza. Haikuwa juu ya kile timu zingine hufanya.

"Hatukuwa mabingwa kwa pointi mara mbili na kutakuwa na baadhi ya watu ambao wanasema ni kwa sababu hatukuwa na mchezaji huyu wakati huo. "Kupata alama 90 ni wazimu kabisa, maalum sana, na hakuna mtu anayepaswa kuchukua mambo haya kuwa ya kawaida.

"Saba bora hukaribiana zaidi, itakuwa ngumu zaidi na yenye ushindani zaidi.

"Haifanyi iwe rahisi, lakini kila mtu aliye na wazo zuri ana nafasi ya kuwa sehemu yake. Ikiwa wewe ni sehemu ya vita huko juu basi unaweza kushinda pia."

●●● Tunaweza kuunda timu ambayo inaweza kushinda michezo mingi? Ndio...

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 583

MECHI KALI
LEICESTER
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 4.58
X | 4.10
2 | 1.59

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LEAO KUONGEZA MKATABA AC MILAN

**MILAN,** Italia

TED Dimvula wakala wa Rafael Leao, ametoa taarifa kuhusu mazungumzo ya mteja wake ya kuongeza mkataba na AC Milan, akithibitisha kwamba majadiliano ni marefu.

Imeripotiwa sana siku za hivi karibuni kwamba nyota huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 23, amekubali kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na 'Rossoneri' hao wenye thamani ya takriban euro milioni saba kwa msimu, ambao unajumuisha kifungu cha kuruhusiwa kuondoka cha euro milioni 150.

Mustakabali wa Leao umekuwa gumzo kuu linaloizunguka Milan msimu huu na klabu itatamani sana kurasimisha mkataba wake mpya hivi karibuni, ikitaka kuepusha vitisho vyovyote vinavyoweza kutokea katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Akizungumza na Foot kuhusu mkataba wa Leao na Milan, Mercato Dimvula alithibitisha kuwa kazi inaendelea kukamilisha mpango huo.

Dimvula alisema; "Ndio, tunajadiliana na Milan kuongeza mkataba wa Rafael. Kama ilivyo kwa ripoti yoyote ya ukubwa huu, majadiliano ni marefu na kila undani ni muhimu. Tunapanga kukutana saa chache zijazo kuhusu suala hili na uongozi wa klabu."

Kwa Rafael, Milan ni klabu ambayo ni muhimu na matarajio yake hayajabadilika tangu awasili hapa. Anataka kucheza chini ya kocha ambaye anajua jinsi ya kumwendeleza, na anataka kucheza Ligi ya Mabingwa," alisema wakili huyo.

Leao, ambaye alikosa mechi ya mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Inter kutokana na jeraha, amefunga mabao 13 na kutoa asisti 13 katika mechi 44 katika michuano yote msimu huu.



# Pochettino aikubalia Chelsea

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kukaribia kumteua Mauricio Pochettino kuwa kocha wao mpya.

'The Blues' hao wamekubaliana na kocha huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur, kwa mujibu wa ripoti katika vyombo mbalimbali vya habari vya Ulaya.

Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 51, atachukua mikoba ya kocha wa muda Frank Lampard mwishoni mwa msimu.

Hakujakuwa na uthibitisho kutoka kwa klabu, lakini Shirika la Habari la PA limewasiliana na Chelsea.

Chelsea inatafuta kocha mpya wa muda baada ya kumtimua Graham Potter ambaye alidumu kwa muda wa miezi saba pekee ya mkataba wake wa miaka mitano aliyosaini Aprili mwaka huu.

Lampard, ambaye hapo awali aliiongoza klabu hiyo kuanzia msimu wa 201 2021, aliletwa kwa mud lakini mapambano ya tim hiyo yameendelea na w nashika nafasi ya 11 kweny Ligi Kuu.

Pochettino, ambaye a iongoza Tottenham kweny fainali ya Ligi ya Mabingw Ulaya mwaka 2019 kabla y kutimuliwa baadaye mwal huo, anapatikana baada y kuondoka Paris St Germa msimu uliopita wa majira y joto.

## HABARI MICHEZO


,071,860

JACKPOT

Lorem ipsum

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/05/23 | 18:00 | Marumo Gallants FC vs Young Africans | 2.50 | 3.30 | 2.50 |
| 02. 17/05/23 | 19:00 | AEL Limassol vs Karmiotissa | 2.69 | 3.27 | 2.48 |
| 03. 17/05/23 | 19:30 | IF Karlstad Fotboll vs Hammarby Talang FF | 2.29 | 3.59 | 2.53 |
| 04. 17/05/23 | 20:00 | Ankaragucu vs Antalyaspor | 2.28 | 3.41 | 2.83 |
| 05. 17/05/23 | 21:30 | National Bank vs Ismaily SC | 2.39 | 2.95 | 3.05 |
| 06. 17/05/23 | 21:35 | Airdrieonians vs Hamilton | 2.45 | 3.23 | 2.66 |
| 07. 18/05/23 | 02:00 | Sport Recife vs Sao Paulo | 2.80 | 2.96 | 2.47 |
| 08. 18/05/23 | 02:30 | Toronto FC vs NY Red Bulls | 2.37 | 3.26 | 2.94 |
| 09. 18/05/23 | 03:30 | America Mineiro MG vs Internacional | 2.56 | 3.01 | 2.65 |
| 10. 18/05/23 | 22:00 | AZ Alkmaar vs West Ham | 2.68 | 3.24 | 2.51 |
| 11. 18/05/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Juventus | 2.35 | 3.14 | 2.98 |
| 12. 19/05/23 | 03:00 | Arsenal Sarandi vs Independiente | 2.90 | 2.85 | 2.47 |
| 13. 19/05/23 | 19:00 | Hillerod vs HB Koge | 2.44 | 3.13 | 2.62 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 15/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4166 | FC Minaj vs SC Dnipro 1 | 7.18 | 4.41 | 1.34 |
| 13:15 | 5249 | FC Bulleen Lions vs Preston Lions | 2.57 | 3.63 | 2.30 |
| 14:35 | 5321 | Beijing Guoan vs Nantong Zhiyun | 1.44 | 3.90 | 6.36 |
| 15:00 | 1315 | Kolos Kovalivka vs Oleksandria | 2.94 | 3.14 | 2.22 |
| 15:00 | 3296 | Arba Minch Kenema vs Welayta Dicha FC | 5.09 | 3.17 | 1.70 |
| 15:00 | 5407 | Van Yerevan vs Ararat Yerevan | 2.39 | 2.85 | 2.70 |
| 15:30 | 4988 | Gareji vs Merani Martvili | 2.20 | 3.32 | 2.91 |
| 16:00 | 2369 | Polisi Tanzania vs Mtibwa Sugar | 2.21 | 2.80 | 3.34 |
| 17:00 | 3210 | Neftchi Fargona vs Bunyodkor | 2.00 | 3.05 | 3.20 |
| 17:00 | 3472 | Metallurg Bekabad vs Nasaf Qarshi | 4.90 | 3.40 | 1.55 |
| 18:00 | 1229 | Artsakh vs Pyunik Yerevan | 10.36 | 5.39 | 1.22 |
| 18:00 | 2280 | Hadiya Hosahina FC vs Wolkite City FC | 1.84 | 3.16 | 4.14 |
| 18:00 | 2968 | Sloboda Tuzla vs Siroki Brijeg | 2.38 | 2.94 | 2.94 |
| 18:00 | 5400 | Oman Club vs Al Nasr Salalah | 2.43 | 2.80 | 3.01 |
| 18:00 | 5810 | AL Musanaa vs Al Suwaiq | 4.57 | 3.22 | 1.75 |
| 19:00 | 1234 | Spartak Subotica vs Mladost Lucani | 1.84 | 3.29 | 3.80 |
| 19:00 | 1302 | Al Khaleej Club vs Al Taawon | 2.87 | 3.46 | 2.31 |
| 19:00 | 2016 | JK Tabasalu vs Flora II | 2.54 | 3.83 | 2.41 |
| 19:00 | 3106 | Al Raed Club vs Dhamk | 2.46 | 3.40 | 2.71 |
| 19:00 | 3418 | Al Masry Club vs El Daklyeh | 1.78 | 3.27 | 4.62 |
| 19:00 | 4096 | AL Baten vs AL Faiha | 2.59 | 3.36 | 2.58 |
| 19:00 | 5419 | Radnicki Nis vs Javor Ivanjica | 1.61 | 3.49 | 4.93 |
| 19:00 | 5913 | Najran SC vs AL Khlood | 2.88 | 2.83 | 2.45 |
| 19:25 | 1359 | Jeddah Club vs Al Faisaly (KSA) | 4.10 | 3.18 | 1.81 |
| 19:30 | 4523 | FC Martigues vs Nancy | 2.22 | 3.26 | 3.05 |
| 20:00 | 1296 | Kristianstads FF vs Hassleholms IF | 3.01 | 3.32 | 2.15 |
| 20:00 | 1774 | Warta Poznan vs Radomiak Radom | 2.31 | 3.03 | 2.88 |
| 20:00 | 2312 | Erzgebirge Aue vs Borussia Dortmund II | 2.80 | 3.43 | 2.32 |
| 20:00 | 3091 | Trelleborgs FF vs Ostersunds | 2.59 | 3.30 | 2.63 |
| 20:00 | 3641 | Randers vs Viborg FF | 2.68 | 3.29 | 2.51 |
| 20:00 | 4033 | GIF Sundsvall vs Helsingborg | 2.58 | 3.26 | 2.66 |
| 20:00 | 5250 | Oliveirense vs SCU Torreense | 2.24 | 3.27 | 2.91 |
| 20:10 | 2942 | AIK Football vs IFK Goteborg | 1.89 | 3.24 | 3.65 |
| 20:20 | 4818 | Hajer Club vs Al Jabalain | 2.44 | 2.85 | 2.65 |
| 20:30 | 2858 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Beer Sheva | 2.13 | 3.34 | 2.93 |
| 20:30 | 5131 | Maccabi Netanya vs Maccabi Haifa | 4.93 | 3.95 | 1.53 |
| 21:00 | 4407 | CS Union Huaral vs FC Carlos Stein | 1.65 | 3.50 | 4.63 |
| 21:30 | 1532 | Al Fateh (KSA) vs AL Adalh | 1.68 | 4.00 | 4.48 |
| 21:30 | 3060 | Enppi Club vs El Ittihad Alexandria | 2.67 | 2.97 | 2.67 |
| 21:30 | 3738 | Barracas Central vs Central Cordoba | 2.48 | 3.01 | 2.75 |
| 21:30 | 4884 | Union Santa Fe vs Sarmiento Junin | 2.08 | 3.10 | 3.36 |
| 21:45 | 1357 | Derry City vs Dundalk FC | 1.59 | 3.59 | 4.93 |
| 21:45 | 2582 | Sampdoria vs Empoli | 3.01 | 3.31 | 2.20 |
| 21:45 | 3533 | Annecy FC vs Le Havre | 3.45 | 3.15 | 2.07 |
| 22:00 | 2069 | Leicester vs Liverpool | 4.58 | 4.10 | 1.59 |
| 22:00 | 3806 | Betis vs Rayo Vallecano | 1.86 | 3.40 | 3.86 |
| 22:00 | 4163 | Levante vs UD Ibiza Eivissa | 1.30 | 4.71 | 9.03 |
| 22:00 | 5084 | Shamrock Rovers vs St Patricks | 1.59 | 3.59 | 4.93 |
| 22:15 | 2195 | GD Estoril vs FC Arouca | 2.49 | 3.11 | 2.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# YANGA, UNICEF WAIFIKIA JAMII KUPITIA ISHI KIJANJA

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kupitia Ofisi ya Afya ya Mkoa kwa pamoja wameendelea kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa mlipuko wa kipindupindu.

**Kampeni hii ya siku nne iliyopewa jina la 'Ishi Kijanja', imelenga kueneza uelewa juu ya magonjwa ya kuhara na kutapika ikiwamo kipindupindu na kuhimiza hatua za kujikinga ili kulinda afya za wananchi.**

Akizungumza na Waandishi wa Habari, Mtendaji wa Yanga, Andre Mtine, alisema siku ya kwanza ya kampeni hiyo ilianzia katika maeneo ya Ilala na Buguruni, ambapo viongozi wa Yanga, UNICEF, na Wizara ya Afya walishirikiana kutoa elimu kuhusu kipindupindu na wananchi wengi walihudhuria na kupata fursa ya kusikiliza na kujifunza kuhusu ugonjwa huo hatari.

Alisema wataalamu wa afya walitoa maelezo ya kina juu ya dalili za kipindupindu, njia za maambukizi, na hatua za kujikinga. Pia, walisisitiza umuhimu wa usafi wa mazingira na matumizi ya maji salama.

Aidha, hawakuishia hapo ila siku iliyofuata alisema walielekea Mwananyamala, Tandale, na Kigogo Luhanga ambayo ni maeneo ya makazi ya watu wengi, jambo ambalo kutoa elimu huko lilikuwa na umuhimu mkubwa. Wananchi walisikiliza kwa makini na kuuliza maswali yanayohusiana na kipindupindu.

Alisema kwa ushirikiano wa karibu na viongozi wa klabu ya Yanga, ambao ni nguzo muhimu katika jamii, ujumbe wa kampeni uliwafikia watu wengi na kuongeza uelewa wa jinsi ya kuzuia kipindupindu.

Kiongozi huyo alisema siku ya tatu, Kampeni ya Ishi Kijanja, ilielekea Mburahati, Mabibo, Manzese na Simu 2000. Maeneo hayo pia yalikuwa na idadi kubwa ya watu, na jitihada za kuelimisha juu ya kipindupindu zilipokelewa vizuri. Wananchi walifurahishwa na jitihada za Klabu ya Yanga katika kuwafikia na kuwaelimisha kuhusu afya yao na afya ya jamii kwa ujumla.

"Siku ya nne na ya mwisho ilikuwa ni Jumatano Mei 10, mwaka huu kuanzia asubuhi kwenye Uwanja wa Mkapa Jijini Dar es Salaam wakati timu hiyo, ikjijiandaa na mchezo wa kwanza wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini."

Aidha, Mtine alisema elimu hiyo ilitolewa kwa mashabiki wote waliofika uwanjani hapo, na kikubwa wametakiwa kuchukua hatua kuelekeza na kuongeza uelewa endelevu kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa yote yanayosambazwa kwa maji yanayosababishwa na aina ya vijidudu ikiwa ni pamoja na mlipuko wa kipindupindu.

Alizitaja hatua zitakazochukuliwa kuwa ni pamoja upatikanaji na matumizi ya majisafi ya kunywa kwa kuchemsha na kutibu maji kwa klorini.

Pili kushughulikia hali duni ya usafi wa mazingira na usafi kibinafsi, hiyo ikijumuisha kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya choo, uondoaji wa taka za maji na taka za viwandani. Tatu kuboresha usafi wa kibinafsi na usafi na usalama sahihi wa chakula, kunawa mikono kwa maji safi na tiririka kabla ya kula/ kuandaa chakula cha mtoto kabla ya kumlisha pamoja na kuhakikisha maji ya kunywa yanahifadhiwa kwenye chombo safi kilichofunikwa muda wote.

"Kampeni ya Ishi Kijanja imekuwa moja ya jitihada muhimu zaidi za Klabu ya Yanga katika kushiriki katika maendeleo ya kijamii. Tumeona umuhimu wa kuunganisha nguvu zetu na mashirika kama UNICEF na serikali katika kuelimisha jamii juu ya kipindupindu. Kupitia kampeni hii, tumewafikia maelfu ya watu na kutoa elimu muhimu ambayo itawawezesha kuchukua hatua za kujikinga na kuzuia ugonjwa huo. Pia, kwa kuweka ndoo za kunawia mikono, sabuni na vitakasa mikono (sanitizers) katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, tulilenga kutoa mfano mzuri kwa mashabiki wetu na umma kwa ujumla juu ya umuhimu wa usafi wa mikono," alisema.

## Kapombe atangaza nia kujifunga tena Simba

INATOKA UK. 23

tayari wasimamizi wake wameanza mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo.

Kapombe alisema: "Kwa sasa sifikirii kwenda klabu yoyote zaidi ya kubaki Simba, mkataba wangu unaelekea ukingoni na wawakilishi wangu wanaendelea na mazungumzo na viongozi, naamini tutafikia makubaliano mazuri," alisema.

Endapo mazungumzo hayo yakikamilika, Kapombe atakuwa mchezaji wa pili kuongeza mkataba mpya baada ya beki kisiki wa kati wa timu hiyo, Henock Inonga, kufanya hivyo Desemba mwaka jana.




Nasreddine Nabi.

## *CAF yabariki Yanga fainali*

INATOKA UKURASA 24

bu tunahitaji ushindi ili tunapocheza dhidi ya Marumo Gallants tusiwe na presha kubwa juu ya kutetea ubingwa na kuwaza mechi ya nusu fainali ya FA," alisema Nabi.

Aliongeza: "Nimeshaongea na wachezaji wangu kwamba furaha na sherehe za ubingwa zimeishia uwanjani na kuwataka kusahau yote, kwa kuwataka kutuliza akili na nguvu zao katika mechi yetu ya marudiano Afrika Kusini".

Kwa upande wa Rais wa Yanga, Hesri Said, alisema malengo yao ni kuona wanashinda kila mechi, na kwamba hili wamefanikiwa na kwa kutwaa mataji ya Ngao ya Jamii sasa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na sasa wanataka kwenda fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na FA Cup.

# Michezo

Jumatatu Mei 15, 2023

Nipashe




Pochettino aikubalia Chelsea

UKURASA 22




Wachezaji wa Yanga kabla ya kuelekea Afrika Kusini jana katika mchezo wa nusu fainali ya pili ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants, wakiwa katika kampeni yao kabambe ya 'Ishi Kijanja', ambayo ni maalum kwa kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa mlipuko wa kipindupindu. Katika kampeni hiyo wanashirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kupitia Ofisi ya Afya ya Mkoa. **HABARI UK. 23. MPIGAPICHA WETU**

# CAF YABARIKI YANGA FAINALI KWA MKAPA

**Na Saada Akida**

## ●●● Serikali yatoa tamko ikiisubiria kama itafuzu, yatua Sauzi kumaliza kazi, Nabi asema...

WAKATI Yanga wakitua salama Afrika Kusini jana baada ya kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu Bara juzi, Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limekubali kusogeza mbele tarehe ya kuanza kufanyika ukarabati katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ili kuipa fursa ya kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika uwanjani hapo endapo itafuzu.

**Yanga ambayo juzi ikiwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ilifanikiwa kutetea ubingwa wake wa Ligi Kuu Bara baada ya kuifunga Dodoma Jiji FC mabao 4-2, hivyo kufikisha pointi 74, ambazo haziwezi kufikiwa timu yoyote katika ligi hiyo msimu huu, imetua Afrika Kusini tayari kwa mchezo wao wa mkondo wa pili wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji, Marumo Gallants.**

Katika mchezo wa mkondo wa kwanza uliopigwa wiki iliyopita Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ilishinda mabao 2-0, hivyo keshokutwa, Jumatano itashuka katika Uwanja wa Royal Bafokeng uliopo Rustenberg, Afrika Kusini, ikihitaji sare yoyote ama kutokubali kufungwa zaidi ya bao 1-0 au kupata ushindi wowote ili kutinga fainali.

Na kutokana na Yanga kuwa katika nafasi ya kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho, Caf wametua barua Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuridhia kusogeza mbele tarehe ya kuanza ukarabati mkubwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili ya michuano ya Super League, ambayo Simba itashiriki, ili kuipa fursa Yanga kuutumia uwanja huo ikiwa itafanikiwa kutinga hatua ya fainali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu, akizungumza na Nipashe jana, alisema walipanga kuufunga uwanja huo mapema mwezi huu, lakini wameamua kusogeza mbele matengenezo hayo kwa kipindi cha mwezi mmoja zaidi baada ya kukubaliana na CAF kutokana mafanikio ya Yanga kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Nataka niwaambie tulikubaliana kuufunga uwanja mwezi huu ili kupisha matengenezo ambayo tumekubaliana ambayo kawaida yanachukua hadi miezi minne.

"Lakini tumeongea na wenzetu wa CAF juu ya suala la Yanga na tumekubaliana kulipeleka mbele kwa kipindi cha mwezi mmoja ili kuacha nafasi ya mchezo wa kwanza wa fainali ikiwa Yanga itafanikiwa kwenda fainali ili ichezwe hapa hapa kabla ya kwenda kwenye mchezo wa marudiano, nafikiria itakuwa ni Juni 3, mwaka huu," alisema Yakubu.

Wakati hayo yakiendelea, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema tayari amewataka wachezaji wake kusahau sherehe za ubingwa baada ya kuifunga Dodoma Jiji FC juzi na badala yake kuelekeza akili zao katika dakika 90 za pili dhidi ya Marumo Gallants keshokutwa, Jumatano.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu dhidi ya Dodoma Jiji kwa sababu inapigania kujinusuru kushuka chini na Yanga ikihitaji matokeo mazuri ili kutokuwa na presha kuelekea mchezo wao wa marudiano dhidi ya Marumo Gallants.

"Haukuwa mchezo rahisi wachezaji wamepambana, nawapongeza vijana wangu, watu wangu wa benchi la ufundi, viongozi na mashabiki ambao wamekuwa na sisi kila hatua hadi kutimiza malengo yetu ya kutetea taji letu la ubingwa.

"Hii mechi ambayo ilikuwa muhimu sana kwetu kwa saba-

INAENDELEA UKURASA 23

# Kapombe atangaza nia kujifunga tena Simba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inakisuka mapema kikosi chake kuelekea msimu ujao, uongozi wa Klabu ya Simba umeanza kwanza kuboresha mikataba ya wachezaji wao inayotamatika mwishoni mwa msimu huu kabla ya kuanza kushusha vifaa vipya, imeelezwa.

Hii ni baada ya msimu huu tena kutoambulia taji lolote huku wakishindwa kufikia lengo lao la kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, walilokuwa wamejiwekea, jambo ambalo limewaamsha na kuahidi usajili mkubwa.

Tayari Yanga imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu, hivyo Simba haina nafasi tena ya kubeba taji hilo huku ikiondoshwa kwenye Kombe la FA katika hatua ya nusu fainali na Azam FC, lakini pia ikikomea robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutolewa na mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Wydad Casabanca ya Morocco kwa mikwaju ya penalti 4-3, hiyo ikitokana na kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Hata hivyo, Simba itakuwa timu pekee katika Ukanda wa Afrika Mashariki, itakayoshiriki michuano mipya na mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu Afrika, Super League, inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Oktoba mwaka huu ikishirikisha klabu nane kubwa, jambo ambalo wamesema wanataka kujipanga mapema.

Ofisa Mtendaji wa Simba, Imani Kajula, amesema watafanya usajili mkubwa wa wachezaji wenye viwango vya hali ya juu kuelekea msimu ujao na wakati akitoa kauli hiyo, jana beki wa kulia, Shomari Kapombe, alisema yupo kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya.

Katika mahojiano yake jana na Meneja Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, Kapombe alisema mkataba wake unafika ukingoni mwishoni mwa msimu huu na

INAENDELEA UKURASA 23



9 770856 541002 >